# Imani za Shiite na Vitendo vilielezea

Karatasi hizi za ukweli zimechukuliwa kutoka

www.al-islam.org/nutshell

Title : Islamic Factsheets
Published By : Ja'fari Propagation Centre
94, Asma Manzil, Room No. 10, Bazar Road,
Opp. Khoja Masjid, Bandra (W),
Mumbai – 400050. Tel.: 2642 5777.
E-mail: jpcbandra@yahoo.com, jpconline.org
Year : May 2013

# Orodha ya Yaliyomo


Kwa nini kufuata familia (Ahlul-bayt) ya Mtume (s.a.w.)?........3

Wasemavyo wasio Waislamu juu ya…........7

Je Mtume (s.a.w.w.) aliteua wasii?........11

Kwa nini Shi'ah?........15

*Rafidi* - Wapokezi wa Kishia katika........19

Je Mashia wanaamini Qur'an nyingine?........24

Ni nani hawa Maimamu kumi na wawili wa Mtume (s.a.w.w)?........28

Umuhimu wa Ijtihad na Taqlid........32

Jinsi ya kutawadha na kufanya *Tayammum*........*36*

Kwa nini Shi'ah huacha mikusanyiko ya swala ya *Tarawih?*........*40*

Kwa nini Waislamu wana utaratibu Maalum wa Mavazi?........44

Kwa nini Mashia wanakusanya Swala?........49

Jinsi ya kuswali Swala za kila siku........53

Kwa nini Mashia wanasujudu juu ya *Turbah*?........58

Wasio Waislamu wanasema ninijuu ya…**Muhammad.**........62

Wasiokuwa Waislamu wanasema nini juu ya …**Ali**........66

Hutuba ya herufi za kiarabu Zisizo na nukta........70

Wanayosema wasio Waislamu juu ya…**Husein**........73

Kutafuta Elimu........77

Mapambano dhidi yaNafsi........81

Hasira........85

*“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba ya Mtume* **(Ahlul-Bayt)** *na kuwatakasa kabisa.”*
[Aya ya Utakaso, Qur’an 33:33]

Mtume Muhammad (s.a.w.) aliulizwa na Maswahaba wake:

“Kwa namna gani tukutakie rehema?” … Akajibu:

“Semeni: ‘*Ewe Mola! Mtakie rehma Muhammad na familia yake, kama ulivyomtakia rehma Ibrahim na familia yake, hakika Wewe uko mwenye kuhimidiwa, Mtukufu*.’”
[*Sahih al-Bukhari*, Juz. 4, Kitabu 55, Hadith Na. 589]

# Kwa nini kufuata familia (Ahlul-bayt) ya Mtume (s.a.w.)?

Shia wanaammini kwamba tirathi mbili za Mtume Muhammad (s.a.w.) ni Qur'an na *Ahl ul-Bayt* (watu maalum katika familia yake). *Ahlul-Bayt* ndio msingi wa kupata *Sunnah* sahihi za Mtume (s.a.w.). Ni kwa kupata maelezo kutoka katika misingi hii miwili tu ndipo mtu anaweza kuwa na matumaini ya kupata uongofu.

**Ni kina nani waliokuwamo katika Ahlul-Bayt?**

Imeonyesha kwamba familia ya Mtume (s.a.w.) mara kwa mara hutajwa kama *Ahlul-Bayt*, *'Itrah* na *Aal* – ikiwa ni pamoja na bintiye Fatima al-Zahra', mumewe Imam 'Ali, na watoto wao Imam al-Hasan na al-Huseyn (a.s.). Ikiwa ni familia ya watu watano, Mtume (s.a.w.) akiwa ni kiongozi wao, ambao walikuwa hai wakati Aya za Qur'an zikishuka kuhusu sifa zao kwa Mtume (s.a.w.). Hata hivyo, maimamu tisa kutoka kwa wajukuu wa Imam Husein (a.s.) pia ni katika wateule wa familia hii, wa mwisho akiwa ni Imam Mahdi (a.s.). Mtume (s.a.w.) amesema:

- "Mimi na 'Ali na al-Hasan na al-Huseyn na **wajukuu tisa wa al-Huseyn** ni watakatifu na wenye heshima." [al-Juwayni, *Fara'id al-Simtayn*, (Beirut, 1978), Uk. 160. Fahamu kwamba heshima ya al-Juwayni kama Mwanachuoni mkuu wa Hadith imethibitishwa na al-Dhahabi katika *Tadhkirat al-Huffaz*, Juz. 4, Uk. 298, na pia Ibn Hajar al-'Asqalani katika *al-Durar al-Kaminah*, Juz. 1, Uk. 67]
- "Mimi ni mkuu wa Mitume na 'Ali ibn Abi Talib ni mkuu wa mawasii, na baada yangu mawasii wangu watakuwa ni kumi na wawili, wa mwanzo wao akiwa ni 'Ali ibn Abi Talib na wa mwisho ni al-Mahdi." [al-Juwayni, *Fara'id al-Simtayn*, Uk. 160]
- "Al-Mahdi ni katika sisi **Ahlul-Bayt**" na "al-Mahdi atakuwa ni katika familia yangu, katika wajukuu wa Fatima" [Ibn Majah, *al-Sunan,* Juz. 2, Uk. 519, Na.s 4085-6; Abu Dawud, *al-Sunan*, Juz. 2, Uk. 207]

**Vipi kuhusu wakeze Mtume (s.a.w.)?**

Aya ya utakaso: "*Hakika Mwenyezi Mungu anataka…* " ilishuka wakati Mtume (s.a.w.) yuko kwenye nyumba ya mkewe Umm Salama (Mungu amuelee radhi); Mtume (s.a.w.) akamwita al-Hasan, al-Huseyn, Fatima na 'Ali, na akawakusanya wote hao na kuwafunika ndani ya shuka. Kisha akasema, **"Ewe Mwenyezi Mungu, hawa ndio watu wangu wa nyumbani, watakase na uchafu wowote na uwatakase kabisa**." Umm Salama akasema, "Je mimi ni pamoja nao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume (s.a.w.) akasema, "**Kaa hapo ulipo, wewe u katika kheri**."

- al-Tirmidhi, *al-Sahih*, Juz. 5, Kurasa 351 na 663
- al-Hakim *al-Naysaburi*, al-Mustadrak *`ala al-Sahihayn*, Juz. 2, Uk. 416. Amesema kwamba hii ni *sahih* kulingana na al-Bukhari
- al-Suyuti, *al-Durr al-Manthur,* Juz. 5, Uk. 197

Mwanzo wa Aya 33:33 na maelezo yaliyofuata yawazungumzia wake za Mtume (s.a.w.) kama inavyoonyesha wazi dhamiri ya wanawake, lakini katika Aya ya Utakaso dhamiri yabadilika na kuwa ya kiume au ya kike na kiume. Hii pia yaonyesha kuwa wahyi pekee unaelezea watu tofauti.

**Kwa maelezo zaid juu ya Uislamu sahihi kama ulivyoelezwa na Ahlul Bayt, tazama Tovuti hii:**

http://al-islam.org/faq/

**Turathi ya Mtume Muhammad (s.a.w.)**

**"Mimi niko karibu na kuitikia mwito (wa mauti). Hakika nawaachia vitu wiwili vizito vya thamani (*thaqalayn*): Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahlul Bayt wangu. Hakika viwili hivyo havitatengana mpaka vinijie kwenye hodhi."**

Hadith hii sahihi ya Mtume Muhammad (s.a.w.) imepokewa na zaidi ya Maswahaba wake thelathini na kunakilwa na Wanavyuoni wengi wa Kisunni, miongoni mwao ambao ni mashuhuri ni pamoja na:

- al-Hakim al-Naysaburi, *al-Mustadrak `ala al-Sahihayn* (Beirut), Juz. 3, Kurasa 109-110, 148, na 533). Huyu amesisitiza kuwa Hadith hii ni *sahih* kulingana na al-Bukhari na Muslim; al-Dhahabi amethibitisha hukmu yake
- Muslim, *al-Sahih*, (Tafsiri ya Kiingereza), Kitabu 031, Na. 5920-3
- al-Tirmidhi, *al-Sahih*, Juz. 5, Kurasa 621-2, Na.s 3786 na 3788; Juz. 2, Uk. 219
- al-Nasa'i, *Khasa'is'Ali ibn Abi Talib*, Hadith Na. 79
- Ahmad b. Hanbal, *al-Musnad*, Juz. 3, Kurasa 14, 17, 26; Juz. 3, Uk. 26, 59; Juz. 4, Uk. 371; Juz. 5, Kurasa 181-2, 189-190
- Ibn al-'Athir, *Jami` al-'usul*, Juz. 1, Uk. 277
- Ibn Kathir, *al-Bidayah wa al-nihayah,* Juz. 5, Uk. 209. Akimnukuu al-Dhahabi na amesema kwamba *Hadith* hii ni *sahih*.
- Ibn Kathir, *Tafsir al-Qur'an al-'Adhim* , Juz. 6, Uk. 199
- Nasir al-Din al-Albani, *Silsilat al-AHadith al-Sahiha* (Kuwait: al-Dar al-Salafiyya), Juz. 4, Kurasa 355-8. Yeye ametaja mapokezi mengi ambayo anayaona kuwa ni yenye kuaminika.

Kuna mapokezi mengi ya *Hadith* ambayo hatuwezi kuyataja hapa.

**Je, Mtume (s.a.w.) hakusema: "Nawaaachia Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah zangu"?**

Suala hili lina utata. Ukweli ni kwamba hapana msingi wa ukweli wa kutegemewa wa kauli hii katika ile hotuba yake ya mwisho ya Mtume (s.a.w.) Kwa hakika haimo kabisa katika kitabu chochote miongoni mwa vitabu sita vya Sihah!! Maelezo katika kitabu cha Malik, *al- Muwatta'*, cha Ibn Hisham, *Sirat Rasul Allah*, na kutoka kwake katika *Tarikh* ya al-Tabari, mapokezi yote ya hawa hayana mlolongo wa uliokamilika wa mapokezi, kwani baadhi ya msururu huo umekatika! Isitoshe mapokezi mengine ambayo yana mlolongo wa mapokezi (*isnad*) – ambao pia ni wachache mno – wote una wapokezi ambao, kiujumla, huchukuliwa – na Wanavyuoni wakubwa wa Sunii wa elimu ya *Rijal* -kuwa si waaminifu. Ukweli huu ulio wazi unaweza kuthibitishwa kwa kurejea vitabu vifaavyo vinavohusika na uwanja huo kwa wale wanaopenda kufanya utafiti.

Ni wazi kwamba hakuna apendekezaye kwamba *Sunnah* za Mtume (s.a.w.) zisifuatwe. Bali kama illivyoelezwa hapo awali kwamba Mtume (s.a.w.) aliwataka Waislamu kuwarejea Ahlu-Bayti wake wakiwa wao ndio waaminifu, watakatifu, na kwa hali yoyote ndio msingi wa *Sunnah zake.*

**Kuna jambo gani mahsusi kuhusu familia ya Mtume (s.a.w.)?**

Wakati Aya ii iliposhuka: *"Sema ewe Muhammad, siwaombi malipo yoyote (Kwa Mtume kuleta ujumbe huu) ila muwapende watu wangu wa karibu*," Waislamu walimuuliza Mtume (s.a.w.): "Ni kina nani hao jamaa zako wa karibu ambao imetupasa tuwapende?" **Akajibu, "Ali, Fatima, na watoto wao wawili.**"

- al-Hakim *al-Naysaburi, al-Mustadrak `ala al-Sahihayn*, Juz. 2, Uk. 444
- al-Qastallani, *Irshad al-Sari Sharh Sahih* al-Bukhari, Juz. 7, Uk. 331
- al-Suyuti, *al-Durr al-Manthur*, Juz. 6, Kurasa 6-7
- al-Alusi al-Baghdadi, *Ruh al-Ma'ani*, Juz. 25, Kurasa 31-2

Daraja ya uaminifu na heshima ya Ahlul-Bayt waliyokuwa nayo imethibitishwa zaidi na Qur'an wakati wa majadiliano na Wakristo wa kutoka Najran. Wakati Aya ii iliposhuka: "*Watakaokuhoji (sasa) baada ya kukufikia ilimu, waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake wetu na wanawake wenu, na sisi na nyinyi, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo."* (3:61), **Mtume (s.a.w.) aliwaita 'Ali, Fatima, al-Hasan na al-Huseyn na akasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, hawa ndio familia yangu (*Ahli*)**'.

- Muslim, *al-Sahih*, (Tafsiri ya Kiingereza), Kitabu 031, Na. 5915
- al-Hakim al-Naysaburi, *al-Mustadrak `ala al-Sahihayn*, Juz. 3, Uk. 150. Amesema kwamba hii ni *sahih* kulingana na al-Bukhari na Muslim
- Ibn Hajar al-'Asqalani, *Fat-h al-Bari Sharh Sahih al-Bukhari*, Juz. 7, Uk. 60
- al-Tirmidhi, al-Sahih, *kitab al-manaqib*, Juz. 5, Uk. 596
- Ahmad b. Hanbal, *al-Musnad*, Juz. 1, Uk. 185
- al-Suyuti, *History of Khalifas Who Took The Right Way*, (London, 1995), Uk. 176

**Je yatosha kuonyesha heshima kwa Ahlul-Bayt?**

Je yatosha kuonyesha heshima kwa Qur'an? Hakika Waislamu ni lazima waifuate ikiwa ni Msingi wa mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika mambo yao *yote*. Mtume Muhammad (s.a.w.) aliacha vitu viwili hivi ikiwa ni tirathi kwa Waislamu, na akaahidi kwamba havitatengana mpaka siku ya Kiyama. **Mtume (s.a.w.) alipoviweka pamoja vitu hivi viwili, Qur'an na Ahlul Bayt alikuwa akitwambia kwamba tusiviheshimu tu bali tuchukue ufananuzi wa mafunzo ya Kiislamu, matendo, *Hadith* na *tafsir* kutoka kwenye viwili hivyo.**

"**Tazama! Ahlul-Bayt wangu ni kama jahazi la (Nabii) Nuh, atakayelipanda basi ataokoka, na atakayeliepuka ataangamia".**

- al-Hakim al-Naysaburi, al-Mustadrak *`ala al-Sahihayn*, Juz. 3, p. 151 na Juz. 2, Uk. 343. Yeye amesema kwamba hii ni *sahihi* kulingana na maelezo ya Muslim
- al-Suyuti, *al-Durr al-Manthur*, Juz. 1, Kurasa 71-72

Ibn Hajar al-Makki, *al-Sawa'iq al-Muhriqa*, Uk. 140. Huyu amesema kwamba Hadith hii imepitia mlolongo mrefu wa mapokezi unaoshikana imara.

*“Ambao husikiliza kauli (nyingi zinazosemwa), wakazifuata zile zilizo njema. Hao ndio aliowaongoza Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili.”*
(Qur'an 39:18)

## Wasemavyo wasio Waislamu juu ya…

# Uislamu

## DINI INAYOKUA KWA HARAKA ZAIDI ULIMWENGUNI

Huuni mkusanyiko wa nukuu fupifupi kutoka kwa watu mbalimbali mashuhuri wasiokuwa Waislamu, wakiwamo wasomi, waandishi, wanafalsafa, washairi, wanasiasa na wanaharakati wa Kimashariki na wa Kimagharibi. Tujuavyo ni kwamba hakuna hata mmoja mwao aliyewahi kuwa Mwislamu. Hivyo basi, maneno haya yanaonyesha maoni yao binafsi juu ya mitazamo mbalimbali wa dini ya Kiislamu.

## Sarojini Naidu

*(1879-1949) Mwanamke huyu ni Mwandishi, Mshairi, ambaye pia alikuwa ni mmoja mwa viongozi mashuhuri India kabla ya uhuru. Rais wa chama cha Indian National Congress na ni Gavana wa kwanza mwanamke baada ya India kupata uhuru. Amesema:*

- "Uadilifu ni moja kati ya maadili mazuri zaidi ya Uislamu, kwa kuwa nisomapo Qur'an nakuta kwamba misingi hii maisha, si nadharia tu bali ni maadili hasa ya kivitendo katika maisha ya kila siku yanayofaa kwa ulimwengu mzima."

- "Ilikuwa ni dini ya kwanza iliyohubiri na kutekeleza kwa vitendo demokrasia, kwani kunapoadhiniwa na waaabuduo wanapokusanyika, ndipo demokrasia ya kiislamu inapodhihirika mara tano kwa siku, pale mfalme na mkulima wanapoinama bega kwa bega na kusema: "Mwenyezi Mungu pekee ndiye Mkuu." Nimekuwa nikiathiriwa mara kwa mara na umoja huu wa kiislamu usiogawanyika unaomfanya mtu moja kwa moja kumpenda mwingine na kumfanya kuwa nduguye."
  [Hotuba iitwayo "The Ideals of Islam;" Tazama: *Speeches and Writings Of Sarojini Naidu*, Madras, 1918, Uk. 167-9]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Arnold J. Toynbee

*(1889-1975) Mwanahistoria Mwingereza, Mhadiri katika Chuo kikuu cha Oxford.*

- "Kutokuwa na ubaguzi kati ya Waislamu ni moja kati ya mafanikio ya kipekee kabisa ya Uislamu, na kwa jinsi ulimwengu wa sasa ulivyo, kuna haja kubwa sana ya kuenezwa maadili haya ya Kiislamu."
  [*Civilization On Trial*, New York, 1948, Uk. 205]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## William Montgomery Watt

*(1909- ) Profesa (Emeritus) wa lugha ya Kiarabu na taaluma ya dini ya Kiislamu katika Chuo kikuu cha Edinburgh.*

- "Mimi si Muislamu kama ijulikanavyo hasa, japokuwa nataraji kuwa ni "Muislamu" yule "anayemnyenyekea Mwenyezi Mungu," lakini naamini kwamba kilichomo ndani ya Qur'an na maelezo mengine ya mtazamo Kiislamu ni hazina kubwa ya ukweli wa dini ya Mwenyezi Mungu ambayo mimi na watu wengine wa Kimagharibi tuna mengi ya kujifunza kutoka kwayo, na kwa hakika Uislamu ndio mshindani mkubwa katika kuleta msingi mkuu wa dini moja ya wakati ujao."
  [*Islam And Christianity Today*, London, 1983, Uk. ix.]

**Ili kujua zaidi kuhusu dini ya Kiislamu, tazama Tovuti hii:**

**Bertrand Russell**

*(1872-1970) Huyu ni Mwanafalsafa wa Kiingereza, Mwanahisabati, na mshindi wa tuzo la umalenga la Nobel, ambaye msisitizo wake katika utafiti wa kimantiki uliathiri sana mwelekeo wa falsafa ya karne ya ishirini. Amesema:*

- "Matumizi yetu ya neno 'the Dark Ages' (zama za giza) tunapotaja kipindi cha kuanzia mwaka 699 mpaka 1,000, yanaonyesha kuwa tunazingatia Ulaya ya Magharibi…Kutoka India hadi Uhispania, maendeleo makubwa ya Kiislamu yalinawiri. Kile kilichopotelea kwa Ukristo wakati huo hakikupotelea kwenye maendeleo ya ustaarabu, bali ni kinyume chake…Kwetu sisi yaonekana kuwa ustaarabu wa Ulaya ya Magharibi ndio ustaarabu, lakini haya ni maoni finyu."
  [*History of Western Philosophy*, London, 1948, Uk. 419]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Hamilton Alexander Roskeen Gibb**

*(1895-1971) Huyu ni mtaalamu bora wa mambo ya Mashariki wa wakati wake. Asema:*

- "Lakini Uislamu ungali na huduma ya kutoa kwa wanaadamu. U karibu zaidi na Mashariki halisi kuliko Ulaya ilivyo, na una maadili ya maelewano na ushirikiano wa tabaka mbalimbali. Hakuna jamii nyingine yoyote yenye kumbukumbu ya mafanikio ya kuweza kuwaunganisha matabaka ya makabila mbalimbali ya wanaadamu katika usawa wa hadhi, nafasi na juhudi kama Uislamu… Uislamu bado una nguvu ya kuzipatanisha tabaka ambazo haiwezekani kuzipatanisha. Iwapo upinzani ulioko wa jamii kubwa za Kimashariki na Kimagharibi yapasa ufanywe kuwa ushirikiano, basi upatanishi wa Uislamu ndio ufaao kabisa. Mikononi mwake mna uamuzi wa tatizo linaloikabili Ulaya juu ya uhusiano wao na Mashariki."
  [*Whither Islam*, London, 1932, Uk. 379.]

- "Kwamba mageuzi yake (Muhammad) yaliyooongeza ubora wa hali ya wanawake kwa ujumla, yanakubalika ulimwengu mzima."
  [*Mohammedanism*, London, 1953, Uk. 33]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**James A. Michener**

*(1907-1997) Huyu ni Mwandishi mahiri Mmarekani; aliyepokea tuzo la heshima ya honorary doctorate, kutoka kwenye Vyuo vikuu 30 katika nyanja tano za kielimu, pia alipata nishani ya Rais ya uhuru, ambayo ni tuzo kubwa zaidi kwa raia wa Marekani. Amesema:*

- "Katika historia, hakuna dini iliyoenea kwa kasi sana kama ya Uislamu . . . Wamagharibi waliamini kwamba kuenea huku kulisababishwa na upanga. Lakini hakuna msomi yeyote wa kisasa anayekubali nadharia hii, na Qur'an iko wazi juu ya suala la kuunga mkono uhuru wa dhamira ya kukubali ukweli na uongo." [*Islam - The Misunderstood Religion*, Readers' Digest (Toleo la Amerika) Mei 1955]

## Edward Gibbon

*(1737-1794) Mwanahistoria mkuu wa Kiingereza wa wakati wake. Amesema:*

- "'Naamini Mungu mmoja na Mohammed ni Mjumbe wa Mungu' kutamka hivi ni jambo la kila siku katika Uislamu. Dhahania ya kiakili ya Mungu katu haijavunjiwa heshima na vimungu-sanamu vyovyote vinavyoonekana; heshima ya Mtume katu haijavunja heshima ya sifa nzuri za mwanaadamu, na miongozo yake imehifadhi ridhaa ya wafuasi wake ndani ya mipaka ya mantiki na dini."
  [*History Of The Saracen Empire,* London, 1870, Uk. 54.]

- "(Uislamu) ni msafi zaidi kuliko mfumo wa ki-Zorosta. Ni wenye kupenda mambo ya wasitani kushinda sheria za Musa, dini ya Mohammed yaonekana kidogo yakubaliana na hoja kuliko imani za kishirikina ambazo, katika karne ya saba, ziliudhalilisha usahali wa Injili."
  [*The History of the Decline and Fall of the Roman Empire*, Juz. 5. Uk. 487]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Jared Diamond

*Profesa wa Saikloogia katika UCLA School of Medicine; aliyepokea zawadi ya Pulitzer for General Non-Fiction mnamo mwaka 1998. amesema:*

- "Enzi za kati (1100-1500) Uislamu ulikuwa umepiga hatua kubwa katika teknolojia, na maendeleo. Ulifikia kiwango cha juu sana cha elimu kuliko Ulaya ya wakati huo; ulikuza tirathi za Kigiriki za zamani za kimaendeleo kiasi kwamba vitabu vingi vya zamani vinavyojulikana kwetu hivi leo tumevijua kupitia kwa nakala za Kiarabu. Uislamu umeunda Vinu vya upepo (*Windmills*), *Trigonometria* (Hesabu ya uhusiano kati ya pembe na pande zake tatu), Tanga la pembe tatu (*Lateen sails*), pia ulileta maendeleo makubwa katika ufuaji wa vyuma, uhandisi wa Kemikali na kimitambo na njia za umwagiliaji maji. Katika enzi ya kati, Teknolojia ilikuwa ikimiminika kutoka kwa Uislamu kwenda Ulaya, na si Ulaya kwenda kwa Uislamu, ila tu baada ya miaka ya 1500 ndipo mwelekeo huo wa mmiminiko ulianza kugeuka na kuwa kinyume."
  [*Guns, Germs, and Steel - The Fates of Human Societies*, 1997, Uk. 253]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Annie Besant

*(1847-1933) Rais wa The Indian National Congress in 1917. Amesema:*

"Daima nadhani kuwa mwanamke, katika Uislamu, ana uhuru zaidi kuliko katika Ukristo. Mwanamke analindwa zaidi na Uislamu kuliko imani nyingione inayohubiri ndoa ya mke mmoja. Katika Qur'an sharia imuhusuyo mwanamke ina uadilifu na sahali zaidi. Ni katika kipindi cha miaka ishirini tu iliyopita Ukristo wa Uingereza ulipotambua haki ya mwanamke ya kumiliki mali, ambapo Uislamu uliruhusu haki hiyo kutoka wakati wote." [*The Life and Teachings of Muhammad*, Madras, 1932, Uk. 25, 26]

*Ewe Mtume, fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hujafikisha ujumbe wake, na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu.*
(Qur'an: 5, 67)

# Je Mtume (s.a.w.w.) aliteua wasii?

Mashia wanaamini kwamba agizo lililotajwa na Aya hiyo ya Qur'an lilitekelezwa na Mtume (s.a.w.w.) alipomteua Imam 'Ali bin Abi Talib (a.s.) kuwa wasii wake kwenye siku ya Ghadir Khumm.

**Lakini je, neno *mawla* halina maana ya rafiki?**

Japokuwa idadi kubwa ya Wanavyuoni wa Sunni wa zama zote na maoni yote wamethibitisha tukio hilo na maneno ya kihistoria ya Mtume (s.a.w.w.), lakini imekuwa ni vigumu kwao kukubaliana na yaliyotokea baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w.). Lakini nakala hii fupi haiwezi kutaja kwa ufafanuzi matukio hayo. La muhimu ni kwamba Wanavyuoni wengi wa Sunni wamedai kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimtangaza 'Ali (a.s.) kuwa ni rafiki na msaidizi wa Waislamu!

Kuna mitazamo mingi ya tukio hili inaoonyesha jinsi lilivyokuwa na umuhimu. Miongoni mwayo ni kufunuliwa kwa Aya nyingi za Qur'an, mkusanyiko mkubwa wa watu, hatua za mwisho za maisha ya Mtume (s.a.w.w.), watu kuthibitisha kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na mamlaka makuu, kupongezwa baada ya tukio hilo na 'Umar, na sababu sababu nyingine nyingi ambazo haitoshi kuzitaja katika nakala hii fupi; yote yanaonnyesha juu ya kutawazwa kwa wasii wa Mtume (s.a.w.w.). Ni dhahiri kwamba neno *mawla* lilitumika kwa maana ya mamlaka kamili baada ya Mtume na si kwa mamlaka ya muda tu.

## Neno la Mwisho

Ikiwa bado kuna shaka juu ya umuhimu wa kihistoria wa hotuba hii, na bidii ya baadhi ya watu ya kuificha, hebu basi neno la mwisho liwe ni hili:

Wakati Imam 'Ali (a.s.), alipokuwa khalifa, na hapo ni miongo kadhaa baada ya tukio la Ghadir, siku moja alimwambia Anas bin Malik, swahaba wa Mtume (s.a.w.w.): "Kwa nini hutoi ushahidi kwa uliyoyasikia kwa Mtume siku ya Ghadir?" Akajibu, "Ee Amir ul-Muminin! Nimezeeka na siwezi kukumbuka." Hapo 'Ali (a.s.) akasema: "Mungu atakupa doa jeupe (la ukoma) lisilofichika na kilemba chako! Ikiwa kwa makusudi waficha ukweli!" Na kabla Anas hajainuka pale alipokuwa amekaa, alipatwa na doa kubwa jeupe usoni kwake.

- Ibn Qutaybah al-Dinawari, Kitab al-Ma'arif, (Cairo, 1353 AH), Uk. 251
- Ahmad bin Hanbal, al-Musnad, Juz. 1, Uk. 119
- Abu Nu`aym al-'Isfahani, Hilyat al-Awliya', (Beirut, 1988), Juz. 5, Uk. 27
- Nur al-Din al-Halabi al-Shafi'i, al-Sirah al-Halabiyya, Juz. 3, Uk. 336
- Al-Muttaqi al-Hindi, Kanz ul-'Ummal, (Halab, 1969-84), Juz. 13, Uk. 131

**Kwa maelezo zaidi juu ya tukio la Ghadir Khumm tazama Tovuti hii:**

**http://al-islam.org/ghadir/**

## Nini kilitokea siku ya Ghadir Khumm?

Ghadir Khumm ni sehemu iliyoko maili kadhaa kutoka Makka kwenye barabara ielekeayo Madina. Mnamo tarehe 18 Dhul hijja (Mfungo tatu), Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akipita

sehemu hii akirejea kutoka kwenye Hijja yake ya kuaga (ya mwisho), Aya hii ilishuka: “Ewe Mtume fikisha uliyoteremshiwa…” Hivyo alisimama kuwatangazia mahujaji aliokuwa amefuatana nao kutoka Makka na ambao walikuwa watawanyike kutoka kwenye njia panda hiyo na kuelekea sehemu mbalimbali waendazo. Mtume akaamrisha mimbari maalum ya matawi ya miti itayarishwe kwa ajili yake. Baada ya Swala ya adhuhuri, Mtume (s.a.w.w.) aliketi juu ya mimbari hiyo na kutoa hotuba yake ya mwisho, akiihutubia kadamnasi kubwa kabla ya kifo chake miezi mitatu baadaye.

Jambo kubwa lililojitokeza katika hadhara hii ni pale alipomshika mkono Imam ‘Ali (a.s.) na kuwauliza wafuasi wake iwapo yeye (Mtume) alikuwa ni bora zaidi (*awla*) katika mamlaka kuliko wao wenyewe. Hapo mkusanyiko wa watu ulijibu kwa sauti moja kuu: "Ni hivyo ee Mtume wa Mwenyezi Mungu."

Kisha Mtume (s.a.w.w.) akatangaza: **"Ambaye mimi ni Bwana (*Mawla*) wake, basi 'Ali pia ni Bwana wake. Ewe Mwenyezi Mungu, mpende ampendaye, na uwe ni adui wa amfanyiaye uadui."**

Mara tu Mtume (s.a.w.w.) alipomaliza hotuba yake, ilishuka Aya hii:

*“Leo nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu”.* (Qur'an 5:3).

Baada ya kumaliza hotuba yake, Mtume (s.a.w.w.) alimtaka kila mtu kutoa kiapo cha utii kwa 'Ali (a.s.) na kisha akampongeza. Miongoni mwa waliompongeza ni 'Umar bin al-Khattab, aliyesema: "Hongera Ibn Abi Talib! Leo umekuwa Bwana wa kila muumini, wanaume na wanawake."

Mwarabu mmoja aliposikia tukio la Ghadir Khumm, alikwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) na kumwambia: "Ulituamrisha kushuhudia ya kwamba hapana Mungu ila Allah na wewe ni Mtume wake, tukakutii. Ulituamrisha kuswali Swala tano kila siku, tukakutii. Ulituamuru kufunga katika mwezi wa Ramadhani, tukakutii. Ukatuamuru kuhiji Makka pia tukakutii. **Lakini hukutosheka na hayo yote, kwa mkono wako ukamwinua binamu yako na kutulazimisha sisi awe bwana wetu ukisema 'Ali ni bwana wa yule ambaye mimi ni Bwana wake.' Kulazimishwa huku kunatoka kwa Mwenyezi Mungu au kunatoka kwako?"** Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Naapa kwa Mungu wa pekee! Hii ni amri itokayo kwa Mwenyezi Mungu mkuu, Mtukufu."

Aliposikia majibu haya, yule mtu aligeuka na kumuelekea ngamia wake huku akisema: "Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ayasemayo Muhammad ni sahihi, basi tuteremshie jiwe kutoka mbinguni na utuadhibu vikali." Basi mtu huyo kabla hajamfikia ngamia wake, Mwenyezi Mungu alimteremshia jiwe lililomwingia mwilini mwake kupitia kichwani kwake na kumwacha akiwa amekufa. Ilikuwa katika tukio hili ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoteremsha Aya ifuatayo:
*Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Juu ya Makafiri - ambayo hapana awezaye kuzuia. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye utukufu mkubwa.* (Qur'an 70:1-3)

## Je Wanavyuoni wa Sunni hulichukulia tukio hili kuwa ni la kweli?

Idadi kubwa ya Wanavyuoni wa Sunni waliosimulia tukio hili, kwa urefu na kwa muhtasari, ni ya kushangaza! Tukio hili la kihistoria limesimuliwa na Maswahaba wa Mtume 110, pia Tabiina (waliokuwako baada ya Maswahaba) wapatao 84, na Wanavyuoni wengi wa ulimwengu wa Kiislamu, kutoka karne ya 1 AH hadi karne ya 14 AH (Karne ya saba hadi ya ishirini CE).

**Takwimu hizi ni zile tu za wapokezi waliotajwa katika Hadith zilizopokewa na Wanavyuoni wa Sunni!**

Idadi chache sana mkusanyiko wa misingi ya marejeo imetajwa hapo chini. Wengi wa Wanavyuoni hawa hawakunukuu hotuba ya Mtume tu bali pia wameiita kuwa ni sahihi, nayo ni:

- al-Hakim al-Naysaburi, al-Mustadrak `ala al-Sahihayn (Beirut), Juz. 3, Uk. 109-110, Uk. 133, Uk. 148, Uk. 533. yeye amesisitiza kuwa Hadith hii ni *sahih* kulingana na vipimo vya al-Bukhari na Muslim; al-Dhahabi pia amethibitisha hili.
- al-Tirmidhi, Sunan (Cairo), Juz.. 5, Uk. 633
- Ibn Majah, Sunan, (Cairo, 1952), Juz. 1, Uk. 45
- Ibn Hajar al-'Asqalani, Fath al-Bari bi Sharh Sahih al-Bukhari, (Beirut, 1988), Juz. 7, Uk. 61
- Al-'Ayni, 'Umdat al-Qari Sharh Sahih al-Bukhari, Juz. 8, Uk. 584
- Ibn al-'Athir, Jami` al-'Usul, i, 277, Na. 65;
- Al-Suyuti, al-Durr al-Manthur, Juz. 2, Uk. 259 na Uk. 298
- Fakhr al-Din al-Razi, Tafsir al-Kabir, (Beirut, 1981), Juz. 11, Uk. 53
- Ibn Kathir, Tafsir Qur'an al-'Adhim, (Beirut), Juz. 2, Uk. 14
- Al-Wahidi, Asbab an-Nuzul, Uk. 164
- Ibn al-'Athir, Usd al-Ghaba fi Ma'rifat al-Sahaba, (Cairo), Juz.3, Uk. 92
- Ibn Hajar al-'Asqalani, Tahdhib al-Tahdhib, (Hyderabad, 1325), Juz. 7, Uk. 339
- Ibn Kathir, al-Bidayah wan Nihayah, (Cairo, 1932), Juz. 7, Uk. 340, Juz. 5, Uk. 213
- Al-Tahawi, Mushkil al-Athar, (Hyderabad, 1915), Juz. 2, Uk. 308-9
- Nur al-Din al-Halabi al-Shafi'i, al-Sirah al-Halabiyya, Juz. 3, Uk. 337

Al-Zurqani, Sharh al-Mawahib al-Ladunniyya, Juz. 7, Uk. 13

*Na shikamaneni kwa kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane*
(Qur'an 3:103)

# Kwa nini Shi'ah?

Neno "Shi'ah" ni sifa ya jina litumikalo kwa Waislamu wanaowafuata Maimam wanaotokana na kizazi cha Mtume (*Ahl al-Bayt*). Hawakulitumia jina hilo kwa sababu za ki-madhehebu au kusababisha migawanyiko miongoni mwa Waislamu. Walilitumia kwa sababu Qur'an inalitumia, Mtume Muhammad alilitumia, na Waislamu wa mwanzo walilitumia – hata kabla ya maneno kama *Sunni* au *Salafi* kuwapo duniani

**Lakini vipi Mtume (s.a.w.w.) atumie neno la kuleta mgawanyiko?**

Je Nabii Ibrahim alikuwa ni wa ki-madhehebu? Vipi kuhusu Nabii Nuh na Nabii Musa? Ikiwa neno Shi'ah ni la kuleta mgawanyiko au la ki-madhehebu, basi Mwenyezi Mungu asingelilitumia kwa Mitume wake wenye daraja ya juu, na wala Mtume Muhammad (s.a.w.w.) asingeliwatukuza.

Ni lazima isisitizwe kwamba Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hakutaka kuwagawaya Waislamu kwa makundi. Bali aliwaamuru watu wote wamfuate Imam Ali (a.s.) akiwa ni mwakilishi wake wakati alipokuwa hai, na akiwa ni mrithi na khalifa wake baada yake. Lakini kwa bahati mbaya waliokubali kufuata matakwa yake walikuwa ni wachache, na walijulikana kama "Shi'ah wa Ali". Walipatwa na kila aina ya ubaguzi na mateso, na waliteseka kuanzia ile siku aliyofariki rehma ya umma, Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Lau Waislamu wote wangelitii na kufuata vile Mtume (s.a.w.w.) alivyotaka, kusingelikuwa na makundi au madhehebu ndani ya Uislamu. Mtume (s.a.w.w.) amesema:

**"Mara tu nitakapofariki, mizozo na chuki itajitokeza miongoni mwenu; wakati hali hiyo itakapodhihiri, basi mtafuteni Ali, kwa sababu yeye anaweza kupambanua kati ya ukweli na uongo."**

- Ali Muttaqi al-Hindi, *Kanz al-'Ummal*, (Multan) Juz. 2 Uk. 612, Na. 32964

Kuhusu ile Aya tuliyoitaja hapo awali, baadhi ya Wanavyuoni wa Sunni wameipokea kutoka kwa Ja'far al-Sadiq (a.s.), Imam wa sita wa Shi'ah, Imam anayetokana na kizazi cha Mtume (*Ahl al-Bayt*), kwamba:

"Sisi ni kamba ya Mwenyezi Mungu ile aliyoitaja akasema: *Na shikamaneni kwa kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane.*"

- al-Tha'labi, *Tafsir al-Kabir*, chini ya maelezo ya Aya 3:103
- Ibn Hajar al-Haythami, *al-Sawa'iq al-Muhriqah*, (Cairo) Sura. 11, She. 1, Uk. 233

Kwa hivyo, ikiwa Allah anakataa migawanyiko ya ki-madhehebu, basi vilevile anakataa wale wanaojitenga na kamba Yake, na si wale wanaoshikamana nayo barabara!

**Mwisho:**

Tumekwishaonyesha kwamba neno Shi'ah limekuwa likitumika katika Qur'an kwa wafuasi wa watumishi wakuu wa Allah, na katika Hadith za Mtume, kwa wafuasi wa Imam Ali (a.s.). Yeyote atakayefuata mwongozo huu wa Mwenyezi Mungu atakuwa amesalimika na mizozo katika dini, na atakuwa ameshikamana na kamba madhubuti ya Mwenyezi Mungu, na atapata bishara njema za Peponi.

**Ili kujua zaidi kuhusu dini ya Kiislamu, tazama Tovuti hii:**

***http://al-islam.org/faq/***

**Shi'ah ndani ya Qur'an**

Neno "Shi'ah" linamaanisha "wafuasi; wanachama wa chama". Allah ametaja katika Qur'an kwamba baadhi ya watumishi Wake wema walikuwa ni wafuasi (Shi'ah) wa wafuasi Wake wengine wema.

*Na hakika Ibrahim alikuwa katika Shi'ah wake,(akaenda mwendo wake)*
(Qur'an 37:83)

*(Nabi Musa) akaingia mjini (siku moja) wakati wenyeji wake walikua katika ghafla (yaani katikati ya mchana), na akakuta humo watu wawili wakipigana: Mmoja ni katika Shi'ah wake na mwengine katika adui zake. Basi yule aliyekuwa Shi'ah wake alimwomba msaada juu ya yule adui yake.*
(Qur'an 28:15)

Hivyo basi Shi'ah ni neno rasmi lililotumika na Allah katika Qur'an yake kwa ajili ya Mitume wake wenye daraja ya juu, na kwa wafuasi wao.

Ikiwa mtu ni Shi'ah (mfuasi) wa watumishi wema sana, basi hapana makosa kuwa Shi'ah. Au kwa maneno mengine, ikiwa mtu atakuwa ni Shi'ah wa dhalimu au wa mkosefu, bila shaka atayapata yatakayompata kiongozi wake. Qur'an yaashiria kuwa siku ya Kiyama watu watakuja kwa makundi, na kila kundi litakuwa na kiongozi wake (*Imam*) mbele yake. Allah amesema:

*(Wakumbushe) siku tutakapowaita kila watu pamoja na waongozi wao.*
(Qur'an 17:71)

Mnamo siku ya Kiyama, majaaliwa ya "wafuasi" wa kila kundi yatategemea na majaaliwa ya Imam wao (kwa sharti kwamba wao, kweli, walimfuata Imam huyo). Allah ametaja ndani ya Qur'an kwamba kuna aina mbili za Maimam:

Na tuliwafanya maimam (waongozi) waitao katika moto, na siku ya Kiyama hawatanusuriwa. Na tukawafuatishia laana katika dunia hii, na siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa wenye hali mbaya (kabisa).

(Qur'an 28:41-42)

Qur'an pia yakumbusha kwamba kuna Maimam walioteuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni viongozi wa wanaadamu:

Na tukawafanya miongoni mwao Maimamu wanaoongoa kwa amri yetu, waliposubiri, na walikuwa wakiziyakinisha Aya zetu.
(Qur'an 32:24)Kwa yakini, wafuasi halisi (Shi'ah) wa Maimam hawa, watakuwa ndio watu waliofaulu hasa, katika siku ya Kiyama.

**Shi'ah katika Hadith**

Katika historia ya Kiislamu, neno "Shi'ah" limekuwa likitumika hasa kwa wafuasi wa Imam 'Ali (a.s.). Msemo huu si kitu kilichobuniwa baada ya Mtume! Mtu wa kwanza aliyetumia istilahi hii ni yeye mwenyewe Mjumbe wa Allah.   Wakati Aya ya Qur'an ifuatayo iliposhuka:

*Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema wa viumbe.*
(Qur'an 98:7)

Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Ali: "**Hii ni kwa ajili yako na wafuasi (Shi'ah) wako."**

Kisha akasema: "**Naapa kwa yule anayeyatawala maisha yangu kwamba mtu huyu (Ali) na wafuasi wake wataokolewa na adhabu mnamo siku ya ufufuo."**

- Jalal al-Din al-Suyuti, *Tafsir al-Durr al-Manthur*, (Cairo) Juz. 6, Uk. 379
- Ibn Jarir al-Tabari, *Tafsir Jami' al-Bayan*, (Cairo) Juz. 33, Uk. 146
- Ibn Asakir, *Tarikh Dimashq*, Juz. 42, Uk. 333, Uk. 371
- Ibn Hajar al-Haythami, *al-Sawa'iq al-Muhriqah*, (Cairo) Sura. 11, Sehemu 1, Uk. 246-247

Mtume (s.a.w.w.) amesema: **"Ewe Ali! (Mnamo siku ya Kiyama) wewe na wafuasi wako mtakwenda kwa Mwenyezi Mungu mkiwa mmeridhiwa na mmeridhika, na maadui zenu watakwenda kwake wakiwa na ghadhabu na huku shingo zimewasimama!**

- Ibn al-'Athir, *al-Nihaya fi Gharib al-Hadith*, (Beirut, 1399), Juz. 4 Uk. 106
- Al-Tabarani, *Mu'jam al-Kabir*, Juz. 1 Uk. 319
- Al-Haythami, *Majma' al-Zawa'id*, Juz. 9, Na. 14168

Mtume (s.a.w.w.) amesema: **"Furaha kuu! O Ali! Hakika wewe na wafuasi wako mtakuwa Peponi**.**"**

- Ahmad Ibn Hanbal, *Fadha'il al-Sahaba*, (Beirut) Juz. 2, Uk. 655
- Abu Nu'aym al-Isbahani, *Hilyatul Awliya*, Juz. 4, Uk. 329
- Al-Khatib al-Baghdadi, *Tarikh Baghdad*, (Beirut) Juz. 12, Uk. 289
- Al-Tabarani, *Mu'jam al-Kabir*, Juz. 1, Uk. 319
- Al-Haythami, *Majma' al-Zawa'id*, Juz. 10, Uk. 21-22
- Ibn 'Asakir, *Tarikh Dimashq*, Juz. 42, Uk. 331-332

Ibn Hajar al-Haythami, *al-Sawa'iq al-Muhriqah*, (Cairo) Sura. 11, Sehemu 1, Uk. 247

*Enyi mlio amini!*
*Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli*
(Qur'an: Sura ya 9, Aya 119)

# *Rafidi*

# Wapokezi wa Kishia katika

# *Sahih al-Bukhari*

Mtazamo wa Shi'ah unafuatwa na wasomi wengi wamwanzo wa Uislamu ambao walikuwa wakichukuliwa kuwa wakweli na waaminifu, na mapokezi yao ya Hadith za Mtume (s.a.w.w) zilikuwa zikitegemewa na wasomi maarufu wa Sunni.

Orodha iliyopo chini ni baadhi ya wasomi wa kishia ambao al-Bukhari

## Swali: Lakini labda al-Bukhari, Muslim, na wengine hutegemewa na watu hawa bila kujua imani yao ya kweli?

Wasomi hawa wamejitolea maisha yao kwa ajili ya kupata na kueneza mila ya Mtume (s.a.w.w) na kusoma maisha ya waenezaji wa mila hizi. Wengi wao waliandika vitabu wakiwa vijana hasa (sayansi ya hukumu , utegemezi wa wapokezi) kwa mitazamo yao. Ingawa uchaguzi wao na mapendekezo yao ya mamlaka na mafundisho yameonyesha msimamo madhubuti wa Sunni, na bado wamejikuta wakitegemea Mashia ambao wao huwa kwenye ukweli. Hii ni pamoja na ukweli kwamba Ushia umejieleza wazi pamoja na kutokukubalika na wengi!

Hivyo, kusema kwamba al-Bukhari, Muslim, na wengine hawakujua ukweli na imani ya wapokezi hawa wa kishia itakuwa kuwaita isivyostahiki katika fani yao!

## Swali: Lakini kwa nini wao wanategemea Sunni kama ndio wenye sheria tu?

Labda wao walikuwa sio kama ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo kama baadhi ya ndugu zetu wa Sunni ambao wanasisitiza juu ya kujihusisha na imani ya Shia na kila aina ya madai ya uongo. Ni lazima kuwa wazi kutokana na wasifu wa waliotajwa kwamba walikuwa wakosoaji wa baadhi ya Makhalifa na Maswahaba – kulingana na ushahidi wa kawaida wa kihistoria – uliovumiliwa na wasomi wa kisuni wa vizazi vilivyopita.

## Swali: Je! Mashia hutegemea wapokezi wa Kisuni katika vitabu vyao?

Kwa muda mrefu mpokezi (msimuliaji) wa kisuni hajulikani adui yake upande wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w) (Ahl al-Bayt) na ni huchukuliwa kweli, kukubaliwa hadithi za Shia.

## Hitimisho:

Ukweli ni kwamba sehemu muhimu ya maandiko ya *Hadith* za Sunni itakuwa imepotea kama vyanzo kutoka kwa wapokezi wa kishia vimekataliwa. Imani ya Shia daima imebakia na kuwa ushahidi mzuri mbadala kwa uhakika wa maoni ya Sunni.

**Ili kujua zaidi juu ya Uislamu sahihi, tembelea:**

***http://al-islam.org/faq/***

| Orodha iliyopo chini ni baadhi ya wasomi wa kishia ambao al-Bukhari imewategemea katika *Sahih* yake. Kama tukiongeza katika haya, waliobaki miongoni mwao itakuwa ni pamoja na wapokezi katika *Sahih* Muslim na wengine wane wa *Sihah Sittah* ambao wamefuata imani ya Mashia, kisha idadi itaongezeka kwa kiasi kikubwa. Kuokoa nafasi, rejea zimetolewa upande wa jina (Kitab) katika kila kitabu kwa Hadith moja tu kwa kila mtu – wengine wanaweza kupatikana kwa kutumia fahirisi au mpango wa Hadith.<br><br>Msomaji wa ilani ya *Rafidi* kila muda, na kisha katika wasifu zifuatazo. Wanazuoni wa Sunni kwa ujumla wamefafanua *Rafidi* kama Mashia ambao kwa uwazi wamekosoa au kukataa uhalali wa Makhalifa kabla ya 'Ali (a.s). | |
|---|---|
| 'Ubayd Allah b. Musa al-'Absi<br>*(Alikufa 213 AH)*<br><br>*Sahih Bukhari* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih Muslim* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih al-Tirmidhi* [*kitab al-salat*]<br>*Sunan al-Nasa'i* [*kitab al-sahw*]<br>*Sunan Abu Dawud* [*kitab al-taharah*]<br>*Sunan Ibn Majah* [*kitab al-muqaddamah*] | ❑ Aboo Daawuud akasema: Yeye alikuwa na shauku ya ushia, [Hadith al-muqaddamah] yake ni halali …. Ibn Mandah alisema: Ahmad ibn Hanbal katumika kwa kumweka nje 'Ubaydullaah pamoja na watu, na yeye alikuwa maalumu kwa ajili ya ***Rafd*** ( alikuwa na urafiki uliokithiri kwa 'Ali), na hakutaka mtu yeyote kuingia nyumba yake aitwaye' "Mu'aawiyah'.[*Imani ya Imaam wa Hadeeth al-Bukhari na wa Wasomi Mkuu ambaye Yesu amesema* (Imechapishwa na Salafi, UK, 1997), uk 89 kutoka kwa Al-Dhahabi, *Siyar A'lam al-Nubala*, Juz. 9, uk 553-557]<br>❑ "Mtu mcha Mungu, mmoja miongoni mwa wasomi muhimu wa Shia … aliyezingatiwa kutegemewa na Yahya b. Ma'in, Abu Hatim alisema alikuwa mwenye kutegemewa, mwaminifu … al-'Ijli akasema: Yeye alikuwa na mamlaka juu ya Qur'an … "[Al-Dhahabi, *Tadhkirat al-Huffaz* chini ya "'Ubayd Allah b. Musa al-'Absi"] |

| | |
|---|---|
| 'Abbad b. Ya'qub al-Rawajini<br>*(Alikufa 250 AH)*<br><br>*Sahih Bukhari* [*kitab al-tawhid*]<br>*Sahih al-Tirmidhi* [*kitab al-manaqib*]<br>*Sunan Ibn Majah* [*kitab ma ja' fi al-jana'iz*] | ❑ Yeye ni ***Rafidi*** na mwenye kutegemewa na Hadith yake ni katika (*Sahih* ya) al-jana'iz al-Bukhari.[Ibn Hajar al-'Asqalani, *Taqrib al-Tahdhib*, chini ya "'Abbad b. Ya'qub al-Rawajani"]<br>❑ Abu Hatim akasema: Yeye ni Shaykh, mwenye kutegemewa. Ibn 'Adi akasema: Yeye katumika kukemea Salaf. Hakika yeye ana msimamo wa Ushia. B. Salih Muhammad akasema: Yeye katumika kumkana Uthman '. Nimemsikia akisema, "Mwenyezi Mungu anahaki zaidi na angeweza kukubali toba yaTalhah na al-Zubayr na kwenda mbinguni baada ya kula kiapo cha utii kwa 'Ali na kisha wakapigana naye." Ibn Hibban akasema: Yeye ni ***Rafidi*** kuwakaribisha (wengine kwa imani yake). amesimulia Hadith hii …, "Kama ukimuona Mu'awiyah juu ya mimbari yangu, muue!" [Ibn Hajar al-'Asqalani, *Tahdhib al-Tahdhib*, chini ya "'Abbad b. Ya'qub al-Rawajani"] |

| | |
|---|---|
| 'Abd al-Malik b. A'yan al-Kufi<br><br>*Sahih al-Bukhari* [*kitab al-tawhid*]<br>*Sahih Muslim* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih al-Tirmidhi* [*kitab tafsir al-Qur'an*]<br>*Sunan al-Nasa'i* [*kitab al-'iman wa al-nudhur*]<br>*Sunan Abu Dawud* [*kitab al-buyu'*]<br>*Sunan Ibn Majah* [*kitab al-zakah*] | ❑ Yeye alikuwa ***Rafidi*** wa Kishia, mmoja wa (watu wa) maoni. [Abu Ja'far al-'Uqayli, *Du'afa al-'Uqayli*, chini ya "'Abd al-Malik b. A'yan"]<br>❑ Yeye alikuwa ***Rafidi*** ,kutegemewa (Saduq). [Al-Mizzi, *Tahdhib al-Kamal*, chini ya "'Abd al-Malik b. A'yan"]<br>❑ Al-'Ijli akasema: Yeye ametoka Kufah, ni Tabi'i (Imam), kutegemewa. Sufyan akasema: 'Abd al-Malik b. 'A'yan Shi'a wametuhadithia sisi, yeye ni ***Rafidi*** kwetu, ni mtu wa maoni. Hamid alisema: Wale ndugu watatu, 'Abd al-Malik, Zurarah, na Hamran wote walikuwa *Rawafid*. Abu Hatim akasema: Yeye alikuwa wa kwanza kukubali Ushia, (alikuwa) juu ya msimamo wakweli, kufuata mila nzuri, na mila yake imeandikwa.<br>[Ibn Hajar al-'Asqalani, *Tahdhib al-Tahdhib*, chini ya "'Abd al-Malik b. A'yan"] |

| | |
|---|---|
| 'Abd al-Razzaq al-San'ani<br>*(Alikufa 211 AH)*<br><br>*Sahih Bukhari* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih Muslim* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih al-Tirmidhi* [*kitab al-taharah*]<br>*Sunan Nasa'i* [*kitab al-taharah*]<br>*Sunan Abi Dawud* [*kitab al-taharah*]<br>*Sunan Ibn Majah* [*kitab al-muqaddamah fi al-'iman*] | ❑ Ibn 'Adi alisema: Wao (yaani wasomi) hakuwa na al-muqaddamah fi al-'iman] na hawakuona tatizo lolote katika Hadith yake ila kwa kuwa wao walitokana na Ushia … Yeye alikuwa ni mtu wa heshima … yeye amesema mila katika nyumba ya Mtume imeheshimiwa (*Ahl al-Bayt*) na zingine zimeshushwa hadhi … Mukhlid al-Shu'ayri alisema: Mimi nilikuwa pamoja na 'Abd al-Razzaq wakati mtu mmoja alipomtaja Mu'awiyah. 'Abd al-Razzaq akasema: Je, si kuchafua mkutano wetu kwa kutaja dhuria wa Abu Sufyan!'.[Al-Mizzi, *Tahdhib al-Kamal*, chini ya"'Abd al-Razzaq al-San'ani"]<br>❑ Ibn 'Adi amesema (a Hadith) kutoka' Abd al-Razzaq …, "Kama wewe utamuona Mu'awiyah juu ya mimbari yangu basi muue!". [Al-Dhahabi, *Mizan al-'I'tidal*, chini ya "'Abd al-Razzaq al-San'ani"] |
| 'Awf b. Abi Jamilah al-'A'rabi<br>*(Alikufa 146 AH)*<br><br>*Sahih Bukhari* [*kitab al-'iman*]<br>*Sahih Muslim* [*kitab al-masajid wa mawadi' al-salat*]<br>*Sahih al-Tirmidhi* [*kitab al-salat*]<br>*Sunan Nasa'i* [*kitab al-taharah*]<br>*Sunan Abi Dawud* [*kitab al-salat*]<br>*Sunan Ibn Majah* [*kitab al-salat*] | ❑ Yeye alikuwa ***Rafidi*** lakini mwenye kutegemewa … Yeye alikuwa akihusishwa na kutegemewa na wasomi wengi, na katika hao yeye ni Shi'a.<br>[Al-Dhahabi, *Siyar A'lam al-Nubala*, chini ya"'Awf b. Abi Jamilah"]<br>❑ 'Awf ilikuwa ni Qadari, Kishia, ni Shaytan!<br>[Abu Ja'far al-'Uqayli, *Du'afa al-'Uqayli*, chini ya"'Awf b. Abi Jamilah"]<br>❑ Yeye alikuwa akielekea kwenye Ushia. Ibn Ma'in alisema: anategemewa, Al-Nasa'i alisema: anategemewa sana.<br>[Al-Mizzi, *Tahdhib al-Kamal*, chini ya "'Awf b. Abi Jamilah"] |

*Kwa hakika sisi tumeuteremsha ukumbusho huu* (*Qur'an*) *na hakika sisi ndio tuulindao.*
*(Qur'an: Sura 15, Aya 9)*

# Je Mashia wanaamini Qur'an nyingine?

Mashia mara kwa mara wanatuhumiwa kwa imani ya ***Tahrif*** ndani ya Qur'an, ambayo maana yake ni kuamini kwamba Qur'an imepotoshwa na haiko sawa na ile aliyoteremshiwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

**Swali: Ni vipi kuhusu zile Hadith zisemazo kwamba baadhi ya Aya si sehemu ya Qur'an?**

Shia hawaamini kwamba mwandishi au mpokezi ana kinga ya kutofanya makosa, na kwa hivyo hawachukulii kwamba Hadith zote ni sahihi. Kitabu pekee chenye kinga ya kutokuwa na kosa lolote ni Qur'an. Mara nyingi Hadith hizi huchukuliwa kuwa ni dhaifu au maneno uliyo teremshwa nje ya Qur'an.

- Ni vizuri itajwe kwamba kuna baadhi ya Hadith kwenye Sahih al-Bukhari na Sahih Muslim zisemazo kwamba Aya nyingi za Qur'an haziko. [Al-Bukhari, Al-Sahih, Juz. 8 Uk. 208; Muslim, Al-Sahih, Juz. 3 Uk. 1317].
- Si hivyo tu, Hadith hizi za Sunni zadai kwamba Sura mbili za Qur'an hazipo, ambapo mojawapo ni kama ya Sura ya al-Bara'ah (Sura ya 9) kwa kirefu!!! [Muslim, Al-Sahih, Kitab al-Zakat, Juz. 2 Uk. 726].
- Hata kuna baadhi ya mapokezi ya Hadith ya Sunni yanayodai kuwa Sura ya al-Ahzab (33) ilikuwa ni ndefu kama ilivyo Sura ya al-Baqarah (2)!!! Ambapo hakika Sura ya al-Baqarah ndio Sura iliyo kubwa zaidi katika Qur'an. Kuna hata Hadith ndani ya Sahih al-Bukhari na Muslim ambazo zimetaja kwa urefu baadhi ya Aya ambazo hazipo. [Al-Bukhari, Al-Sahih, Juz. 8 Uk. 208].

Kwa bahati nzuri, Shia katu hawajawatuhumu ndugu zao Sunni kwa kuamini kwamba Qur'an haikukamilika. Sisi tunasema kwamba Hadith hizi za Sunni, ama ni dhaifu, au zimezushwa.

**Hitimisho:**

"Sisi twaamini kwamba Qur'an ambayo Mwenyezi Mungu alimteremshia Mtume wake Muhammad (s.a.w.w.) ni kama ile iliyoko baina ya jalada mbili. Na ndiyo hiyo hiyo iliyoko mikononi kwa watu, na haina tofauti zaidi ya ile… Na anayedai kuwa sisi tunasema kwamba (Qur'an) ni tofauti kuliko hii (ya sasa), huyo ni muongo."
[As-Saduq, Kitabu'l-I`tiqadat (Tehran: 1370 AH) Uk. 63; Tafsir ya kiingereza, The Shi'ite Creed, tr. A.A.A. Fyzee (Calcutta: 1942) Uk. 85].

Ili kujua zaidi kuhusu dini ya Kiislamu, tazama Tovuti hii:

http://al-islam.org/faq/

v1.0

**HII SI KWELI!!!**

Wanavyuoni wakubwa wote wa Shi'ah Imaamiya tangu siku za mwanzo hadi karne za sasa wanaamini kuwa Qur'an imehifadhiwa kikamilifu. Wanavyuoni mashuhuri wa Shia wa mwanzoni wamesema hivi wazi katika vitabu vyao, miongoni mwao ni:

- Shaykh al-Saduq (aliyefariki 381 AH), *Kitabu'l-Itiqadat*, (Teheran.1370) Uk. 63;
- Shaykh al-Mufid (aliyefariki 413 AH), *Awa'ilu l-Maqalat*, Uk. 55-6;
- Sharif al-Murtadha (aliyefariki 436 AH), *Bahru 'l-Fawa'id* (Teh, 1314) Uk. 69;
- Shaykh at-Tusi (aliyefariki 460 AH), *Tafsir at-Tibyan*, (Najaf, 1376), Juz. 1 Uk. 3;
- Shaykh at-Tabrasi (548AH), *Majma'u 'l-Bayan*, (Lebanon), Juz. 1 Uk. 15.

Baadhi ya Wanavyuoni waliokuja baadaye waliotoa maoni kama hayo ni:

- Muhammad Muhsin al-Fayd al-Kashani (aliyefariki 1019 AH), *Al-Wafi*, Juz. 1 Uk. 273-4, na *al-'Asfa fi Tafsir al-Qur'an*, Uk. 348;
- Muhammad Baqir al-Majlisi (aliyefariki 1111 AH), *Bihar al-'Anwar*, Juz 89 Uk. 75.

Imani hii iliendelea bila ya kukatizwa mpaka leo hii. Wanavyuoni wa Shia wa karne hii waliokariri imani hii, kwamba Qur'an imehifadhiwa kikamilifu na haikubadilishwa, ni wale miongoni mwa wenye majina mashuhuri kama vile Sayyid Muhsin al-Amin al-'Amili (aliyefariki 1371 AH); Sayyid Sharaf al-Din al-Musawi (aliyefariki 1377 AH.); Shaykh Muhammad Husein Kashif al-Ghita' (aliyefariki 1373 AH); Sayyid Muhsin al-Hakim (aliyefariki 1390 AH); 'Allamah at-Tabataba'i (aliyefariki 1402 AH); Sayyid Ruhullah al-Khumayni (aliyefariki 1409 AH); Sayyid Abu al-Qasim al-Khu'i (aliyefariki 1413 AH) na Sayyid Muhammad Ridha al-Gulpaygani (aliyefariki 1414 AH).

**Hii, kwa kweli, si orodha nzima.**

**Swali: Lakini ni vipi kuhusu Mashia waliokuwapo kabla ya Wanavyuoni hawa, je wao waliamini tahrif?**

Hapana! Hebu chukulia mfanio wa **'Ubaydullah b. Musa al-'Absi** (120-213 AH), Mwanachuoni wa Shia mwaminifu ambaye masimulizi yake kutoka kwa Maimamu yanapatikana katika mkusanyo wa Hadith wa Shia kama vile *al-Tahdhib* na *al-Istibsar*. Hebu na tuangalie baadhi ya Wanavyuoni wa Sunni wanasema nini kumhusu:

- "... ni mcha Mungu, miongoni mwa Wanavyuoni muhimu wa Shia ...alikubaliwa kuwa mwaminifu na Yahya b. Ma'in. Abu Hatim amesema: 'Alikuwa mwaminifu, mkweli...' al-'Ijli amesema kwamba yeye alikuwa ni mtu mwenye cheo kikuu katika elimu ya Qur'an..." [Al-Dhahabi, *Tadhkirat al-Huffaz* (Haydarabad, 1333 AH), Juz. 1 Uk. 322]
- "...Yeye alikuwa ni Imam katika Fiqh, Hadith na Qur'an, alisifika kwa uchaji Mungu na wema, lakini alikuwa mmoja kati ya wakuu wa Shia."

[Ibn al-'Imad al-Hanbali, *Shadharat al-Dhahab* (Cairo, 1350 AH), Juz. 2 Uk. 29]

**Kama wanavyuoni hawa wa Sunni wangeona kuwa yeye aliamini kuwapo kwa Qur'an nyingine, basi hata mmoja wao asingelimsifu kwa ujuzi wake!**

Na Ubaydullah alikuwa akichukuliwa kuwa ni mwaminifu sana, licha ya kuwa alikuwa ni Shia, kiasi kwamba Wanavyuoni maarufu wa kisunni wa Hadith, al-Bukhari, Muslim na wengineo wengi, katika mikusanyiko ya Hadith, wamechukuwa Hadith kutoka kwake!
[*The Creed of the Imaam of Hadeeth al-Bukhari* (Salafi Pub., UK, 1997), Uk. 87-89]

**Swali: Je Shia hawaamini *Msahafu wa Fatimah* ambao mkubwa mara tatu ya ukubwa wa Qur'an?**

Qur'an ni *Mushaf* (Kitabu), lakini, si kwamba kila kitabu lazima kiwe Qur'an! Hakuna kamwe "Qur'an ya Fatimah"! *Mushaf Fatimah* kilikuwa ni kitabu kilichoandikwa au kuelezwa na Fatimah (a.s.) baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w). Hicho si sehemu ya Qur'an na hakina uhusiano wowote na amri za Mwenyezi Mungu au hukmu za kisharia.

**Swali: Lakini je, hakuna Hadith katika vitabu vya Shia zinazotaja Aya za Qur'an zenye maneno mengine zaidi ya hii tuliyo nayo leo?**

Kuna baadhi ya mifano ambapo maneno zaidi yametajwa lakini kwa minajili ya kufafanua tu, haimaanishi kwamba Aya asili za Qur'an zimegeuzwa. Hii hutokea pande zote, kwa upande wa Shia na wa Sunni. Hebu zingatia mifano ifuatayo, yote ni kutoka upande wa sherhe maarufu za Qur'an za Sunni:

- "Ubayy b. Ka'b alikuwa akisoma '…basi wale mnao faidi nao ***kwa kipindi maalum***, wapeni mahari yao kama ilivyoamriwa…' (Qur'an, Sura 4, Aya 24), na Ibn Abbas pia alikuwa akisoma hivyo hivyo."
  [Fakhr al-Din al-Razi, *Mafatih al-Ghayb* (Beirut, 1981), Juz. 9 Uk. 53]
  [Ibn Kathir, *Tafsir al-Qur'an al-'Adhim* (Beirut, 1987), Juz. 2 Uk. 244]

Maelezo yaliyomo katika hashia ya Tasfir ya Ibn Kathir yanafafanua kwamba maneno yaliyoongezwa hapo juu, ambayo si sehemu ya Qur'an, yalisomwa na maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.) **kwa ajili ya *tafsir* na ufafanuzi tu.**

- "Ibn Mas'ud amesema: "Wakati wa Mtume (s.a.w.w.) tulikuwa tukisoma, 'Ewe Mtume wetu (Muhammad) fikisha lile ulilotumwa kutoka kwa Mola wako ***nalo ni 'Ali ni Bwana wa Waumini*** na kama hukufanya, basi hujafikisha ujumbe Wake.'" (Qur'an Sura 5, Aya 67).
  [Jalal al-Din al-Suyuti, *Durr al-Manthur*, Juz. 2 Uk. 298]

Katika hali hii pia inavyoonyesha, kipande kilichoandikwa kwa mshazari (*italics*) kwa hakika si sehemu ya Qur'an, hata hivyo, swahaba Ibn Mas'ud alikuwa akisoma hivyo alipokuwa akifafanua ufunuo wa Qur'an.

Jabir ibn Samura amesimulia: Nilimsikia Mtume (saww) akisema: “Kutakuwa na Maimamu kumi na wawili.” Kisha akatamka sentensi ambayo sikuweza kuisikia. Baba yangu akasema, Mtume aliongeza, “Na wote watatokana na Maquraysh.” [*Sahih al-Bukhari* ( Ya Kiingereza), Hadithi namba 9.329, Kitabul Ahkam; *Sahih al-Bukhari*, (Ya Kiarabu), 4:165, Kitabul Ahkam]

Mtume (saww) akasema: “Dini (Uislamu) itaendelea mpaka Saa (ya Kiyama), na kuwepo kwa Maimamu kumi na wawili kwa ajili yenu, wote watatokana na Maquraysh.”
[*Sahih Muslim*, (Ya Kiingereza), Sura ya 754, juzuu ya 3, uk1010, Hadith namba 4,483, *Sahih Muslim* (Ya Kiarabu), Kitab al-Imaara, 1980 Toleo la Saudi Arabia, Juzuu ya 3, Uk 1453, Hadith namba 10]

# Ni nani hawa Maimamu kumi na wawili wa Mtume (s.a.w.w)?

**Mkanganyiko?**

Tunahitaji mwanachuoni mwingine wa Sunni wa kuhitimisha ufafanuzi wa hawa maimamu kumi na wawili, Makhalifa, viongozi na Maimamu hasa ni nani:

Al-Dhahabi mwanazuoni maarufu anasema katika Tadhkirat al-Huffaz, Juz. 4, Uk. 298, na Ibn Hajar al-'Asqalani anasema katika al-Durar al-Kaminah, Juz. 1, Uk. 67 kwamba Sadruddin Ibrahim bin Muhammad bin al-Hamawayh al-Juwayni al-ash-Shaafi'iy alikuwa mwanachuoni mkubwa wa Hadithi. Al-Juwayni amesimulia hivyohivyo kutoka kwa Abdullah ibn Abbas (R) kutoka kwa Mtume (S) ambaye alisema, "Mimi ni kiongozi wa Manabii na Ali ibn Abi Talib ni kiongozi wa

maimamu, na baada yangu mimi, maimamu wangu watakuwa kumi na wawili, wa kwanza wao atakuwa Ali ibn Abi Talib na wa mwisho wao atakuwa Al Mahdi. "

Al-Juwayni pia anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas '(R) kutoka kwa Mtume (s.a.w.w): "Hakika Maimamu wangu na warithi wangu na watakaomthibitisha Mwenyezi Mungu juu ya viumbe wake baada yangu ni kumi na wawili. Wakwanza wao ni ndugu yangu na wa mwisho wao ni mjukuu wangu. " Mtume aliulizwa: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni nani huyo ndugu yako?" Alisema, "Ali ibn Abi Talib". Kisha wakamuuliza, "Na ni nani huyo mtoto wako?" Mtukufu Mtume (S) akasema, ni "Al Mahdi, ambaye ataujaza ulimwengu kwa haki na usawa kama utakavyo kuwa umejaa dhuluma na uadui. Na ndiye atakaye ninyanyua mimi kama muonyaji na kutoa habari njema kwa viumbe, hata kama siku itabakia kwa ajili ya maisha ya dunia, na Mwenyezi Mungu Mtukufu atairefusha siku hii kwa kiasi fulani mpaka atakapo mtuma mtoto wangu Mahdi, kisha atampeleka dhuria wake ‘Ru’uhullah’ Isa ibn Maryam (a.s) na ataomba nyuma yake ( imam Mahdi ). Na dunia itakuwa imeenea mwanga na nuru yake. Na nguvu au uwezo wake utaenea pande zote za mashariki na magharibi. "

Al-Juwayni pia anasimulia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (S) ametujulisha:. "Mimi na Ali na Hasan na Husayn na tisa watokanao na Husayn ndio watwaharifu na maasuum" [Al-Juwayni, Fara'id al-Simtayn, Mu'assassat al-Mahmudi li-Taba'ah, Beirut 1978, Uk. 160.]

Miongoni mwa fikra au mawazo ya wanazuoni wengi wa Kiislamu, ni Shia Imamiyyah Ithna Ashariyyah '(Maimamu kumi na wawili wa Ki’shia) huamini maimamu hawa kumi na wawili kama watwaharifu wa Mtume(s.a.w.w) na kupata uelewa wa Uislamu kutoka kwao. Ili kujua zaidi juu ya Uislamu sahihi, tembelea tovuti:

***http://al-islam.org/faq/***

| **Wanavyuoni wa Sunni wanasema nini:** | |
|---|---|
| Ibn al-'Arabi: | Tumehesabu Maimamu baada ya Mtume (s.a.w.w) wako kumi na wawili. Tuliwapata kama ifuatavyo: Abu Bakr, ‘Umar,’ Uthman, Ali, Hasan, Mu’awiyah, Yazid, Mu’awiyah ibn Yazid, Marwan, ‘Abd al-Malik ibn Marwan, Yazid bin’ Abd al-Malik, Marwan bin Muhammad bin Marwan, As-Saffah … Baada ya hao kulikuwa na makhalifa 27 kutoka Bani Abbas.<br>Ikiwa tutafikiria kumi na wawili miongoni mwao tunaweza kufika mpaka kwa Sulayman. Ikiwa tutachukulia maana halisi, sisi tunao watano miongoni mwao na kwa hao tunaongeza Makhalifa wema wanne, pamoja na ‘Umar bin’ Abd al-Aziz …<br>**Siwezi kuelewa maana ya Hadithi hii.**<br>[Ibn al-'Arabi, *Sharh Sunan Tirmidhi*, 9:68-69] |

| | |
|---|---|
| Qadi 'Iyad al-Yahsubi: | Qadhi ‘Iyad al-Yahsubi: Idadi ya Makhalifa ni zaidi ya hao. **Kupunguza idadi yao hadi kumi na mbili sio sahihi.** Mtume (saww) hakusema kuwa kutakuwa na Maimamu kumi na wawili tu na hakuna wigo kwa idadi hiyo. Hivyo inawezekana kwamba kuna zaidi ya hao. [Al-Nawawi, *Sharh Sahih Muslim*, 12:201-202; Ibn Hajar al-'Asqalani, *Fath al-Bari*, 16:339] |
| Jalal al-Din al-Suyuti: | **Kuna Makhalifa kumi na wawili tu mpaka Siku ya Malipo.** Na wao wataendelea kutenda mema, hata kama sio kwa mfululizo (kufuatana). Tunaona kwamba kutoka katika hao kumi na wawili, wanne ni Makhalifa wema, kisha Hasan, kisha Mu’awiyah, kisha Ibn Zubayr, na hatimaye ‘Umar bin’ Abd al-Aziz. Wao ni nane. Wanne miongoni mwao wamebaki. Labda Mahdi, Abbas anaweza kuwa ni pamoja na hao kama yeye ni Abbasid kama ilivyo kwa ‘Umar bin’ Abd al-Aziz alivyokuwa Umayyad. Na Tahir Abbasi ‘pia awe miongoni mwao kwa sababu alikuwa mtawala. **Hivyo wawili bado hawajafika**. Mmoja wao ni Mahdi, kwa sababu yeye anatokana na Ahlul Bayt (a.s). [Al-Suyuti, *Tarikh al-Khulafa*, Page 12; Ibn Hajar al-Haytami, *Al-Sawa'iq al-Muhriqa* Page 19] |
| Ibn Hajar al-'Asqalani: | **Hakuna mwenye maarifa mengi zaidi kuhusu Hadith maalumu ya *Sahih Bukhari*.** Sio sahihi kusema kwamba hawa Maimamu watakuwepo kwa sasa na kwa wakati mmoja (wakati huo huo). [Ibn Hajar al-'Asqalani, *Fath al-Bari* 16:338-341] |

| | |
|---|---|
| Ibn al-Jawzi: | Khalifa wa kwanza wa Bani Umayya alikuwa Yazid ibn Mu’awiyah na wa mwisho ni, Marwan Al-Himar. **Jumla yao ni kumi na tatu. ‘Uthman, Mu’awiyah na ibn Zubayr hakuhusishwa kama walikuwa miongoni mwa maswahaba wa Mtume (S).** Kama tukimtenga Marwan bin al-Hakam kwa sababu ya utata wake kuhusu kuwa swahaba au kwamba alikuwa katika utawala hata kama Abdullah ibn Zubayr alikuwa akiungwa mkono na watu. **Basi tunaweza kupata idadi ya kumi na wawili.** … Wakati Khalifa alipotoka kwa Bani Umayya, mvurugano mkubwa uliibuka. Mpaka Bani Abbas walipo simama imara wenyewe. Hivyo, mazingira ya asili yalibadilika kabisa. [Ibn al-Jawzi, *Kashf al-Mushkil*, as quoted in Ibn Hajar al-'Asqalani, *Fath al-Bari* 16:340 from Sibt Ibn al-Jawzi] |

| | |
|---|---|
| Al-Nawawi: | Inaweza pia kuwa na maana kwamba Maimamu kumi na wawili watabakia mpaka wakati wa kipindi cha mamlaka ya juu kabisa katika Uislamu. Wakati ambao Uislamu utakuwa ndio Dini inayotawala. **Makhalifa hawa watakuwepo, wakati wa umiliki wao, na kuitukuza Dini.** [Al-Nawawi, *Sharh Sahih Muslim* ,12:202-203] |
| Al-Bayhaqi: | **Hii idadi ( ya kumi na wawili) itaonekana mpaka muda wa Walid ibn Abd al-Malik. Baada ya hapo, kutakuwa na machafuko na usumbufu.** Hapo, itakuja kutokea nasaba ya Abbasid. Taarifa hii itaongeza idadi ya Maimamu. Kama tutaacha baadhi ya tabia zao ambazo zitakuja baada ya mvurugano, basi idadi yao itakuwa kubwa sana. "[Ibn Kathir, *Ta'rikh*, 6:249; Al-Suyuti, *Tarikh al-Khulafa* Page 11] |
| Ibn Kathir: | Kila ambaye ataifuata tafsir ya Bayhaqi na kukubaliana na madai yake kwamba Jama'ah ina maana ya hao Maimamu wote ambao watakuja kwa vipindi mpaka wakati wa **Walid ibn Yazid ibn 'Abd al-Malik mhalifu** atokeaye chini ya upeo wa macho ya mapokeo tuliyoyanukuu na kukosoa na kuwalaani watu wa aina hiyo.<br>Na kama tungekubali ukhalifa wa Ibn Zubayr kabla ya 'Abd al-Malik **jumla ya maimamu ingekuwa kumi na sita.** Ambapo jumla yao inapaswa kuwa kumi na wawili kabla ya 'Umar ibn' Abd al-Aziz. **Katika njia hii Yazid ibn Mu'awiyah atakuwemo na sio 'Umar ibn' Abd al-Aziz.** Hata hivyo, imethibiti kwamba wengi wa Maulamaa wamekubali kuwa 'Umar ibn' Abd al-Aziz ni mkweli na Khalifa muaminifu. [Ibn Kathir, *Ta'rikh*, 6:249-250] |



# Umuhimu wa Ijtihad na Taqlid

*"Kama baada ya ghayb ya Qa'im wako kulikuwa hakuna kubakia mtu kutoka miongoni mwa wasomi ambao:*
*wamekaribishwa upande wake (Imam); kuwaongoza wengine kwake; kuilinda dini yake kwa uthibitisho wa Mwenyezi Mungu (s.w.t); kuwaokoa watumishi wa Mwenyezi Mungu wanaokandamizwa kutoka kwenye mitego ya Iblees (Shetani) na wasaidizi wake, na mitego ya adui (wa Ahlul Bayt), kisha hatabakia mtu (juu ya ardhi) ila yule ambaye ameiacha dini ya Mwenyezi Mungu (s.w.t). Hata hivyo, wasomi hulichukulia hili wenyewe kuwa ni ulinzi wa mioyo ya wafuasi wanaokandamizwa, sawa na nahodha wa mashua anapochukua udhibiti wa maisha na usalama wa walewalioko kwenye meli yake. Hivyo, hawa (wasomi - Ulamaa) ni watu bora mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), Mtukufu na Mkubwa. "*

Biharul Anwar, kitabu cha 2, uk wa 6, sehemu ya. 8, Hadithi namba. 12.

Kujua zaidi kuhusu Uislamu halisi kama ulivyoelezwa na Ahlul-Bayt - tembelea:
www.al-islam.org/faq/

Hadithi ya Mtume Muhammad (S) na warithi wake kumi na wawili pia wamesisitiza juu ya ukweli kwamba lazima wataalamu wawepo ili kuongoza waumini kwenye wajibu wao kwa Muumba, kama ilivyo kwa Imam wa mwisho wa Ahlul Bayt ameeleza: "Hivyo basi, kama ilivyo kwa Fuqaha (msomi) ambaye huilinda nafsi yake mwenyewe, ambaye huilinda dini yake, ambaye anakwenda kinyume na matakwa na tamaa ya chini ya matakwa yake, na ambaye ni mtiifu kwa amri za Bwana wake, basi ni halali kwa watu mashuhuri kuafuata katika masuala ya kidini (kufanya Taqleed yao) na hali hii (ya kiroho) inapatikana tu kwa baadhi ya wanazuoni wa Shia – na sio wote. ". (Wasail ash-Shia, kitabu cha 27., uk 131, Hadith ya 33,401)
Kuna mifano mingi, wakati wa uhai wa Mtume Muhammad (S) na Maimamu wake waliotakasika na ambao huwaelekeza jamaa zao ili kuwaongoza wafuasi wao katika maeneo ya mbali na kuwafundisha mbinu za jinsi ya kupata sheria za Kiislamu kwa ajili ya 'masuala mapya' ambayo yanajitokeza

**Mazingira muhimu kwa sifa za kuwa Mujtahid**

ni kuelewa maandiko ya dini ambayo hujitokeza kwenye utaalamu wa Fiqh ya Kiislamu na nyingine katika sayansi ya Kiislamu, yenyewe haijitoshelezi kwa ajili ya sifa za kuwa Mujtahid ambaye kila mtu anaweza kumfuata. Mbali na kiwango cha juu cha masomo ya Kiislamu ambayo ni lazima mtu awe ameyaelewa, sheria ya Kiislamu inasema kwamba Mujtahid lazima awe ni mtu huru (amezaliwa kihalali na ambaye amefikia kipindi cha umri wa kubaleghe, akili timamu, Ithna -Asheri Shia na mtu ambaye ni, Adil - tabia ambayo inaweza kutafsiriwa kama 'tu' ni pamoja na maadili na sifa za kisheria, kama vile ucha - Mungu na kujitenga na yale yote yaliyokatazwa na Shari'ah na kutimiza majukumu yake yote.

**Ni kwa jinsi gani muumini wa kawaida huweza kugundua ni nani Mujtahid anayeweza kumfuata**

Kuna njia tatu za kutambua: 1) Maarifa binafsi kama yeye ni msomi wa dini, 2) Ushahidi wa watu wawili (waadilifu) Adil, na mtu mwenye ujuzi wa kuwa Mujtahid; 3) Kiwango cha umaarufu ambacho kitaondoa shaka ya mtu kuwa Mujtahid. Aidha, siku hizi wasomi hudumisha tamaa ya kufuata Mujtahid ambaye ni al-A'lim. Katika wazo la jumla hii ina maana ya mjuzi zaidi', lakini katika mazingira haya maalumu ina maana, mwanasheria ambaye ana utaalamu mkubwa uliotokana na maamuzi ya Shari'ah kutoka kwenye vyanzo. Kujifunza zaidi kunaweza kuwa na kutambuliwa katika moja ya njia tatu zinazopelekea mtu kuwa Mujtahid, hata hivyo wakati mwingine ni vigumu kwa wasomi wa Ki,Shia kutofautisha kati ya wanasheria, ni yupi ambaye ni msomi zaidi Matokeo yake, Mujtahid zaidi ya mmoja anaweza kufuatwa katika taqleed kwa wakati mmoja (ingawa sio tu, kwa mtu huyohuyo), kama ilivyo sasa ambapo kuna zaidi ya wasomi kumi na tano ambao waumini wanaweza kuchagua kuwafuata, lakini yeyote katika mlolongo huu, haina maana katika kila tendo kutokukubaliana juu ya masuala muhimu ya kisheria ndani ya jumuiya ya Mashia

Wakati wa maisha ya Mtume Muhammad (amani iwe juu yake na familia yake), alikuwa na mamlaka pekee katika masuala yote ya kidini na kisiasa, na masuala ya dini au masuala ya kushughulika na jamii yalikuwa yakipelekwa kwake au kwa mtu ambaye amewekwa katika mamlaka (kwa amri ya Mwenyezi Mungu) juu ya Waumini. Pamoja na kufariki kwake, mlolongo wa warithi – Maimamu kumi na wawili - kuanza. Wakwanza wa viongozi wa waziwazi kuteuliwa alikuwa Ali ibn Abi Talib (a.s) na mrithi wa mwisho ni Imam wa 12, al-Hujjat ibnil Hasan al- Askari (Mwenyezi Mungu aharakishe ujio wake).

Uongozi wa Maimamu kumi na wawili ulikuwa tofauti kabisa na ule wa Maimamu kumi na moja waliotangulia tangu kutokea kwa hekima ya Mwenyezi Mungu (s.w.t), alipotakiwa kwenda katika pande mbili tofauti na aina tofauti ya ghaibu. Ghaibu yake ndogo ilidumu kidogo kwa zaidi ya miaka 60 wakati ambapo wawakilishi maalum wa nne waliteuliwa.

Waliwajibika kwa ajili ya usambazaji maswali na masuala muhimu toka kwa mu'umini mpaka kwa Imam, siku hadi siku, na kukusanya fedha mbalimbali za hazina ya Kiislamu (Khums, Zakat, nk.) na kuzisambaza kama Imam akiona inafaa, kwa shughuli nyingine.
Baada ya kifo cha mwakilishi wa nne katika mwaka 328 AH, milango maalum ya uwakilishi ilifungwa. Hata hivyo, uongozi haukukoma na kulingana na maelekezo yaliyotolewa na Imam wa kumi na mbili (Mahd), walipaswa kuwafuata wasomi (Fuqaha) ambao: "... ni walinzi wa nafsi zao, huilinda dini yao, na hufuata maagizo ya Bwana wao (Mwenyezi Mungu (s.w.t )..." Hivyo, 'uwakilishi wa jumla' umewekwa juu ya mabega ya vyanzo vya tabia (Mara'ja Taqleed).

## <u>Taqleed ni nini?</u>

Taqleed inatoka kwenye mzizi wa neno la Kiarabu la qal-la-da/yuqal-li-du/taqleed' maana yake ni 'kuiga' au 'kufuata'. Haina maana "kufuata kibubusa" kama wengine wanavyolitafsiri - badala yake, katika mfumo wa kazi hii ya sheria za Kiislamu, ina maana kwamba tokea mtu asiwe na uwezo wa kuendesha sheria za Kiislamu kutoka kwenye vyanzo vyake, inahusu na kutekeleza hukumu ambayo msomi aliye na uwezo wa kutunga, masuala.
Hatulazimishwi kufuata Taqleed, badala yake kama wasomi wamearifu, chaguo letu la kwanza ni kuwa Mujtahid - mtu ambaye amefikia kiwango cha Ijtihaad - na uwezo wa kujitegemea kuandaa sheria za Uislamu kutoka vyanzo vyao, na huu ni wajibu juu ya waumini wote, hata hivyo kama mtu mmoja anatimiza kazi hii, basi wote tunaondokewa na dhima.
Tangu kufikia ngazi hiyo haiwezekani kwa kila mtu - na kwa sababu ya ukweli kwamba kama kila mtu atakuwa akijitolea maisha yake kwa 'masomo ya Kiislamu' tunaweza kupungukiwa kuwa na wanasayansi, madaktari, wahandisi, wasanii, wabunifu, nk .. chaguo la pili tulilopewa ni kufanya hadhari (Ihtiyaat)

katika sheria ya Kiislamu.
Kama mtu anaamua kufuata njia hii, kisha juu ya suala fulani, lazima kupitia maamuzi ya Kiislamu ambayo yote ni ya Mara'ja wa kisasa waliotoa na kuchagua "zaidi ya tahadhari" makhsusi. Tangu njia ya pili kuwa ngumu kuifuata, chaguo zaidi la kivitendo ni kwamba turejee kwa wataalamu ambao wamefikia uwezo wa kutuongoza sisi kwenye majukumu yetu – tutekeleze Taqleed yake na kujinyenyekesha kwenye hitimisho lake.

Hivyo, kwa kurejea kwa mtaalam, Waumini wameondoa shaka katika kutimiza majukumu yao (ya kutekeleza sheria na hukumu za Kiislamu) kama ilivyo katika kufuata sheria ya msomi anayetambuliwa.

Ikumbukwe kwamba Taqleed anafungamana kwenye eneo la Shari'ah tu, kuna uwezekano wa kutokuwa na Taqleed katika mambo muhimu ya imani (Usulu'd-din). Muislamu ni lazima kushikilia imani yake katika misingi ya dini yake baada ya kufikia kusadikisha ukweli wao kwa njia ya uchunguzi na kutafakari. Kwa hakika Qur'an iko wazi sana na inawalaani wale ambao hufuata wengine kwa upofu katika mambo muhimu ya imani

Hata hivyo, ili matendo ya ibada ya mtu yawe yamefanyika kiusahihi na kukubalika, lazima yafanyike chini ya kivuli cha moja ya chaguzi tatu hapo juu – kushindwa kufikia kiwango cha Mujtahid, sio kutekeleza Ihityaat, na sio kufuata Taqlid ya Marja anayetambuliwa, 'inaweza kupelekea matendo yote ya mtu (kama vile swala na funga) kufutwa na kutupwa.

**<u>Ushahidi wa kimantiki juu ya Taqleed</u>**

Kama vile katika nyanja yoyote ya maisha yetu,  Tunarejea kwa wataalamu wa kutatua matatizo yetu tangu tusiwe na uwezo wa mamlaka katika kila kipengele na katika mambo muhimu kama vile uhandisi, dawa, vipimo vya macho, kukarabati magari, nk ... daima tunapeleka matatizo yetu kwa wale ambao ni  wasomi na kujikita katika eneo maalumu la maisha. Kidini sheria na tafsiri havina tofauti na hivyo, mantiki inatuonyesha kwamba kama sisi sio katika ngazi ya uelewa wa Shari'ah, lazima kuuliza wale ambao wamefikia hatua hiyo

**<u>Ushahidi wa maandiko juu ya Taqleed</u>**

Qur'an imerejea kuawafuata 'wengine' (katika muongozo wa dini) na idadi ya matukio. Katika Qur'an sura ya 9 aya ya 122 tunaelezwa:
Wala haiwafalii waumini kutoka wote. Kwa nini kisitoke kikundi katika kila kundi miongoni mwao kujifunza dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia. Ili wapate kujihadhari.
Aya hii inaonyesha kuwa kundi la watu lazima lienda mbele kupata uelewa wa kina wa dini, na wakati wa kurudi kutoka masomoni na wengine kurudi nyumbani kutoka kwenye uwanja wa vita, ni juu yao kuwafundisha na kuwaelekeza waumini kuhusiana na majukumu ya dini yao.

*"Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkaswali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu na miguu yenu mpaka vifundoni…*

*na ikiwa hamkupata maji, basi fanyeni tayammum ya udongo (mchanga) ulio tohara na kupaka nyuso zenu na mikono yenu."*
(Qur'an: Sura 5, Aya 6)

# Jinsi ya kutawadha na kufanya *Tayammum*

Kabla ya kuswali Swala za kila siku, au ibada zingine kuna masharti ya wajib au ya sunna yapaswayo kufanywa, Waislamu ni lazima wajitoharishe – huku, kwa kawaida, hufanywa kwa kutumia maji. Tendo hili dogo la kujitoharisha kwa maji linaitwa *Wudhu*, na lile kubwa linaitwa *Ghusl*. Kama hakuna maji, kujitoharisha kunaweza kufanywa kwa kutumia mchanga au udongo ulio tohara, huku kunaitwa *kutayammam*.

## Wakati gani wa kufanya *Tayammum*

Unatakiwa kufanya *Tayammum* badala ya *Wudhu* au *Ghusl* pale inapokuwa:

1. Hakuna maji ya kutosha kwa ajili ya kufanya *Wudhu* au *Ghusl*.
2. Kutumia maji kwa ajili ya *Wudhu* kutahatarisha maisha yako au mali au huwezi kupata maji kwa njia yoyote.
3. Matumizi ya maji pekee yaliyoko yatasababisha kusiwe na maji ya kutosha kwa kunywa na hivyo kuleta kifo kwa kiu au maradhi, au kusababisha matatizo kwako na kwa wanaokutegemea.
4. Kuosha uso wako na mikono yako kwa maji kutahatarisha afya yako.
5. Maji ya kutosha yapo, lakini huna ruhusa ya kuyatumia.
6. Kuna uwezekano kwamba kutawadha (*Wudhu)* au kuoga (*Ghusl)* kutasababisha kwisha kwa muda wa Swala nzima au sehemu yake.
7. Ikiwa mwili au vazi limenajisika (*najis*) na mtu ana maji machache ambayo iwapo atatawadha kwayo (*Wudhu)* au aoge (*Ghusl)*, basi hakutasalia maji ya kutosha kutoharisha mwili au nguo yake kwa ajili ya Swala.

## Jinsi ya kutayammamu (Kufanya *Tayammum*)

**Niyya** : Tia niya: "Natayammamu badala ya *Wudhu* (au *Ghusl*), kwa ajili ya kutaka radhi na ukuruba wa Mwenyezi Mungu." (Hii husomwa kwa kiarabu).

**Hatua 1** : Piga viganja vya mikono yote miwili kwa pamoja juu ya ardhi, au mchanga, au juu ya jiwe ambalo ni kavu na safi. (**Tazama picha Na. 1**).

**Hatua 2** : Pangusa kwa viganja vyote viwili kwa pamoja kuanzia mwanzo wa komo la uso pale nywele zinapoanza kuota, kisha uendelee hadi chini hadi kwenye muanzi wa pua, sehemu zote mbili za uso zinazoungana na masikio, na juu ya nyusi. (**Picha 2,3**).

**Hatua 3** : Kisha futa kiganja cha mkono wa kushoto juu ya nyuma ya mkono wote wa kulia kuanzia kwenye mfupa wa kiwiko mpaka kwenye hadi kwenye ncha za vidole. (**Picha Na. 4**).

**Hatua 4** : Kisha futa kiganja cha mkono wa kulia juu ya nyuma ya mkono wote wa kushoto.

**Hatua 5** : Piga viganja vyote pamoja chini kwa mara ya pili kama ulivyofanya katika hatua ya 1.

**Hatua 6** : Rudia hatua 3.


**Hatua 7** : Rudia hatua 4.



**Picha 1**



**Picha 2**



**Picha 3**



**Picha 4**

**Kwa maelezo zaidi juu ya ibada na mambo ya kidini au *Wudhu*, *Tayammum*, na *Ghusl*, Tazama Tovuti:**

***http://al-islam.org/ritualandspiritual/***

*v1.0*


**Wakati wa kutawadha**
Ni wajibu kwa kila Muislamu kuwa tohara kabla ya Swala za kila siku. Ni lazima pia awe tohara kabla ya kufanya ibada nyinginezo, kama vile Swala za Sunna, kugusa maandishi ya Qur`an na anapokuwaa kwenye ibada za kuhiji (hajj). Katika hali nyingi, yatosha kutawadha tu ili kuwa tohara, lakini, mara nyingine, lazima mtu aoge (Ghusl). Ni vizuri ufahamu kwamba Ghusl haijaelezwa katika makala hii.

**Jinsi ya kutawadha**
Niyya : Tia nia kwa kusema: 'Nanuia kutawadha kwa kumridhisha na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.' (Hii husemwa kwa kiarabu).

Kuosha uso : Kwanza: Kabla ya kutawadha, ondoa chochote, juu ya uso au mikono, kitakachozuia maji kufika kwenye ngozi (hivyo ni vitu k.v. saa, pete n.k. au hata rangi, au chochote kitakachokuwa ni kizuizi juu ya ngozi). Teka maji kwenye kiganja cha mkono wa kulia na uyamimine usoni, kuanzia juu (juu kidogo ya paji la uso). Kisha, ukitumia mkono wa kulia, upake uso wako kuanzia pale nywele zinapoota mpaka chini ya kidevu, kwa namna ambayo maji yatafika sehemu ya uso wote, na mzunguko wote wa uso pale unapofika mkono kutoka kwenye kidole cha kati mpaka kwenye kidole gumba. Ili kuhakikisha kuwa sehemu yote imeoshwa ikiwa ni pamoja na sehemu ya ndani ya pua yako, midomo miwili na macho. Hata hivyo, huhitajiki kuosha sehemu zote za ndani za viungo hivi. Ni wajibu kuosha mara moja, kama ilivyoelezwa. Kuosha mara ya pili ni sunna, ambapo kuosha mara kwa mara baadaye kumekatazwa.




Kuosha mikono: Huku ukitumia mkono wako wa kushoto, mimina maji juu ya mkono wako wa kulia kutoka kwenye kiwiko cha mkono mpaka kwenye ncha za vidole, kisha, kwa mkono huo huo futa maji juu ya pande zote za mkono ili kuhakikisha kwamba sehemu zote zimeoshwa. Kisha fanya hivyo hivyo juu ya mkono wa kushoto kwa kutumia mkono wa kulia. Kuosha lazima kuanzie kutoka kwenye viwiko hadi kwenye ncha za vidole, na si kinyume chake. Mimina maji kutoka juu kidogo ya kiwiko kuhakikisha kwamba mkono wote umeoshwa. Osha kwa namna ambayo maji yataingia ndani ya nywele, kama ziko, na kufikia kwenye ngozi. Vivyo hivyo, kuosha mara moja ni wajibu kama ilivyoelezwa. Kuosha mara ya pili ni sunna na kuosha mara kwa mara baadaye kumekatazwa.




**Jinsi ya kuosha uso na mikono:**
- Osha kwa kumimina maji kuanzia juu kuelekea chini. Ama kuosha kwa namna nyingine kutatengua Wudhu wako.
- Kwa ujumla, osha zaidi kidogo ya inavyotakiwa ili kuhakikisha kwamba sehemu zote zimepata maji.

**Kupaka uso** : Kisha, paka sehemu ya mbele-robo ya kichwa, kwa majimaji yaliyobaki kwenye mkono wako wa kulia. Futa kuanzia sehemu ya juu ya kichwa kuelekea chini (kutokea nyuma ya uso kuelekea usoni). Ni sunna kupaka japo kwa kutumia urefu wa kidole kimoja. Yawezekana pia kupaka kwa kidole kimoja tu; hata hivyo imependekezwa kutumia vidole vitatu kwa pamoja (Cha kati, cha shahada na cha pete). Hayo majimaji ni lazima yafike kwenye ngozi ya kichwa, lakini kama nywele ni fupi sana zisizochanika, basi yatosha kupaka nywele zako tu. Wakati ukipaka kichwa chako, mkono wako hautakiwi uguse sehemu ya mbele ya uso wako. Vinginevyo, itasababisha maji yaliyoko usoni kuchanganyika na umajimaji ulioko kwenye mkono wako, na hii itafanya upakaji wa wako wa mguu wako ubatilike, kwa sababu kitendo cha kupaka ni lazima kifanywe na majimaji yaliyo mikononi tu.



**Kupaka miguu** : Mwisho, paka miguu yako kwa majimaji yaliyobaki mikononi mwako. Paka kuanzia kwenye ncha ya kidole mpaka kwenye maungio ya kifundo cha mguu. Paka mguu wako wa kulia kwa kutumia mkono wako wa kulia, na mguu wako wa kushoto kwa kutumia mkono wa ko wa kushoto. Ni vizuri kupaka kwa kufuatilia upana wa vidole vitatu vya mkono (cha kati, cha pete na cha shahada), na ni vizuri pia kupaka mguu wako wote kwa kutumia mkono wako wote. Na wakati unapopaka mguu, futa kuanzia kwenye mwanzo wa vidole hadi kwenye maungio ya kifundo cha mguu (kama ilivyotajwa hapo awali) kufuatia urefu wancha yakidole mpaka kwenye vifundo. Usiweke tu mkono wako wote juu ya mguu wako na kufuta tu kidogo. Fahamu ya kwamba haijuzu kupaka juu ya soksi au viatu isipokuwa katika hali zisizokuwa za kawaida.



### Mambo yanayohusu kupaka kichwa na miguu:

- Unahitajika uupitishe mkono wako juu wakati unapopaka kichwa na miguu yako. Kuutuliza mkono wako juu ya kichwa au mguu na kisha kuutingisha mguu au kichwa chako kutabatilisha *Wudhu* wako. Hata hivyo , hapana ubaya iwapo kichwa au mguu wako utatingishika kidogo wakati unapopaka.
- Sehemu unazozipaka ni lazima ziwe kavu kabla ya kuzipaka, iwapo zitakuwa majimaji sana kiasi kwamba majimaji yaliyoko mkononi mwako hayatakuwa na athari yoyote, basi kupaka huko kutabatilika. Ikiwa sehemu uipakayo ina majimaji kidogo, inaruhusiwa kuipaka, mradi tu majimaji yaliyoko mkononi mwako yachanganyike mara moja nayo unapopaka.
- Kupaka ni lazima kufanywe na majimaji yanayobaki mkononi baada ya kuosha. Usiiloweshe mikono yako na maji mengine, au usichanganye mikono yako na majimaji yatokayo kwenye viungo vingine vya *Wudhu*. Iwapo viganja vyako vitakauka kabla ya kupaka (usoni na miguuni), hapo utavitia majimaji yaliyoko kwenye ndevu, masharubu, nyusi, au viungo vingine vya *Wudhu*.

***Na katika usiku amka kwayo ni ziada kwa ajili yako; huenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika.***
*(17:79)*

Mtume Muhammad (s) alisema kuhusu mwezi wa Ramadhani: "Yeyote atakayeanzisha maombi kwa swala za usiku (*Qiyam al-Layl*) katika hiyo na akawa na Imani thabita na akatumainia malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, dhambi zake zote

zilizotangulia zitasamehewa."

[*Sahih al-Bukhari*, juzuu ya 3, Kitabu 32, ukurasa 226]

# Kwa nini Shi'ah huacha mikusanyiko ya swala ya *Tarawih?*

Ahl al-Sunnah kwa ujumla hufikiria kwamba ni *sunnah* kuomba maombi maalum usiku - *Tarawih* - katika mkusanyiko wa swala ya *tarawih* wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan. Ambapo Mashia,humtukuza Allah kwa kutekeleza sawa ibada za sunnah ( swala zilizopendekezwa), hawalazimiki kuswali swala ya *tarawih* katika mkusanyiko. Hii ni desturi ya Mashia kwa mujibu wa maagizo ya *sunnah* za Mtume (saww).

## Je, Maimamu wa Shia wameswali *Tarawih* ?

Imam al-Baqir ('a) na Imam al-Sadiq (a') waliulizwa kuhusu kujuzu kuomba maombi ya hiari kwa mkusanyiko wakati wa usiku wa Ramadhan. Wote wawili wamesimulia mapokeo ya Mtume Muhammad (s) ambapo walisema:

- "**Hakika, mwenye kuswali sunnah (swala za hiari) katika mkusanyiko wakati wa usiku wa Ramadhan ni *BID'AH***... Enyi watu! msiswala swala za sunnah usiku wa Ramadhani katika mkusanyiko .... Bila shaka, kufanya tendo dogo la ibada ambalo ni kwa mujibu wa sunna ni bora kuliko kufanya tendo kubwa la ibada ambalo ni bidah (uzushi)."
  [al-Hurr al-`Amili, *Wasa'il al-Shi`ah*, juzuu ya 8, ukurasa wa 45]

Mtazamo huu wa Maimamu kutoka kizazi cha Mtume imethibitishwa na msomi maalumu miongoni mwa Ahl al-Sunnah ambaye ameandika:

- "Dhuriya wa Mtume (s) kasema kuwa mkusanyiko katika *Tarawih* ni'***BID'AH'***.
  [al-Shawkani, *Nayl al-Awtar*, juzuu ya 3, ukurasa wa 50]

## Wasomi wa Ki'Sunni wanasema nini kuhusu kuswali *Tarawih* nyumbani?

- "Wasomi wamekubaliana juu ya faida zake, lakini wametofautiana ikiwa ni bora kuswali katika nyumba ya mtu mmoja mmoja au katika mkusanyiko msikitini." Al-Nawawi, mchambuzi maarufu wa Sahih Muslim, anaendeleza orodha ya wasomi ambao wameunga mkono mtazamo wa pili na maoni yaliyotawala. Kisha anaandika: "**Malik, Abu Yusuf, na baadhi ya wanazuoni wa Shafi'i, na wengine wanasema kwamba ni bora kuswali mmoja mmoja katika nyumba**".
  [al-Nawawi, *Sharh Sahih Muslim*, juzuu ya 6, ukurasa 286]

## Hitimisho

Mashia siku zote hutamani kuomba swala ya usiku - inayoitwa *Tahajjud* au **Qiyam al-Layl** au *Salat al-Layl* - katika sehemu ya mwisho ya usiku ya kila mwezi, hasa wakati wa Ramadhan. Wao pia hutukuza ibada za ziada wakati wa usiku wa Ramadhan. Hata hivyo, huomba maombi haya ya hiari zaidi katika nyumba zao na kamwe sio katika kusanyiko. Kwa kufanya hivyo wameshikamana na Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad (s).

**Ili kujua zaidi juu ya Uislamu sahihi, tazama Tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

Wanaume na Wanawake kutoka Ahl al-Sunnah huja pamoja katika mikusanyiko ya swala ya*Tarawih* wakati wa jioni mwanzoni kabisa mwa mwezi wa Ramadhani. Husimama katika swala na kusoma Qur'an, na huenda Mwenyezi Mungu (swt) atawalipa thawabu kwa sababu ya nia yao ya dhati na vitendo. Hata hivyo, **neno *Tarawih* kamwe halikutajwa na Qur'an au Mtume (s) na kuelezea ziada ya mkusanyiko wa swala ya jamaa wakati wa jioni wa mwezi wa Ramadhan.** Ni muda wa maendeleo ya baadaye miongoni mwa Waislamu. Kilugha, neno **"*Tarawih*"** ni wingi wa neno la *'tarwiha'* likimaanisha kipindi kifupi cha kupumzika kati ya kila rakaa nne za maombi. Baadaye, kuingia kwa mkusanyiko wa swala ya jamaa katika usiku wa Ramadhan kuliitwa kwa tamko hilo (*Tarawih*).

## Asili ya *Tarawih* kama sala ya jamaa

Ni ukweli uliothibiti kwamba uanzilishi wa *Tarawih*, kama swala ya jamaa usiku wa Ramadhan, inadaiwa kuwepo kwake kwa amri ya Khalifa wa pili, 'Umar bin. al-Khattab

- Amehadithia Abu Hurayra: Mtume wa Allah alisema, "Yeyote mwenye kuswali usiku wote wa mwezi wa Ramadhani akawa na imani ya kweli na matumaini kwa malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa." Ibn Shihab (msimuliaji wakawaida) alisema , "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokufa, watu waliendelea kutekeleza hilo (**yaani swala za sunnah hutekelezwa na mmoja mmoja, si katika mkusanyiko**), na ilibakia hivyo wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr na katika siku za kwanza za 'ukhalifa wa Umar."' Abdur Rahman bin ' Abdul alisema, "Mimi nilienda kwenye kundi la 'Umar bin Al-Khattab usiku mmoja ndani ya mwezi wa Ramadhan kwenye msikiti na nikakuta watu wakiswali katika makundi tofauti - mtu anaswali peke yake, au mtu anaswali kwenye kikundi kidogo nyuma yake. Kisha, 'Umar akasema,' **Kwa maoni yangu mimi** ingekuwa bora kukusanya hawa (watu) chini ya uongozi wa Qari mmoja (msomaji mmoj) [yaani wawe wanaswali katika jamaa]! '. Hivyo, yeye alikusanya mawazo yake kwa kukusanya watu wote (kuswali) nyuma ya Ubayy bin Ka'b. Kisha, usiku mwingine, nilikwenda tena katika kampuni yake na watu walikuwa wamekusanyika nyuma ya msomaji wao. Kwa hayo, **Umar alisema, 'Ni ipi BID'A bora** (**uzushi** katika dini) **ni hii**, lakini maombi ambayo hawakufanya, lakini badala ya kulala kwa wakati wake, ni bora kuliko mtu mwenye kuitekeleza'. Alikuwa na maana kwamba swala katika sehemu ya mwisho ya usiku."
[*Sahih al-Bukhari*, juzuu ya 3, Kitabu 32, namba 227]

- “Imeitwa ***BID’AH*** kwa sababu Mtume (saww) hakuwahi kuiswali swala hiyo katika jamaa, na yawezekana ilikuwa ikiswaliwa kama hivyo wakati wa al-Siddiq (akimaanisha Khalifa wa kwanza), wala sio katika sehemu ya awali ya usiku au kwa idadi ya rakaa hizi ”
[al-Qastallani, *Irshad al-Sari Sharh Sahih al-Bukhari*, juzuu ya 5, ukurasa wa 4]
[al-Nawawi, *Sharh Sahih Muslim*, juzuu ya 6, ukurasa 287]

- “'Umar alikuwa wa kwanza ambaye alitoa mfano wa swala ya usiku wa Ramadhan, *Tarawih*, na kuwakusanya watu kwa ajili yake, na akaelekeza mikoa mbalimbali kuhusu hilo. Hii ilikuwa wakati wa mwezi wa Ramadhan wa mwaka wa 14 (Hijri). Yeye alimteua msomaji wa Qur'an kwa ajili ya watu ambaye aliongoza swala ya *Tarawih* kwa wanaume na wanawake.”
[Ibn Sa’d, *Kitab al-Tabaqat*, juzuu ya 3, ukurasa wa 281]
[al-Suyuti, *Tarikh al-Khulafa'*, ukurasa 137]
[al-‘Ayni, *‘Umdat al-Qari fi Sharh Sahih al-Bukhari*, juzuu ya 6, ukurasa wa 125]

## Mkusanyiko katika Msikiti au mmoja mmoja nyumbani?

Kutekeleza swala za hiari mmoja mmoja ndani ya nyumba mbali na mkusanyiko katika msikiti imependekezwa sana na Mtume (saww) kama ambavyo huleta baraka zaidi kwa ajili ya nyumba na familia na husaidia katika malezi ya Kiislamu ya watoto.

- Mtume (saww) alisema: "Enyi watu! Tekelezeni swala zenu (sunnah) katika nyumba zenu, kwa vile **swala bora ya mtu ni ile anayoiswalia nyumbani kwake, isipokuwa swala ya lazima (jamaa). "**

[*Sahih al-Bukhari*, juzuu ya 9, kitabu cha 92, namba 393]
[al-Nasa'i, *Sunan*, juzuu 3, uk 161, uk 198]

- Mara Abdullah bin Mas'ud akamuuliza Mtume (saww): "Ni kipi bora; kuswali katika nyumba yangu au katika msikiti?" Mtume (saww) akasema: "Je, huoni jinsi gani nyumba yangu ilivyo karibu na msikiti ? **Kuswali katika nyumba yangu ni mapenzi zaidi kwangu kuliko kuswali katika msikiti isipokuwa kwa swala za wajib. "**

[Ibn Majah, *Sunan*, juzuu 1, ukurasa wa 439, namba 1378]

- Amehadithia Zayd bin Thabit: Mtume wa Allah (s) alifanya chumba kidogo (pamoja na mkeka wa majani ya mtende). Yeye (s) akatoka nje (ya nyumba yake) na kuswali ndani yake. Baadhi ya watu wakaja na kujiunga naye katika swala hiyo. Kisha tena usiku uliofuata walikwenda kwa ajili ya swala, lakini Mtume (s) akachelewa na hakutoka nje kwa ajili yao. Basi walipandisha sauti zao na kugonga mlango kwa mawe madogo (kwa kuteka mawazo yake). **Mtume (saww) akatoka nje akiwa katika hali ya hasira,** wakasema, "Wewe bado unasisitiza (juu ya tendo lako) kwamba unahofia swala hii inaweza kuwa wajibu juu yetu. Kwa hiyo, Enyi watu! Tekelezeni swala hii katika nyumba zenu, **swala bora ya mtu ni ile anayoiswalia nyumbani kwake, isipokuwa swala ya lazima (jamaa). "**

[*Sahih al-Bukhari,* juzuu ya 8, kitabu cha 73, namba134

“*Na waambie waumini wanaume wainamishe katika macho yao na wazilinde tupu zao. Hilo ni usafi zaidi kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za wanayoyafanya. Na waambie waumini wanawake wainamishe katika macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao, isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasidhihirishe uzuri wao ila kwawaume zao, au baba zao, aubaba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au ndugu zao, au watoto wa kaka zao, au watoto wa dada zao, au iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio, au watoto wadogo ambao hawajajua uchi wa wanawake. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane mapambo waliyoyaficha. Na tubieni kwa Mwenyezi Mungu nyote enyi waumini ili mpate kufanikiwa.….*”

(Qur'an: Suura 24, Aya 30-31)

# Kwa nini Waislamu wana utaratibu Maalum wa Mavazi?

Uislamu haukuwakataza wanawake na wanaume kushirikiana kiutendaji, lakini umewaamrisha kufuata kanuni, tabia na sifa zakutokujiona ili waweze kumlea mtu mwingine kwa heshima kamili na sahihi. Tabia ya Kiislamu ya kawaida ina unyoofu na kuheshimiana, kama vile hali ya mavazi mara nyingi hutambuliwa kutokana na mitandio ambayo huvaliwa na wanawake wa Kiislamu

“Katika jamii ya kisasa ya leo, mwanamke daima amekuwa anaonekana kama kitu tu kingine cha kijinsia kwa wanaume. Kwa nini mtu kuonyesha uzuri wa mtu mwingine kwa macho yasiyohitajika kwa kujifurahisha? Hijab hulinda heshima ya mwanamke na hana shauku ya kumfanya yasiyohitajika kutoka jinsia tofauti. Najisikia kama wanawake wote watakuwa tayari kuvaa vazi la Kiislamu lilopitishwa na kanuni za Uislamu, kiwango cha matukio ya uchokozi, ubakaji, kunajisi, na kadhalika utakuwa kidogo. Kuvaa hijab kunanisababishia kujiamini zaidi mwenyewe kama mwanamke na haiwezi kunizuia kwa njia yoyote katika taaluma yangu ". Bi Salva I Rasool, Graphic Designer

“Mimi nimeukubali Uislamu na hivyo siwezi kulinganisha na uzoefu wa maisha na bila mavazi ya Kiislamu. Ni vizuri kufahamu tabia katika jamii ya Magharibi kuwa hijab ni kandamizi au inazuia uhuru wa mwanamke. Uzoefu wangu wa hijab na mafunzo yangu ya Kiislamu yananiruhusu mimi kuelewa kwamba hili sio tatizo. Watu wasio Waislamu wakati mwingine hukodoa macho, lakini katika hijab Mimi siku zote ninaheshima. Sijawahi kupata shida au kudumisha kazi, Muda mrefu sijakutana na yasiyohitajika au maoni machafu kutoka jinsia tofauti, Nikivaa hijab huhisi heshima zaidi kuliko kukaa bila ya hijab. Sasa natambua naweza kukubalika na kushirikiana na wengine kama nafsi yangu ya kweli, mara moja muonekano wangu hauruhusiwi kuwa sababu ya kidhibiti. Hata katika vitongoji vibaya, watu wachafu kawaida hutembea mbali na mimi. Dhana ya jumla katika mavazi ya Kiislamu ni kudumisha heshima halisi na uzoefu wangu ni kwamba hakika hijab huongeza heshima na maingiliano mazuri inajenga ongezeko la usalama wakati ninapotoka nje katika umma. Kujua kwamba hijab inaniogezea, kamwe sitorudi nyuma kwenye maisha bila hijab. Nakwenda nje hadharani kama mwanamke wa kiislamu anayetambuliwa - najikumbusha mwenyewe na wote wanaoniona kwa yale ninayoomba kwa ajili ya kuishi katika hali ambayo ni nzuri na safi. Mimi ni miongoni mwa wale ambao huomba kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu katika mambo yote. Watu wanajua hili ni vazi la watawa wakati wakiliona, na wanajua hivyo hata kwangu mimi. Hata kama hawawezi kuelewa sababu kwa ajili ya mtindo wa mavazi yangu, na kwamba sioyakawaida hapa nchini Marekani, hueleza Pongezi kwa mtu ambaye hana hofu ya kuishi kwa kanuni zake ". Bi Diana Beatty, Mwalimu

“Niligundua napenda kuvaa hijab. Kweli, 'kupenda' sio neno sahihi, kwa sababu sio chanya zaidi. Napenda hijab. Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu kama mwanamke wa Marekani, nilihisi kuwa mwili wangu hatimaye ni wa kwangu. Nilihisi kana kwamba hatimaye mwishowe naweza kuelezea vipi kukosa maneno bora zaidi, kama uadilifu wa mwili wangu mwenyewe wa ndani. Niligundua kwamba nimetendewa vizuri sana, kwa heshima sana, na nilibainisha wazi juu ya tabia ya sehemu ya wanaume isiokoma, hasa vijana, kuniacha peke yangu na kupata mapunziko ya kutosha. Njia hii imejidhihirisha yenyewe kwa nguvu zaidi ilikuwa kiwango ambacho nimeona sifuatwi tena na macho ya wanaume.Hjab hunipa ujumbe, hata hivyo kiasi 'hazipatikani,' ingawa nadhani kwamba ni sehemu yake, lakini kitu chenye nguvu ... "ni makafiri wa Marekani mshiriki katika mitandio baada ya Septemba 11 kwa ajili ya Kampeni ya Mshikamano, kama alinukuliwa katika barua kwa Mambo ya nyakati ya San Francisco, Mei 9, 2002

**Kwa maelezo zaidi kuhusu Uislamu, tembelea:**

*http://al-islam.org/faq/*

## Inamisha Macho Yako kwa Ubora wa Nafsi Yako

Falsafa ya umashuhuri wa kujulikana hijab – Ni vazi la kawaida laKiislamu - ni dhana iliyojikita kwenye kulinda mawazo ya mtu na kitu ambacho kinaweza kupunguza hatia ya mtu. Imam 'Ali, binamu na mwana-mkwe wa Mtume wa Uislamu (amani iwe juu yake na familia yake), alisema,

*"Jicho ni kupeleleza ya mioyo na mjumbe wa akili, kwa hiyo inamisha macho yako kutokana na chochote kicho sahihi kwa imani yako ..."*

Taa ya Njia

Katika dunia ya kisasa, hisia zetu ni bombarded kutoka pande zote na wingi uliokitiri wa kuona, sauti, na harufu. Uislamu unatufundisha kudhibiti hisia zetu na yale ambayo hujidhihirisha wazi kwa sababu uzoefu wetu huonesha yanatuathiri nje pamoja na kiroho. Harufu ya marashi inaweza kukumbusha mbali na ukakumbuka bibi ya mtu fulani; sauti ya fataki inaweza kukuogofya na kuzaa mfano wa vita, kuona mwanamke mzuri katika mavazi ya kuvutia inaweza kuleta hisia za mvuto zisizohitajika na zahovyo.

Wakati akili inaposhuhudia ukatili, uhalifu, au ufisadi, hata kama sio sisi wenye hatia ya kufanya kosa, tunapoteza kiwango cha kutokuwa na hatia. Wote tunakubali kumbukumbu ya utoto ya muda iwapo tungerejea kupitia hasara ya kutokuwa na hatia hiyo. Ni kipi ambacho kimekushtua mara moja au kilichofanyika katika hali maalum
huanguka katika ulimwengu wa kawaida.

Katika Uislamu, sio tu kwa ajili ya wazazi kuwa makini kulinda watoto wao kutokana na wanayofanya wazi wazi, lakini ni kwa watu wazima pia wajilinde wenyewe. Kushindwa kufanya hivyo hatimaye kunaweza kusababisha maradhi ya kiroho.

Hivyo basi, falsafa kubwa iliyoko nyuma ya hijab ni kudumisha utu, usafi na heshima na kuitumia kwa pande zote za maisha na si mavazi pekee. Ni lazima kujizuia wenyewe kutokana na kuangalia jinsia tofauti katika njia mbaya, na ni lazima tuvae mavazi ya heshima ili kwamba sisi tuonekana kwa heshima.

## Maadhimisho sahihi ya Hijab

Qur'an imeelekeza mavazi ya Kiislamu ya kawaida kama ifuatavyo:

"***Na waambie waumini wanaume wainamishe katika macho yao na wazilinde tupu zao. Hilo ni usafi zaidi kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za wanayoyafanya. Na waambie waumini wanawake wainamishe katika macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao, isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasidhihirishe uzuri wao ila kwawaume zao, au baba zao, aubaba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au ndugu zao, au watoto wa kaka zao, au watoto wa dada zao, au iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio, au watoto wadogo ambao hawajajua uchi wa wanawake. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane mapambo waliyoyaficha. Na tubieni kwa Mwenyezi Mungu nyote enyi waumini ili mpate kufanikiwa.***…."(Qur'an: Suura 24, Aya 30-31

Lengo la staha hii ni kudumisha utu wa wanaume na wanawake wakati wanapo shirikiana au kuingiliana katika shughuli zao.

 Kwanza, watu wanatakiwa kuongoza katika kuheshimu wanawake. Wanapaswa kutokushiriki katika au kukubaliana na shughuli yoyote ambayo hailazimu au kuhitaji mwanamke. Wao pia wanatakiwa kuinamisha macho yao chini kwa unyenyekevu na kwa kuzingatia falsafa ya jumla ya staha ya moyo na mavazi. Ni lazima kuvaa mavazi ya heshima na kuepuka shughuli katika maeneo ambayo yatasababisha kushuhudia yale ambayo hawapaswi kuyashuhudia.

 *Hijab* haizuii wanaume na wanawake kutoka katika kushirikiana kwa lengo la masomo, kazi, kufanya matendo mema, na kadhalika. Badala yake, ikiwa hijab itavaliwa ipasavyo, maingiliano hayo yatafanyika katika usafi wa lilokusudiwa na bila ya matumizi mabaya.

 Wanawake wanapaswa kujiheshimu wenyewe kama viumbe wa heshima na kushirikiana na watu katika usafi. Wanapaswa kurekebisha tabia zao karibu na watu wengine ili kutoonekana kuvutia kuvutia au kupendeza na hivyo kuruhusu wenyewe kutokuwa na vipingamizi.

 Iwapo miongoni mwa watu ambao si ndugu wa karibu, wanawake wanapaswa kuvaa mavazi ya kujisitiri ili uzuri wao (chanzo cha uzuri na kivutio) umefunikwa. Wasomi wa Kiislamu kwa kauli moja wamesema hali ya kuwa mwanamke lazima ajiheshimu kufunika mwili wote, isipokuwa vitanga vya mikono yake na uso. Wanawake Waislamu kutimiza mahitaji haya kwa kuvaa nguo pana na inayomtosha na kufunika nywele zao kwa mitandio.

 Mahitaji kwa mavazi ya kawaida hutofautiana kati ya jinsia kutokana na tofauti za kibiolojia na sababu ya msingi ya kivutio. Mtu anaweza kuchunguza tofauti hizi katika jamii ya Magharibi ambapo idadi ndogo ya wanawake husoma magazeti ya picha za ngono au kutembelea makahaba ikilinganishwa na wanaume ambao hushiriki katika shughuli hizo.

 Kinyume na maoni ya baadhi  watu, hijab siyo dalili ya unyonge wa mwanamke wala vilivyowekwa juu yake na jinsia tofauti. Mbele ya Mwenyezi Mungu, wanaume na wanawake wanaweza  kutofautishwa mmoja baada ya mwingine tu katika suala la uchaji wa mtu binafsi. Iwapo tutaangalia mavazi ya kawaida, kabla mtu mmoja baada mwingine, tutawatofautisha kwa sifa zisizo za kimwili kama vile akili na uadilifu.

 Mavazi ya Kiislamu ya kawaida kijamii hayawakoseshi hewa wanawake na kuwanyima uhuru na harakati muhimu, kujieleza na kutoa maoni, elimu, huduma ya afya na haki nyingine za binadamu. Badala yake, hijab husaidia katika kujenga sauti ya jamii na kupunguza idadi ya uhalifu kama vile ubakaji na udhalilishaji,  ingawa uwezekano wa kichocheo kwa uhalifu wa aina hii unaweza usiwepo wakati hijab ikizingatiwa. Utunzaji wa hijab ni sehemu ya mfumo mkubwa katika Uislamu na kwamba wakati hijab itavaliwa vizuri na kufuatiwa inaouwezo wa kuinua utu wa wanaume, wanawake, na jamii kwa ujumla.

## Ni Nini Hasa Wanawake wa Kiislamu Wanafikiri Kuhusu Hijab?

"Naweza kuhisi heshima ya ziada kuja njia yangu. Watu hunichukulia mimi kwa umakini zaidi, na mimi nahisi ulinzi na ujasiri wakati nikitoka nje ". Dk Bi NZ Vakil, M.D.

*“Simamisha Swala Jua linapopinduka mpaka giza la usiku, na (kusoma) Qur’an ya Alfajiri. Hakika Qur’an katika Alfajiri ni yenye kushuhudiwa.”*
(Qur'an: Sura: 17, Aya: 78)

# Kwa nini Mashia wanakusanya Swala?

Mashia wanatekeleza Swala tano za kila siku za *wajib*. Hata hivyo aghlabu wao hukusanya ya *Dhuhr* na ya *'Asr* kwa kuziswali kwenye kipindi kilichoelezwa kuwa kinaanzia mwanzo wa *Dhuhr* hadi mwisho wa *'Asr*. Vilevile wanaonelea kuwa inajuzu vivyo hivyo kukusanya Swala za *Maghrib* na *'Isha*. Kufanya hivi ni kwa uthibitisho kamili wa Qur'an na Hadith sahih za Mtume (s.a.w.w.).

### *Hata kama imeruhusiwa, kwa nini kufanya hivyo?*

Hakuna anayesema kuwa kuna ubaya kuziswali Swala bila ya kuzikusanya. Swala za *Dhuhr* na *`Asr*, pia *Maghrib* na *'Isha'* zinaweza kuswaliwa, aidha, kwa kukusanywa au kwa kutenganishwa. Hata hivyo, kukusanya Swala mbili kulikofanywa na Mtume (s.a.w.w.) kunaonyesha huruma ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ya kuwarahisishia *ummah*, na ziko sababu kwa nini imekuwa ni ada miongoni mwa Mashia, nazo ni:

- Watu mara nyingi wana shughuli na majukumu yao mengi, hususan katika nchi ambazo utaratibu wa nchi hizo wa kielimu na kikazi haukidhi mahitaji ya Waislamu ya kuweza kuswali Swala zao tano za kila siku. Baadhi ya kazi hufanywa kwa masaa mengi mfululizo, bila ya kuingiliwa. Kwa hivyo, ni vizuri, na ili kujiepusha na kukosa Swala ya pili, Shia huziswali mbili katika kipindi kimoja, iwe ni mapema au baadaye katika wakati wanaouchagua.

- Ni pale watu wanapokutana kutoka mbali ili kuswali mojawapo ya Swala hizo mbili; na kwa kuwa imeruhusiwa kukusanya zote mbili, wao huziswali zote mbili kwa jamaa, moja baada ya nyingine. Kwa njia hii wanakuwa wametekeleza yote, wajib na kuswali kwa jamaa *(jama'ah)* na hivyo kupata thawabu zaidi. Hebu mathalan angalia mfano wa Swala ya Ijumaa. Tumeona kwamba maelfu ya ndugu zetu wa kisunni huswali Swala za Ijumaa kwa wakati wake kabisa, lakini wengi wao hawapati kuswali Swala ya *`Asr*, wacha kuswali kwa jamaa. Kwa upande mwingine Mwislamu Mshia anayeswali Swala ya Ijumaa, ataweza kuiswali Swala ya *`Asr* kwa *jama'ah*.

- Kwa sababu *sunnah* hii haitekelezwi na ndugu zetu wa kisunni, ndio ikawa ni sababu nyingine ya Mashia kuhisi kwamba ni vyema waihuishe. Tungelipenda kuona watoto wetu na Waislamu wawe wanajua kwamba kukusanya Swala za *Dhuhr* na *`Asr*, pia *Maghrib* and *'Isha'* kunaruhusiwa, na hivyo ni kunatokana na *sunnah* za Mtume (s.a.w.w.).

### Hitimisho:

Kukusanya Swala za *Dhuhr* na *`Asr*, na kukusanya za *Maghrib* na *'Isha'*, kunajuzu kulingana na Qur'an na *sunnah* za Mtume Muhammad (s.a.w.w.), isitoshe kwafaa zaidi. Kutotekelezwa na ndugu zetu wa Sunni kwa *Sunnah* hii yenye ushahidi wa kutosha, hakuifanyi kwamba iwe haifai katika maisha yetu, kama Mwanachuoni mashuhuri mfafanuzi wa *Sahih Muslim*, Sheikh An-Nawawi alivyoandika:

*Pindi Sunnah inapothibitishwa kuwa ni sahih, basi haiwezi kuachwa kwa sababu tu watu wengi hawaifanyi.*
[an-Nawawi, *Sharh Sahih Muslim*, (Beirut, 1392 A.H.), Juz. 8, Uk. 56]

**Kwa maelezo zaidi juu ya Uislamu sahih, Angalia Tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

Madhehebu ya Sunni ki-fiqh – sipokuwa ya Hanafi– yanaruhusu kukusanya Swala za *wajib (al-jam` bayn al-swalatayn)* kama kutakuwa na sababu ya mvua, safari, hofu, au dharura zozote. Lakini madhehebu ya Hanafi hayaruhusu kukusanya Swala za kila siku za *wajib* wakati wowote ule, isipokuwa Swala za *Al-Muzdalifa* wakati wa kuhiji. Ama madhehebu ya Maliki, Shafi'i, na Hanbali, wote wanakubaliana kujuzu kukusanya Swala pindi pale mtu anaposafiri, lakini wametofautiana kuhusu sababu zingine. Na madhehebu ya Shia Ja'fariyya yanasema kwamba mtu anaweza kukusanya Swala tano bila ya sababu yoyote.

## Nyakati za Swala kulingana na Qur'an

Imam Fakhr al-Din al-Razi, mwanachuoni, mfasiri mashuhuri wa Qur'an wa Sunni, ameandika haya kuhusu Aya zilizonukuliwa (Sura 17, Aya 78):

- "Ikiwa kama tutafasiri giza (*ghasaq*) kwa maana ya pale giza linapoanza kuingia, basi neno *ghasaq* litakuwa na maana ya mwanzo wa *Maghrib*. Kwa msingi huu, nyakati tatu zimetajwa katika Aya hiyo: 'wakati wa mchana, wakati inapoanza kuingia *Maghrib* na wakati wa of *Fajr*'. Hii itakuwa kwamba mchana, ni wakati wa *Dhuhr* na *`Asr*, nyakati hizi huchanganywa kwa Swala hizi mbili (*Dhuhri* na *Asr*). Wakati inapoingia *Maghrib* ndio wakati wa *Maghrib* na *'Isha'* kwa hivyo nyakati hizi pia huchanganywa kwa Swala hizi mbili. Hii inaruhusu kukusanya Swala ya *Dhuhri* na *Asr*. Na *Maghrib* and *'Isha'* wakati wote. Hata hivyo, kuna ushahidi kwamba kukusanya wakati uko nyumbani bila ya udhuru wowote hakuruhusiwi. Hii yaashiria mtazamo kwamba kukusanya kunaruhusiwa wakati wa safari au kama kuna mvua, n.k.."
  [Fakhr al-Din al-Razi, *al-Tafsir al-Kabir*, Juz. 5, Uk. 428]

Tutaonyesha kwa kifupi ushahidi usiopingika kwamba kukusanya Swala bila ya dharura yoyote kunajuzu. Hata hivyo ni wazi kwamba *nyakati* za Swala za wajib ni tatu pekee: 1) Wakati wa Swala mbili za faradhi, *Dhuhr na `Asr*, ambao unashirikishwa pamoja kwa mbili hizo. 2) Wakati wa Swala mbili za faradhi, *Maghrib* (jioni) na *'Isha'* (usiku) ambao pia unashirikishwa pamoja kwa mbili hizo. 3) Wakati wa Swala ya *Fajr* (mapema alfajiri) ambao ni maalum pekee kwa hiyo.

## Je Mtume (s.a.w.w.) alikusanya Swala?

- Amepokea Ibn 'Abbas kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (amani imshukie) aliswali Madina (rak'ah) saba na (rak'ah) nane, yaani (zimekusanywa) Swala za mchana (*Dhuhr*) na alasiri (*`Asr*) (rak'ah) nane; na Swala za jioni (*Maghrib*) na usiku (*'Isha'*) (rak'ah) saba.
  [*Sahih al-Bukhari* (Tafsiri ya kiingereza), Juz. 1, Kitabu cha.10, Namba 537; *Sahih Muslim* (Tafsiri ya kiingereza), *Kitab al-Salat*, Kitabu 4, Sura 100 *Combination of prayers when one is resident*, Hadith Na. 1522]

- 'Amepokea Abdullah b. Shaqiq: Siku moja Ibn 'Abbas alituhutubia mchana (baada ya Swala ya mchana) mpaka jua likachwa na nyota zikaangaza, watu wakaanza kusema: Swala! Swala! Akaja bwana mmoja kutoka ukoo wa Banu Tamim akiwa ameshikilia kusema bila ya kugeuka: Swala! Swala! Ibn 'Abbas akakemea: "Mwana wa kukoswa na mamaye we! Wanifundisha mimi Sunna?" Kisha akasema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akikusanya Swala za *Dhuhr* na *`Asr* pia Swala za *Maghrib* na *'Isha'* ." 'Abdullah b. Shaqiq amesema: "Nilikuwa na shaka kidogo akilini mwangu kuhusu jambo hilo, kwa hivyo nilikwenda kwa Abu Huraira na kumuuliza juu ya jambo hilo, naye alitoa ushahidi wa maelezo yake."
  [Sahih Muslim (Tafsiri ya kiingereza), *Kitab al-Salat*, Kitabu cha 4, Sura 100 *Combination of prayers when one is resident*, Hadith Na. 1523, 1524]

## *Lakini hiyo haikuwa kwa ajili ya safari, hofu, au mvua?*

Hadith nyingi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) zaonyesha waziwazi kwamba yeye alikuwa akikusanya Swala *bila* ya udhuru wowote maalum.

- Mtume (s.a.w.w.) aliswali akiwa mjini Madina, ***bila ya kuwa safarini***, saba na nane (hii yaashiria Rakaa saba za *Maghrib* na *'Isha'* zikiwa zimekusanywa, pia Rakaa nane za *Dhuhr* na *`Asr* zikiwa zimekusanywa).
  [Ahmad ibn Hanbal, *al-Musnad*, Juz. 1, Uk. 221]

- Mtume (s.a.w.w.) aliswali *Dhuhr* na *`Asr* kwa kuzikusanya, pia *Maghrib* na *'Isha'* kwa kuzikusanya ***pasi na kuwa na sababu ya hofu au safari.***
  [Malik ibn Anas, *al-Muwatta'*, Juz 1, Uk. 161]

Kwa hakika hata twaambiwa na baadhi ya Hadith nini sababu ya Mtume (s.a.w.w.) kufanya hivyo. **IIlikuwa ni kuwarahisisishia ummah!**

- Ibn 'Abbas ameeleza kwa Mtume (s.a.w.w.) alichanganya Swala ya mchana na ya alasiri, pia ya *Magharibi* na ya *'Isha'* akiwa Madina, ***bila ya kuwa katika hali ya hofu au mvua***. Na katika Hadith iliyopokewa na Waki' (maneno yake ni): "Nilimwambia Ibn 'Abbas: Ni nini kilichomfanya yeye kufanya hivyo? Akasema: **Ili umma huu (wa Mtume) usifanyiwe mambo kuwa mazito."**
  [*Sahih Muslim* (Tasiri ya kiingereza), *Kitab al-Salat*, Kitabu cha 4, Sura 100 *Combination of prayers when one is resident*, Hadith Na. 1520; *Sunan al-Tirmidhi*, Juz 1, Uk. 26]

- Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliswali Swala za mchana na za alasiri pamoja akiwa Madina ***bila ya kuwa katika hali ya hofu au katika hali ya kusafiri***. Abu Zubair amesema: "Nilimuuliza Sa'id (mmoja kati ya wapokezi) kwa nini yeye alifanya hivyo. Naye alisema: Nilimuuliza Ibn 'Abbas kama ulivyoniuliza wewe, naye alinijibu kwamba **yeye (Mtume mtukufu) hakutaka mtu yeyote katika umma wake atiwe katika uzito.**"

[*Sahih Muslim*, Tafsiri ya kiingereza, *Kitab al-Salat*, Kitabu cha 4, Sura 100 *Combination of prayers when one is resident*, hadith no. 1516]

*"…na mtakapopata amani (mkawa katika salama, hakuna vita) basi simamisheni Swala (kama kawaida). Kwa hakika Swala kwa Wanaoamini ni faradhi iliyowekewa nyakati maalum."*

(Qur'an: Sura 4, Aya 103)

# Jinsi ya kuswali Swala za kila siku

Ni wajibu kuswali Swala tano zifuatazo kila siku kwa nyakati zilizowekwa:

- *Salat al-Fajr* (Swala ya **Alfajiri**), ambayo ina rakaa mbili
- *Salat al-Dhuhr* (Swala ya **Mchana**) yenye rakaa nne
- *Salat al-`Asr* (Swala ya **Alasiri**) ambayo ina rakaa nne
- *Salat al-Maghrib* (Swala ya **Magharibi**) yenye rakaa tatu
- *Salat al-`Isha* ( Swala **ya Usiku**) yenye rakaa nne.

Kuswali Swala tano za kila siku kulingana na madhehebu ya Shia Ja'fariyya ni kuswali kulingana na utaratibu (*tartib*) na kuzifuatanisha, pasi na kuchelewa kati yazo (*muwalat)*. Mwenye kuswali anahitajika kwanza ajitoharishe ( kwa *ghusl*, ikibidi, au kwa *wudhu*) na anahitajika kufanya mengine ya msingi yanayohitajika kabla ya Swala.

**Tashahhud** : Baaa ya sijda ya pili ukae na usome:

| | |
|---|---|
| **Ash- hadu al laa ilaaha illallaahu wahdahu laa shariika lah,**<br>**wa ash- hadu anna Muhammadan `abduhu wa rasuluh**<br>**Allaahumma swalli `alaa Muhammadin wa Aali Muhammad** | *Nashuhudia kwa hapana Mola ila Allah, aliye wa pekee asiye na mshirika.*<br>*Na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja na mtume wake.*<br>*Ewe Mola, mtakie rehma Muhammad na Aali zake.* |

Ikiwa unaswali Swala ya *Al-Fajr* (Alfajiri), wacha mengine na uende kwenye maelezo ya sehemu ya **Mwisho.**

Ikiwa unaswali Swala ya *Dhuhr* (Adhuhuri), ya*`Asr* (Alasiri), ya *Maghrib* (Magharibi), au ya*`Isha* (Usiku), endelea kwa kusimama kwa rakaa ya tatu huku ukisoma ***Bihawlillahi…***kama ilivyoelezwa kwenye mwisho wa sehemu ya ***Rakaa ya kwanza***.

*Rakaa ya tatu*

**At-Tasbihat ul-Arba`ah (Tasbihi nne)** : baada ya kuinuka na kusimama wima, hapo, aidha utasoma *Surat al-Fatiha*, au utasoma *al-Tasbihat ul-Arba`ah* mara tatu, kama ifuatavyo:

**Subhaanallaahi wa'l hamdu lillaahi wa laa ilaaha illallaahu wallaahu akbar**

*Utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu, Shukrani zote ni za Mwenyezi mungu; hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Allah, naya ni Mkuu.*

Utarukuu, simama kwa muda mfupi, kisha utasujudu. Hii ni kama ilivyoelezwa katika sehemu ya maelezo ya ***Rakaa ya kwanza***. Ikiwa unaswali Swala ya *Maghrib* (Magharibi), utasoma *Tashahhud* baadaye. Kasha wacha mengine na uende kwenye maelezo ya sehemu ya **Mwisho.**

Ukiwa unaswali Swala ya *Dhuhri* (Adhuhuri), ya*`Asr* (Alasiri), au ya *`Isha* (Isha), utaendelea kwa kusimama kwa rakaa ya nne huku ukisoma ***Bihawlillahi….*** kama ilivyoelezwa katika mwisho wa sehemu ya maelezo ya ***Rakaa ya kwanza***.

## *Rakaa ya nne*

Hii ni kama rakaa ya tatu. Baada ya kusujudu endelea na kukaa, na usome *Tashahhud.*

*Mwisho*

Baada ya kusoma *Tashahhud* ya Rakaa ya mwisho, soma **Taslim** *(Salaam)* ambayo itakamilisha Swala yako, nayo ni:

| | |
|---|---|
| **Assalaamu `alayka ayyuhan nabiyyu wa rahmatullaahi wa barakaatuh**<br>**Assalamu `alaynaa wa `alaa `ibaadillaahis swaalihiin**<br>**Assalamu `alaykum wa rahmatullaahi wa barakaatuh** | *Amani iwe juu yako ewe Nabii na pia ziwe juu yako rehma za Allah na baraka zake.*<br>*Amani iwe juu yetu na juuya waja wako wema.*<br>*Amani iwe juu yenu (nyote) na pia rehma na baraka za Allah ziwashukie.* |

Kisha baadaye (ukipenda) soma *Takbir* mara tatu.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu ibada na mamabo ya kiroho ya Swala za kila siku, Tazama tovuti hii:**

***http://al-islam.org/faq/***

*v1.0*


## Matayarisho

Simama wima ukielekea *Qiblah* (kuelekea Makka) kisha uadhini (*adhan)* na usome *iqama*. Na fahamu ya kwamba visomo vyote utavyosoma wakati wa Swala viwe ni kwa lugha ya kiarabu. Japokuwa namna ya kutamka imeelezwa hapo chini kwa kila kisomo, ni vizuri kujaribu kusoma maandishi na matamshi ya kiarabu.

**Niyya** : Tia nia kwa maneno haya akilini mwako: **"Naswali Swala hii ____** (taja Swala unayoiswali), **yenye rakaa ____** (taja ni rakaa ngapi) **kwa kutaka ukaribu wa Mwenyezi Mungu."**

## *Rakaa* ya kwanza

**Takbiratul Ihram** : Inua mikono yote miwili juu kufikia masikioni na useme:



**Allaahu akbar**

*Mungu ni mkuu*

Neno hili, la **Takbir**, litarudiwa mara kwa mara wakati wa Swala.

**Qiyam** : Uendelee kusimama wima wakati utaposoma kwenye hatua nyingine ya *Qira'ah*.

**Qira'ah** : Mwanzo, soma Sura ya kwanza katika Qu'an tukufu, *Surat al-Fatiha*

| | |
|---|---|
| **Bismillaahi'r-Rahmaani'r-Rahiim** | *Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu* |
| **Al-hamdu lillaahi rabbil-`aalamiin** | *Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.* |
| **Arrahmaanir rahiim** | *Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu* |
| **Maaliki yawmid-diin** | *Mwenye mamlaka siku ya malipo;* |
| **Iyyaaka na`budu wa iyyaaka nasta`iin** | *Ni wewe tu ndiye tunayekuabudu na ni wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.* |
| **Ihdinas-swiraatwal-mustaqiim** <br> **swiraat al-ladhiina an`amta `alayhim** <br> **ghayril maghdhuubi `alayhim** <br> **wa la'dhwaal-lliin** | *Tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale uliowaneemah, sio ya wale uliowakasirikia, wala waliopotea.* |

Kisha, soma Sura kamili nyingine ya Qur'an tukufu (hapa tumechagua Sura fupi, Sura ya 112, *Surat al-Ikhlas*).

| | |
|---|---|
| **Bismillaahi'r-Rahmaani'r-Rahiim** | *Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu* |
| **Qul huwallwaahu ahad** | *Sema: Yeye ni Allah mmoja,* |
| **Allwaahus swamad** | *Allah anayekusudiwa na waja (kwa kumuomba na kumtegemea),* |
| **Lam yalid walam yuulad** <br> **Wa lam yakullahu kufuwan ahad.** | *Hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hana anayefanana naye hata mmoja.* |

**Rukuu** : Baada ya kumaliza kusoma Sura hii ya pili, anayeswali atasema *Takbir* (Tazama juu) kisha atainama hadi mikono yake aiweke kwenye magoti yake. Atasoma utajo huu *dhikr* mara moja akiwa amerukuu, atasema:



**Subhaana rabbiy al-`adhiimi wa bihamdih**

*Utakatifu wote ni wa Mola wangu mkuu, na shukrani zote ni zake.*

Endelea ukiwa umesimama useme:

**Sami`allaahu liman hamidah**

*Mwenyezi Mungu humsikia anayemhimidi*

Sema *Takbir*, kisha utasujudu (*sujud*)

**Sujud** yaani ni mtu kuweka paji lake la uso chini kwa njia maalum kwa nia ya kumnyenyekea Mwenyezi Mungu.



Wakati ukifanya *sujud*, ni wajib viganja vyote vya mikono, magoti na vidole gumba vya miguu vyote viwe viko chini (ardhini). Na *dhikr* ifuatayo itasomwa mara moja wakati ukiwa umesujudu:

**Subhaana rabbiy al-a`laa wa bihamdih**

*Utakatifu ni wa Mola wangu aliye mtukufu na shukrani ni zake.*



Na baada ya sijda ya kwanza, utainua paji lako la uso ukae katika hali ya kifundo cha mguu wa kulia kiwe juu ya nyayo ya mguu wa kushoto, huku mikono yako ikiwa juu ya mapaja na useme *Takbir*, kisha useme (ukipenda):

**Astaghfirullaaha rabbii wa atuubu ilayh**

*Namuomba msamaha Mola wangu na natubu kwake.*

kisha usome *Takbir* tena. Utarudia kusujudu tena, kisha utakaa na useme *Takbir*.

Kaa kwa muda, kisha uinuke huku ukisema (ukipenda):

**Bihawlillaahi wa quwwatihi aquumu wa aq`ud**

*Nasimama na nakaa kwa uwezo na kwa nguvu za Allah.*

## *Rakaa ya pili*

Ukishainuka na kunyooka sawasawa, soma *Surat al-Fatiha* na Sura nyingine ya Qur'an tukufu kama ilivyokuwa katika rakaa ya kwanza. Kisha useme *Takbir*, na kisha utasoma *Qunut.*

**Qunut** : Inua mikono yako mbele ya uso wako, viganja vyako vielekee juu, huku ukiwa umeishikamanisha mikono yote miwili na vidole pamoja. Na usome dua ifuatayo:



**Rabbanaa aatinaa fi'd-dun-yaa hasanatan wa fi'l-aakhirati hasanatan wa qinaa `adhaab an-naar**

*Ee Mola wetu! Tupe mema duniani, na utupe mema Akhera, na utukinge na adhabu ya moto*

[Qur'an, Sura 2, Aya 201]

[Taz.: *Qunut* si lazima, ila ukipenda utasoma]

Kisha sema *Takbir*, kisha urukuu, kisha usujudu sijda mbili, kama ilivyoelezwa katika rakaa ya kwanza.

*Basi mtukuze Mola wako pamoja na kumsifu, na uwe ni miongoni mwa wanaosujudu.*
(Qur'an 15:98)

# Kwa nini Mashia wanasujudu juu ya *Turbah*?

Waislamu wa madhehebu ya Shia wanapendelea kusujudu juu ya vijiwe vidogo vya udongo, viitwavyo Turbah, ambavyo kwa kawaida hutengenezwa kutokana na udongo wa ardhi ya Karbala iliyoko Iraq.

## Kwa nini ni lazima kusujudu juu ya udongo wa kutoka Karbala?

**Hapana si lazima!** Bali Mashia *wanapendelea* kusujudu juu ya mchanga uliotoka mji wa Karbala kwa sababu ya umuhimu wake uliopewa na Mtume (s.a.w.w.) na Maimam kutoka kwenye kizazi chake (*Ahl al-Bayt*). Na baada ya kuuwawa shahid kwa Imam Husein (a.s.), mwanawe Imam Zayn al-'Abidin (a.s.) aliuteka mchanga wa hapo kidogo na akautangaza kwamba huo ni mchanga mtukufu na akauhifadhi kwenye mkoba. Na Maimam (a.s.) walikuwa waki sujudu juu ya udongo huo wa Karbala na wakiutengenezea *tasbih*, kwa kumtakasa Mwenyezi Mungu kwayo.
[Ibn Shahrashub, *al-Manaqib*, Juz. 2, Uk. 251]

Vilevile waliwahimiza Mashia kusujudu juu ya udongo huo, kwa kuelewa kwamba si wajib, bali kwa mtazamo wa kupata thawabu zaidi. Maimam (a.s.) wamesisitiza kwamba kumsujudia Mwenyezi Mungu ni lazima kufanywe juu ya ardhi tohara tu, na hivyo wakapendelea kufanywe juu ya udongo wa Karbala.
[al-Tusi, *Misbah al-Mutahajjad*, Uk. 511]
[al-Saduq, *Man la yahduruhu'l faqih*, Juz. 1, Uk. 174]

Mashia, kwa muda mrefu wameuhifadhi udongo huu. Na kwa kuchelea usije ukavunjiwa heshima, ndipo wakautengeneza vipande vidogo vidogo vinavyoitwa *Muhr* au *Turbah*. Wakati wa Swala, tunasujudu juu ya udongo huo, lakini si kwa kuwa ni wajib, bali ni kwa mtazamo wa kuwa huo ni umbile maalum. Vinginevyo, tunapokuwa hatuna udongo tohara, tunasujudu kwenye ardhi liyo tohara, au juu ya kitu kinachotokana nayo.

Kwa kweli ni jambo la kusikitisha kwamba baadhi ya watu - kwa nia mbaya - husisitiza kwamba Shia wanaabudu mawe, au wanamuabudu Husein (a.s.). lakini ukweli ni kwamba sisi tunamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake kwa kusujudu ***juu*** ya Turbah, na sio ***kuisujudia***. Na kamwe hatumuabudu Imam Husein, Imam Ali, au Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Tunamuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na ni kulingana na amri yake huwa tunasujudu juu ya ardhi tohara tu.

## Hitimisho:

Hii ndio sababu ya Waislamu wa madhehebu ya Shia huchukua vijiwe vidogo, ambavyo kwa kawaida hutengenezwa kutokana na udongo wa Karbala, uaowawezesha kusujudu juu ya vijiwe hivi vinavyopendelewa, vilevile hufuata *sunnah* za Mtume (s.a.w.w.).

**To find out more about authentic Islam, visit:**
***http://al-islam.org/faq/***

Kulingana na fiqh ya madhehebu ya Shi'ah Ja'fari - ambayo ni moja miongoni mwa madhehebu tano za kiislamu - Sijda ni lazima ifanywe juu ya ardhi iliyo tohara au kinachoota juu yake, kwa sharti kwamba kisiwe ni kitu kinacholiwa au kuvaliwa. Hii - kufaa kusujudu juu yake - ikiwa ni pamoja na vumbi, jiwe, mchanga na nyasi, kwa sharti kwamba visiwe ni madini. Inaruhusiwa kusujudu juu ya karatasi, kwa sababu imetengenezwa kutokana na kinachomea ardhini, lakini haifai juu ya nguo au zulia.

Wanavyuoni wa madhehebu yote ya Sunni wanakubaliana na kujuzu kwa kusujudu juu ya ardhi na kinachoota juu yake.

## Je Mtume na Maswahaba wake walifanya hivi?

Kuswali juu ya ardhi kulikuwa kukifanywa na Mtume (s.a.w.w.) na waliokuwa karibu naye.

- Amehadithia Abu Sa'id al-Khudri: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akisujudu juu ya matope na maji, nikaona alama ya matope kwenye paji lake la uso.
  [Al-Bukhari, *Sahih* (Tafsiri ya kiingereza), Juz. 1, Kitabu 12, Na. 798; Juz. 3, Kitabu 33, Na. 244]
- Amehadithia Anas bin Malik: “Tulikuwa tukiswali na Mtume kwenye vuguto la joto kali, na ikiwa mmoja wetu hakuweza kuweka uso wake - kwa kusujudu - juu ya ardhi (kwa ajili ya joto), basi yeye alikuwa akiitandika nguo zake chini na kusujudu juu yazo.
  [Al-Bukhari, *Sahih* (Tafsiri ya kiingereza), Juz. 2, Kitabu 22, Na. 299]

Kulingana na Hadith hii yaonyesha kwamba ilikuwa ni katika mazingira na hali zisizokuwa za kawaida tu ndipo Mtume (s.a.w.w.) na maswahaba wake waliweza kusujudu juu ya nguo.

Mtume (s.a.w.w.) pia alikuwa akisujudu juu ya ***Khumra*.**

- Amehadithia Maymuna: Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akisujudu juu ya ***Khumra***.
  [Al-Bukhari, *Sahih* (Tafsiri ya kiingereza, Juz. 1, Kitabu 8, Na. 378]
- Kulingana na mwanachuoni mashuhuri wa kisunni, Al-Shawkani: Zaidi ya maswahaba kumi wa Mtume (s.a.w.w.) wametaja Hadith kuhusu yeye kusujudu juu ya ***Khumrah,*** na ameorodhesha marejeo yote ya kisunni yaliyopokea Hadith hii, ikiwa mni pamoja na **Sahih Muslim**, **Sahih al-Tirmidhi**, **Sunan Abu Dawud**, **Sunan al-Nasa'i** na nyinginezo.
  [Al-Shawkani, *Nayl al-Awtar* , Sura ya ‘Kusujudu juu ya Khumrah’, Juz. 2, Uk. 128]

## *Khumrah* ni nini?

- Ni mswala (mkeka) mdogo unaotoshea kuweka uso na mikono pindi mtu anaposujudu wakati wa Swala.
  [Al-Bukhari, *Sahih* (Tafsiri ya kiingereza), Juz. 1, Kitabu 8, Na. 376 (kama ilivyofafanuliwa na mfafanuzi)]

Ibn al-'Athir, mwanachuoni mwingine wa Sunni, ametaja katika kitabu chake *Jami al-'Usul*:

- "*Khumra* ni ile ambayo Mashia wa sasa wanasujudia juu yake wanaposwali."
  [Ibn al-'Athir, *Jami' al-Usul*, (Cairo, 1969), Juz. 5, Uk. 467]
- "*Khumra* ni mswala dogo uliotengezwa kwa nyuzi za mtende au kwa malighafi nyingine…. Ni kama zile wazitumiazo Mashia wanaposujudu."
  [*Talkhis al-Sihah*, Uk. 81]

## Kwa nini udongo wa ardhi ya Karbala?

Sifa maalum za udongo wa mji wa Karbala (nchini Iraq) zinajulikana, na ulikuwa una muhimu maalum wakati wa Mtume (s.a.w.w.) na baadaye:

- Umm Salama amesema: Nilimuona Husein (a.s.) ameketi juu ya paja la babu yake, Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa ameshika kipande cha udongo mwekundu mkononi mwake, huku akikibusu na kulia. Hapo nikamuuliza ule udongo ulikuwa ni udongo gani. Mtume (s.a.w.w.) akajibu: "Malaika Jibril amenipa habari kwamba mwanangu huyu Husein atauwawa huko Iraq. Yeye ameniletea mchanga huu utokao huko kwenye ardhi hiyo. Nalia kwa mateso yatakayompata Husein wangu." Kisha Mtume (s.a.w.w.) akampa udongo ule Umm Salama na akamwambia: "Utakapouona udongo huu umebadilika na kuwa rangi ya damu, hapo utajua kuwa Husein wangu amechinjwa." Umm Salama aliuhifadhi udongo huo kwenye chupa, akawa akiuangalia, mpaka siku moja wakati wa siku ya Ashura, tarehe 10 ya Mwezi wa Muharram, mwaka 61 A.H., aliuona umekuwa na rangi ya damu. Kisha akajua kuwa Husein bin Ali (a.s.) ameuwawa.
  [al-Hakim, *al-Mustadrak*, Juz. 4, Uk. 398]
  [al-Dhahabi, *Siyar a`lam al-nubala'*, Juz. 3, Uk. 194]
  [Ibn Kathir, *al-Bidayah wa'l-nihayah*, Juz. 6, Uk. 230]
  [al-Suyuti, *Khasa'is al-kubra*, Juz. 2, Uk. 450; *Jam` al-Jawami*, Juz. 1, Uk. 26]
  [Ibn Hajar al-Asqalani, *Tahdhib al-tahdhib* , Juz. 2, Uk. 346]

- Ali ibn Abi Talib alipita Karbala baada ya vita vya Siffin. Aliuteka mchanga kido kwa mkoono wake akanung'unika akisema: 'Ah, ah, mahali penye alama hii baadhi ya watu watauwawa, na wataingia Peponi bila hisabu!'

[Ibn Hajar al-Asqalani, *Tahdhib al-tahdhib* , Juz. 2, Uk. 348]

*Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Mitume*
(Qur'an 33:40)

## Wasio Waislamu wanasema nini juu ya…

# Muhammad

MTUME WA UISLAMU
*(Rehma na amani zimshukie juu yake na juu ya kizazichake)*

Ufuatao ni mkusanyiko wa nukuu fupi fupi kutoka kwenye marejeo mbalimbali ya watu mashuhuri wasiokuwa Waislamu mongoni mwa wasomi, waandishi, wanafalsafa, washairi, wanasiasa na wanaharakati wa kimashariki na kimagharibi. Tuwajuavyo, hakuna hata mmoja kati yao aliyewahi kuwa Muislamu. Kwa hivyo, maneno haya yanaonyesha maoni yao binafsi juu ya mitazamo mbalimbali ya maisha ya Mtume (s.a.w.w.).

## Washington Irving

*(1783-1859 )Anayejulikana kama "The first American man of letters":*

- "Alikuwa na tabia tulivu na mwenye nidhamu katika chakula, na akifuata sana utratibu wa kufunga. Hakuvama katika kupenda mavazi ya mapambo, namna wanavyojionyesha wenye mawazo finyu; pia kunyenyekea kwake katika mavazi kuliathiri pia kulionyesha matokeo ya kutopenda kwake kujitofautisha... alikuwa muadilifu katika muamala wake wa kibinafsi. Aliamiliana na watu wote kwa usawa: marafiki na wageni, matajiri na maskini, na wenye nguvu na wanyonge; na alipendwa na watu walala hoi kwa kuwa jinsi alivyokuwa akiwapokea kwa vizuri, na kusikiliza matatizo yao... Ushindi wake wa kijeshi vitani haukumfanya awe na ujuba au kibri, kama ambavyo wengine wangefanya hivyo kwa kuathiriwa na ubinafsi. Alipokuwa katika enzi za utawala wake wenye nguvu, aliendelea kujiweka kinyenyekevu kama alivyokuwa katika siku za shida. Alijiweka mbali na heshima kuu ya uongozi na hakuwa akifurahishwa iwapo ataingia mahali na apewe heshima kuu mno."
  [*Life of Mahomet*, London, 1889, Uk. 192-3, 199]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Annie Besant

*(1847-1933) Mwingereza na kiongozi India.Pia Rais wa chama cha Indian National Congress mnamo mwaka 1917:*

- "Haiwezekani kwa atakayesoma maisha na tabia za Mtume mkuu wa Arabia, akajua vipi alifundisha na vipi aliishi, kuhisi chochote ila atahisi utukufu aliokuwa nao mtume huyo mkuu, mmoja kati ya wajumbe wakuu wa Mungu. Japo nitakayokueleza yatakuwa ni mengi yaliyozoeleka kwa watu wengi, lakini mimi binafsi ninapoyarudia kuyasoma nahisi kuyapenda upya na napata kuhisi heshima kubwa juu ya mwalimu huyo mkuu wa Arabia." [*The Life And Teachings Of Muhammad*, Madras, 1932, Uk. 4]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Edward Gibbon

*(1737-1794) Anayechukuliwa kuwa ndiye mwanahistoria mkuu wa enzi zake.*

- "Alikuwa (Muhammad) na kumbukumbu pana na nzuri, mzaha wake ulikuwa wa kawaida na wa kushirikiana na watu, mwenye mawazo yenye kutia moyo, maamuzi yake yalikuwa ya wazi, ya haraka na ya kukata. Alikuwa na ujasiri wa kufikiri na kutenda."
  [*History of the Decline and Fall of the Roman Empire*, London, 1838, Juz. 5, Uk. 335]

**Kwa maelezo zaidi juu ya Mtume Muhammad (s.a.w.w) na mafunzo yake, tazama Tovuti:**
***http://al-islam.org/faq/***

## Michael H. Hart

*(1932- ) Profesa wa Unajimu ( Astronomy), Fizikia na elimu ya Historia anasema:*

- "Chaguo langu la kumchagua Muhammad kuongoza katika orodha ya kuwa ni kiongozi wa kwanza mwenye uwezo wa uongozi duniani huenda likawashangaza baadhi ya wasomaji na kudadisiwa na wengine, lakini yeye alikuwa ndiye mtu pekee katika historia aliyefanikiwa sana upande wa kidini na kidunia."
  [*The 100: A Ranking Of The Most Influential Persons In History*, New York, 1978, Uk. 33]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## William Montgomery Watt

*(1909- ) Profesa (Emeritus)wa lugha ya kiarabu na masomo ya kiislamu, Chuo kikuu cha Edinburgh:*

- "Kuwa tayari kwake kuteseka kwa ajili ya imani yake, maadili ya hali ya juu ya watu waliomuamini na kumuona kuwa ni kiongozi, na ukuu wa mafanikio yake katika kufikia malengo yake – yote yanaonyesha uaminifu wake wa kimsingi. Kufikiria kuwa Muhammad ni mzushi, hakutatui matatizo bali huyazidisha. Hata hivyo, hakuna shakhsiya kuu katika Historia iliyopuuzwa nchi za Magharibi kama Muhammad."
  [*Mohammad At Mecca*, Oxford, 1953, Uk. 52]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Alphonse de Lamartine

*(1790-1869) Mshairi na kiongozi wa kifaransa:*

- "Mwanafalsafa, msemaji, mtume, mwanasheria, shujaa, mshindi wa nadharia, aliyeweka imani ya kimantiki, ya dini isiyo ya kufikirika; mwanzilishi wa himaya ishirini za ulimwengu na moja ya kidini; huyo ni Muhammad. Ana daraja ambazo mwanaadamu yeyote mkuu anatakiwa apimwe kwazo, hata tungeliweza kuuliza, je kuna mwanaadamu aliye mkuu kuliko yeye?"
  [Imefasiriwa kutoka: *Histoire De La Turquie*, Paris, 1854, Juz. II, Uk. 276-277]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Reverend Bosworth Smith

*(1794-1884) Koleji ya Trinity, Oxford.*

- "… yeye alikuwa ni Caesar na ni Papa (Pope); lakini alikuwa ni Pope bila ya kuwa na mambo ya Pope, na alikuwa ni Caesar bila ya kuwa na majeshi ya Caesar. Bila ya majeshi yaliyo tayari kwa vita, bila ya mlinzi, bila ya kasri, bila ya kuwa na pato maalum, ikiwa mtu ana haki ya kusema kuwa alitawala kwa haki ya Mungu, basi huyo alikuwa ni Mohammed; kwani yeye alikuwa na nguvu zote bila ya kutumia vifaa vyake na kuungwa mkono."
  [*Mohammed and Mohammedanism*, London, 1874, Uk. 235]

## Mohandas Karamchand **Gandhi**

*(1869-1948) Mwanafikra wa India , kiongozi wa nchi:*

- "....Nimeridhishwa kwa kukubali kabisa kwamba si upanga ulioupatia ushindi Uislamu katika siku hizo katika utaratibu wa maisha. Ulikuwa ni unyenyekevu mnyoofu, uzuri wa tabia wa Mtume, alivyokuwa akiuchukulia wito wake, kujitolea kwake kwa marafiki na wafuasi wake, ushujaa wake, ujasiri wake, kuamini kwake Mungu na wajibu wake katika kazi yake. Mambo haya, na si upanga, ndiyo yaliyowapatia kila kitu na kushinda kila tatizo."
  [*Jarida la Young India* (periodical), 1928, Toleo X]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Edward Gibbon

*(1737-1794) Anachukuliwa kuwa ni mwanahistoria mkuu wa Uingereza wa zama zake:.*

- "Mafanikio makuu ya maisha ya Mohammad yalipatikana kutokana na nguvu ya maadili kamili bila ya kutumia upanga."
  [*History Of The Saracen Empire*, London, 1870]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## John William Draper

*(1811-1882) Mwanasayansi wa kimarekani, mwanafalsafa na mwanahistoria:*

- "Miaka minne baaada ya kifo cha Justinian, A.D. 569, huko Makka, Arabia, alizaliwa Mohammed ambaye yeye, miongoni mwa watu wote, aliweza kuwaathiri wanaadamu."
  [*A History of the Intellectual Development of Europe*, London, 1875, Juz.1, Uk. 329-330]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## David George Hogarth

*(1862-1927) Mwingereza mtunzi, na mwangalizi wa Makumbusho ya Ashmolean, Oxford:*

- "Iwe ni jambo kubwa au dogo, lakini maadili yake ya kila siku yameunda kanuni inayotekelezwa na mamilioni ya watu kwa dhamira hasa. Hakuna katika wanaadamu anayechukuliwa kuwa ni mtu anayefuatwa kwa karibu zaidi kama yeye. Mwenendo wa mwanzilishi wa ukristo haukuathri maisha ya kawaida ya wafuasi wake. Aidha, hakuna mwanzilishi wa dini aliyekuwa na heshima ya utukufu wa kipekee kama wa Mtume wa kiislamu."
  [*Arabia*, Oxford, 1922, Uk. 52]

*Namna hii anakubainishieni Mwenyezi Mungu Aya zake ili mpate kufahamu*
(Qur'an 2:242)

**Wasiokuwa Waislamu wanasema**

## nini juu ya ...

# 'Ali

## MRITHI WA KWANZA WA MTUME MUHAMMAD

*(Rehma na amani ziwe juu yao)*

Imam Ali bin Abi Talib alikuwa ni mrithi wa Mtume Muhammad, amani ziwe juu yao. Huu ni mkusanyiko wa nukuu fupi fupi kumhusu yeye kutoka kwenye maelezo mbali mbali ya wasomi wa imani nyingine, wakiwamo wanataaluma, waandishi, wanafalsafa, washairi, wanasiasa na wanaharakati.

## Simon Ockley

*(1678-1720) Profesa wa lugha ya kiarabu katika chuo kikuu Cambridge:*

- "Jambo moja maalum ambalo lapaswa kugunduliwa kwa Ali, ni kwamba mama yake alimzaa Makka ndani ya Al-Kaaba, ambapo haijawahi kutokea kwa mtu yeyote."
  [*History of the Saracens*, London, 1894, Uk. 331]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Washington Irving

*(1783-1859) Aalijulikana kama "The first American man of letters":*

- "Ali alikuwa anatokana na tawi lenye heshima kuu katika matawi ya kikureishi. Alikuwa na sifa tatu zilizokuwa zikitukuzwa sana kwa waarabu: Ujasiri, ufasaha na ukarimu. Moyo wake usio na hofu ulimpatia sifa kutoka kwa Mtume ya kuwa simba wa Mungu, mifano ya ufasaha wake imebaki katika baadhi ya semi na kuhifadhiwa miongoni mwa waarabu; na ukarimu wake ulionekana dhahiri katika kupenda kwake kugawanya na watu, kila siku ya ijumaa, kile kilichobaki katika hazina. Kuhusu utukufu wake, tumetoa mifano mara kwa mara; utukufu wake ulichukia kila kitu chenye udanganyifu na uchoyo."
  [*Lives of the Successors of Mahomet*, London, 1850, Uk. 165]

- "Yeye alikuwa ni mmoja wa miongoni mwa wa mwisho na wenye thamani miongoni mwa waislamu wa kale, ambaye alikusanya nguvu ya kidini kwa ushindi akiwa na Mtume mwenyewe, na kufuata ruwaza ya mwisho kabisa ya Mtume Muhammad. Yeye ni mtu anayetajwa kwa heshima kama khalifa wa kwanza aliye kirimu na kulinda elimu. Alikuwa ndani ya mashairi yeye mwenyewe, na nyingi miongoni mwa methali na semi zake zimehifadhiwa na kufasiriwa katika lugha mbalimbali. Pete lake ulikuwa na maandishi hili: 'Ufalme ni wa Mwenyezi Mungu'. Moja katika semi zake inaonyesha jinsi alivyokuwa hathamini vivutio vinavyopita tu vya dunia, ni (kusema kwake): 'Maisha ni kivuli tu cha mawingu - ndoto ya mwenye kulala.'"
  [*Lives of the Successors of Mahomet*, London, 1850, Uk. 187-8]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Robert Durey Osborn

*(1835-1889) Meja wa kikosi cha the Bengal Staff Corps:*

- "Pamoja naye umepotea moyo hasa na Muislamu bora ambaye Historia ya Mohammad imehifadhi kumbukumbu hiyo."
  [*Islam Under the Arabs*, 1876, Uk. 120]

**kwaw kujua habari zaidi juu ya Imam 'Ali bin Abi Talib, tazama Tovuti:**
***http://al-islam.org/faq/***

## Thomas Carlyle

*(1795-1881) Mwanahistoria mskochi, mkosoaji, na mwandishi wa elimu ya jamii:*

- "Kuhusu huyu kijana Ali, mtu yeyote atampenda tu. Ni kiumbe mwenye akili kuu, kama anavyojionyesha yeye mwenyewe sasa, na kila siku na baadaye; mwenye mapenzi maridhawa, mwenye ujasiri wa hali ya juu. Ana uungwana; shujaa kama simba; huku akiwa na huruma, ukweli na mapenzi yafaayo kwa imani ya kikristo."
  [*On Heroes, Hero-Worship, And the Heroic in History*, 1841, Hotuba 2: The Hero as Prophet. Mahomet: Islam., Mei 8, 1840)]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Edward Gibbon

*(1737-1794) Mwanahistoria mkuu wa kiingereza katika enzi zake:*

- "Sifa kuu alizokuwa nazo Ali hazikuzidiwa na mbadilishaji dini yeyote wa siku za hivi karibuni. Alichanganya sifa za kuwa ni mshairi, mwanajeshi, na mcha Mungu; busara zake bado zinapatikana kwenye mkusanyiko wa misemo yake ya kimaadili na ya kidini; na kila adui, kwenye vita vya maneno au vya upanga, alishindwa na ufasaha na ujasiri wake. Kuanzia saa ya mwanzo ya ujumbe wake wa dini mpaka mwisho wa ibada za kuzikwa kwake, Mtume Muhammad hajaachwa kuwa na rafiki mkarimu, ambaye alifurahishwa kwa kumwita kuwa ni ndugu yake, wasii wake, na kuwa yeye (Ali) ni 'Harun mwaminifu' wa 'Nabii Musa' wa pili."
  [*The Decline and Fall of the Roman*

*(1886-1978) Profesa wa lugha za kisemiti, Chuo kikuu cha Princeton:*

- "Shujaa vitani, mwenye busara katika ushauri, fasaha wa kuzungumza, mkweli kwa marafiki zake, anayeheshimiwa na maadui zake. Yeye alikuwa ni ruwaza wa heshima na maadili mema ya kiislamu. Na alikuwa ni Suleiman wa utamaduni wa kiarabu, ambapo kwake mashairi, methali, hotuba na simulizi - zisizo na idadi - zimekusanyika."
  [*History of the Arabs*, London, 1964, Uk. 183]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Sir William Muir** *Empire*, London, 1911, Juz. 5, Uk. 381-2]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Philip Khuri Hitti

*(1819 - 1905) Msomi na kiongozi wa kiskochi. Alikuwa na wadhifa wa Waziri wa mambo ya nchi za nje katika serikali ya India, pia alikuwa Lieutenant Gavana wa mkoa wa Kaskazini Magharib:*

"Alijaaliwa kipaji cha maarifa, mwenye mapenzi, na mwenye kujifunga na urafiki, tangu uvulana wake alikuwa amejitolea roho na moyo wake kwa Mtume. Mnyenyekevu, mpole, na asiyependa makuu. Ambapo baada ya kupita siku kadhaa, alipotawala nusu ya ulimwengu wa kiislamu, kwa hakika alilazimishwa pasi na kutaka."

[*The Life of Mahomet*, London, 1877, Uk. 250]

### Dr. Henry Stubbe

*(1632-1676) Muhafidhina, Mwanafizikia, na mwanafalsafa:*

- “Hakuipenda dunia na mapambo yake bali alimcha sana Mwenyezi Mungu, alitoa sadaka nyingi, alikuwa mwadilifu katika vitendo vyake vyote, mnyenyekevu na mwepesi wa kuzoeana na watu; huku akiwa na maneno ya ya haraka ya kufurahisha na ubunifu usio wa kawaida, alikuwa na elimu maridhawa, sio elimu zinazoishia kwa maneno tu bali zinazoendelea kwa vitendo.”
  [*An Account of the Rise and Progress of Mahometanism*, 1705, Uk. 83]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

### Gerald de Gaury

*(1897 - 1984) Mwanajeshi mahiri na mwanadiplomasia:*

- “Alikuwa ana hekima sana katika kutoa ushauri, na shujaa vitani, mkweli kwa marafiki zake na mkarimu kwa maadui zake. Yeye daima alikuwa ni ruwaza ya heshima na maadili mema ya kiislamu.”
  [*Rulers of Mecca*, London, 1951, Uk. 49]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

### Wilferd Madelung

*Profesa wa lugha ya kiarabu, chuo kikuu cha Oxford:*

- "Kwenye madai ya uongo ya Bani Umayya ya kuuhaalisha utawala wa Mwenyezi Mungu kuwa wao ni makhalifa wa Mungu duniani, na ulaghai wao na serikali yao yenye mizozo na kulipiza kisasi, pamoja na hayo yote, waliukubali uaminifu wake kutolegalega kwake na kujitolea katika kuutumikia uongozi wa kipindi hicho wa kiislamu, uaminifu wake binafsi, kuwatendea usawa wote waliomuunga mkono na pia ukarimu wake wa kuwasamehe maadui wake aliowashinda."
  [*The succession to Muhammad: a study of the early caliphate*, Cambridge, 1997, Uk. 309-310]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

### Charles Mills

*(1788 - 1826) Mwanahistoria bingwa wa enzi zake:*

- “Akiwa ni kiongoazi wa familia ya Hashim na binamu na mkwe wa (Mtume) ambaye waarabu walimheshimu… inashangaza kuwa Ali hakuandaliwa kuwa khalifa mara tu bada ya kufa Muhammad. Pamoja na heshima ya kuzaliwa kwake na ndoa yake, pia alikuwa na urafiki na Mtume. Huyu mtoto wa Abu Talib alikuwa ni wa mwanzo kuingia Uislam na alikuwa ni kipenzi cha Mohammad, kwani alikuwa ni wa pili kama alivyokuwa Harun kwa Musa. Kipaji chake kama msemaji, na ujasiri wake kama shujaa, vilitukuzwa na taifa ambalo ujasiri ulikuwa ni sifa njema na ufasaha ulikuwa ni busara.”

[*An history of Muhammedanism*, London, 1818, Uk. 89]

Mtume Muhammad (s) alisema:
**Mimi ni nyumba ya hekima na 'Ali ni mlango wake**

(*Sahih al-Tirmidhi*, (Toleo la Cairo), Kitab al-Manaqib, juzuu ya. 5, Uk wa 637., Hadith namba 3723)

# Hutuba ya herufi za kiarabu Zisizo na nukta

Maarifa, hekima na ufasaha wa Imamu Ali bin. Abi Talib (a) ni maalumu miongoni mwa Waislamu wa madhehebu zote za wanafikra. Mojawapo ya mfano wa ustadi wake juu ya lugha ya Kiarabu umejitokeza wenyewe katika mahubiri haya ambayo ni ya papo kwa papo , katika maandishi yake ya herufi za kiarabu zisizo na nukta, yoyote!!

## Ni kitu gani makhususi kuhusu hutuba hii?

Wale wanaojua Kiarabu au wanaoweza angalau kusoma maandishi ya Qur'an hufahamu kwamba baadhi ya herufi za alfabeti ya Kiarabu zisizo na nukta zilizohusishwa na wao. Alfabeti hizi zimetajwa hapa chini na zinatumika wakati wote katika hutuba za Kiarabu na matini zilizoandikwa.

ش ب ت ن ض ث ق ف غ خ ج ز ظ ذ ي

Kubuni maandiko ya aina yoyote yenye maana, bila ya kutumia herufi yoyote kati ya hizo, ni kazi ngumu. Kufikisha hutuba kama hiyo bila ya maandalizi rasmi, kama Imamu Ali (a) inajulikana kuwa akifanya hivyo kwa mahubiri yake yote, ni muujiza kweli!
[Kumbuka: herufi zinawakilisha zaidi marbutah yaliyotumika kuandikwa bila herufi za kiarabu zisizo na nukta mwanzoni mwa maandiko ya Kiarabu]

## Je! kuna mahubiri mengine yoyote?

Imam ‘Ali (a) mara tu alipofikisha hutuba nyingine nzuri ambayo haikuwa na herufi ya alif !!
Herufi hizi za alfabeti za Kiarabu bila shaka ni tabia ya kawaida kutokea katika lugha. Kama kutunga sentensi chache bila ya maana ni vigumu sana, vipi kuhusu kutoa mahubiri, ambayo yamejaa hekima na ambayo mara nyingi ukubwa wa muonekano wake unavutia, lakini bila hata kutumia herufi ya alif !!

Mahubiri haya kawaida huitwa al-Khutbah al-Muniqah na hurikodiwa na wasomi wengi wa Kiislamu. Miongoni mwa wanavyuoni ambao wamenukuu hutuba hizi wameweza kutajwa:

- Muhammad b. Muslim al-Shafi’i, *Kifayat al-Talib*, uk. 248
- Ibn Abi’l Hadid al-Mu’tazili, *Sharh Nahj al-Balaghah*, vol. 19, uk. 140

## Ni vipi Imam Ali (a.s) aliweza kukamilisha maajabu haya?

Imam 'Ali (a) alipata elimu yake kubwa na kwa ufasaha, kwa uadilifu wake wa muda mrefu na kwa uhusiano wake wa karibu na Mtume Muhammad (s). Mtume (saww), kutokana na msukumo wa wahyi kutoka kwa Allah (s.w.t), ni chanzo cha maarifa yote na hekima na mwalimu bora kwa Imamu Ali (a).

**Ili kujua zaidi kuhusu Uislamu halisi, kama ulivyofundishwa na Mtume Muhammad (s) na kama ulivyoelezwa na Imamu Ali (a) baada yake, tembelea:**

***http://al-islam.org/faq/***

Sifa zote ni za Mwenyezi Mungu, Mfalme mwenye kusifiwa, Mwenye upendo, Muumba wa viumbe wote wenye kuzaliwa (na visivyozaliwa), huchukua hatua kwa kila mwenye kukandamizwa, Mnyooshaji wa ardhi, Muanzilishi wa milima madhubuti, Mwenye kuleta mvua, Mwenye kuondosha matatizo, Mjuzi na Atambuaye yaliyo ya siri, Mwangamizi wa falme na kuharibu vile wanavyomiliki, Msamehevu kwa wliokosea na wakatubia makosa yao, Yeye ni chanzo cha kila kitu na mashukio yao ni kwake. Ukarimu wake mkubwa na kutosha kulikoenea mawinguni na usambazaji wa mvua.

Anajibu kwa aombaye au atumainiaye, hutoa kwa mapana na kwa wingi.
Mimi humsifu bila ukomo. Ninamfikiria yeye mmoja tu kama vile afikiriavyo wale ambao hurejea kwake. Tazama! Yeye ni Mwenyezi Mungu, hapana mungu ila Yeye kwa ajili ya mataifa. Hakuna mtu anayeweza kupotosha haki na aliyoyaanzisha. Alimtuma Mtume Muhammad mpelekaji ujumbe wa utii (Uislamu), kiongozi kwa ajili ya viongozi na muonyaji wa wanao kandamizwa, Mdhoofishaji wa mamlaka ya Wudd na Sawa `(masanamu mawili). Alitoa taarifa na elimu, alielekeza na kukamilisha. Alianzisha misingi na kuwawekea (watu kuifuata), Alisisitiza ahadi maalumu (ya Siku ya Kiyama) na alionya. Mwenyezi Mungu naye alimuongoza kwa heshima na kumpa amani ya nafsi yake, na Mwenyezi Mungu huwa na huruma juu ya dhuriya zake na familia yake inayoheshimiwa, kwa muda mrefu kama nyota zinavyoongoza na kukuangazia, mwezi muandamo unaendelea kuongezeka, na kukaririwa umoja wa (La ilaha illa Allah) kunafanywa na kusikika kote.

Mwenyezi Mungu akulinde! Kuwajibika kuelekea kwenye matendo bora. Hivyo tembea kweye njia kutafuta halali, na kuacha ya haramu na kuyapuuza kabisa. Kusikiliza amri za Mwenyezi Mungu na kuwa na ufahamu wa hayo. Kudumisha mahusiano na kuyaendeleza. Kutotii tamaa na pia uzipuuze.Shikamana kama ndugu, pamoja na watu wema na wacha Mungu, na kuachana na mambo ya pumbao na uchoyo.
Unadhifu wako utakuepusha na makosa ya watu huru kwa kuzaliwa, wakarimu mno na wenye heshima na utukufu, na wenye nasaba nzuri. Hapa alikuja kwako, alichukua jamaa yako kwa idhini, katika ndoa, bibi mtukufu. Alitoa mahari, kama Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa Umm Salamah. Hakika, yeye [s] alikuwa ni mwenye neema na mwana wa kisheria. Mwema kwa uzao wake. Akawapa katika ndoa ambaye alimtaka. Wala hakuchanganyikiwa katika uchaguzi wake wa mke wala hakuwa amekosea.

Namuomba Mwenyezi Mungu, kwa niaba yako, kwa neema za kudumu na uhusiano wake. Na muendelezo wa raha zake, na ili kuhamasisha watu wote: kurekebisha hali zao wenyewe, na maandalizi kwa ajili ya hatima yao binafsi na Akhera. Shukrani ni zake milele na sifa kwa Mtume wake Muhammad [s].

Hotuba hii inaonekana kuwa ilitolewa na Imamu Ali (a) wakati wa ndoa ya mtu (nikah), na inaweza pia kuwa ndoa yake mwenyewe. Imenukuliwa na wasomi kadhaa kama vile:

- Muhammad Rida al-Hakimi, *Saluni qabl an tafqiduni*, juzuu. 2, uk. 442-3.
- Sayyid al-Musawi, *al-Qatarah min bihar manaqib Aal-Nabi wa al-`Itrah*, juzuu. 2, uk. 179
- Hasun al-Dulafi, *Fada'il Aal al-Rasul*, uk. 6
- Hasun al-Dulafi, *Fada'il Aal al-Rasul*, p. 6

*Wala usiwadhani wale waliouwawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wa hai, wanaruzukuiwa kwa Mola wao.*
(Qur'an 3:169)

## Wanayosema wasio Waislamu juu ya...

# Husein

MRITHI WA TATU WA MTUME MUHAMMAD
*(Rehma na Amani ziwashukie)*

Imam Husein alikuwa ni mjukuu wa Mtume Muhammad, amani ziwashukie, aliyeuwawa shahid na majeshi maovu ya utawala wa kiimla. Ufuatao ni mkusanyiko wa nukuu fupi fupi kuhusu yeye kutoka kwa watu mbalimbali mashuhuri duniani.

## Edward G. Brown

*Sir Thomas Adams Profesa wa lugha ya kiarabu na masomo ya kimashariki katika chuo kikuu cha Cambridge:*

- "… ni kumbukumbu ya uwanja uliojaa damu wa Kerbala, ambapo mjukuu wa Mtume alianguka, akateswa na kiu na kuzungukwa na miili ya watu wake waliouwawa, kifo hicho wakati wowote chatosha kuchemsha hisia kali hata za asiyejali, na moyo ambao uchungu, hatari na kifo hupungua na kuwa mdogo mno."
  [*A Literary History of Persia*, London, 1919, p. 227]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Ignaz Goldziher

*(1850-1921) Mhangari mashuhuri na msomi wa kimashariki:*

- "Tangu siku ile nyeusi ya Karbala, historia ya kizazi hiki…imekuwa ni mlolongo wa kutabika na mateso. Haya huelezwa kwenye mashairi na tungo fasihi za kuhusu kufa shahid - kwenye madhehebu ya Shia - na kufanya majilisi za Shia kuwapo katika mwanzo wa mwezi wa Muharram, ambapo siku ya kumi (*a'shura*) huwekwa kuwa ni siku maalum ya kumbukumbu ya msiba wa Karbala. Matukio ya janga hilo huwa yanaonyeshwa kwa njia ya *ta'aziya.* 'Sikukuu zetu ni siku za maombolezi', akitimiza mashairi haya ni amiri wa kuieleza hali ya Mashia akikumbusha mitihani mingi iliyokipata kizazi cha Mtume. Manung'uniko na maombolezo juu ya maovu na mateso waliyofanyiwa kizazi cha Ali, na maombolezo juu ya watu wake waliokufa mashahid: Haya ndiyo mambo ambayo wafuasi wao waaminifu hawawezi kuyaacha. Hata kuna methali isemayo: '..Yahuzunisha zaidi kuliko machozi ya Shia..' imekuwa ni methali itumikayo ya kiarabu."
  [*Introduction to Islamic Theology and Law*, Princeton, 1981, Uk. 179]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

## Edward Gibbon

*(1737-1794) Anayechukuliwa kuwa ni mwanahistoria mkuu wa kiingereza enzi zake:*

- "Katika enzi hizo na hali ya hewa ya wakati huo, mandhari ya huzuni ya kifo cha Husein yataamsha hisia za huruma za msomaji asiye na huruma."
  [*The Decline and Fall of the Roman Empire*, London, 1911, Juz. 5, Uk. 391-2]

**Kwa maelezo zaidi juu ya Imam Husein na tukio la msiba wa Karbala, tazama Tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

**Peter J. Chelkowski**

*Profesa wa elimu ya mambo ya Mashariki ya kati, Chuo kikuu cha New York:*

- "Husein alikubali mwito na akaondoka Makka akiwa amefuatana na familia yake na kikosi cha wafuasi wake wapatao sabini. Lakini alipofika ardhi kame ya Karbala, walishtukizwa ghafla na uvamizi uliofanywa na khalifa Yazid. Japokuwa walionekana wazi kushindwa, lakini Husein alikataa kuukubali utawala wa Yazid. Wakiwa wamezingirwa na jeshi kubwa la maadui, Husein na watu wake walikaa bila ya kuwa na maji kwa siku kumi wakiwa katika jangwa lenye joto kali la Karbala. Hatimaye, Husein, watu wazima na baadhi ya wavulana katika familia yake na ya maswahaba wake walikatwakatwa kwa mishale na mapanga ya jeshi la Yazid; wanawake upande wake na watoto waliosalia walitekwa nyara na kupelekwa kwa Yazid mjini Damascus. Mwaandishi mashuhuri wa historia, Abu Rayhan al-Biruni asema: '… kisha moto uliwashwa kwenye kambi zao na miili yao kukanyagwa na kwato za farasi; ambapo katika historia ya mwanaadamu hakuna aliyepata mauaji mabaya kama hayo.'"
  [*Ta'ziyeh: Ritual and Drama in Iran*, New York, 1979, Uk. 2]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Simon Ockley**

*(1678-1720) Profesa wa lugha ya kiarabu katika chuo kikuu cha Cambridge*:

- "Kisha Husein akapanda farasi wake, akaichukua Qur'an na kuilaza mbele yake, akaenda kwa watu na kuwataka watekeleze jukumu lao: akiongeza, 'Ewe Mola, wewe ndiye tegemeo langu katika kila tatizo, na ni tumaini langu katika kila janga!'… Kisha akawakumbusha utukufu wake, heshima ya kuzaliwa kwake, ukuu wa nguvu zake, akasema, 'Hebu fikirieni wenyewe mtu kama mimi niwe ni bora au si bora kwenu; Mimi ni mtoto wa binti ya Mtume wenu, asiye na mfano wake duniani. Ali ni baba yangu; Jaafar and Hamza, viongozi wa mashahid, wote ni ammi zangu; na Mtume wa Mwenyezi Mungu - amani zimshukie - alisema, mimi na ndugu yangu, sisi sote ni viongozi wa vijana wa peponi. Ikiwa mwaniamini niyasemayo ni ya kweli, wallahi, sijasema uongo tangu niwe na fahamu zangu; kwa sababu Mwenyezi Mungu anachukia uongo. Ikiwa hamuniamini, waulizeni maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu [hapa aliwataja], na watawaambia hivyo hivyo. Hebu nirejee nyuma kwa nilicho nacho.' Wakamuuliza, 'Ni nini kilichomzuia asiongozwe na mahusiano yake hayo.' Akajibu, 'Mungu akataza mimi nisiache kupigania haki yangu kiholela tu. Nina sababu ya Mungu ya kupambana na kila mtawala wa mabavu asiyeamini siku ya hisabu.'"
  [*The History of the Saracens*, London, 1894, Uk. 404-5]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Reynold Alleyne Nicholson**

*(1868-1945) Sir Thomas Adams Profesa wa kiarabu, chuo kikuu cha Cambridge:*

- "Husein alianguka, akadungwa na mshale, na wafuasi wake mashujaa wakakatwakatwa wakiwa pamoja naye hadi mtu wa mwisho. Mila ya Muhammad, ambayo daima ilipinga utawala wa Bani Umayya, humzingatia Husein kama shahid, na Yazid kama muuaji wake."
  [*A Literary History of the Arabs*, Cambridge, 1930, Uk. 197 ]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Robert Durey Osborn**

*(1835-1889) Meja wa Kikosa cha Bengal:*

- "Husein alikuwa na mwana mwenye umri wa mwaka mmoja tu aitwaye Abdallah. Alikuwa amefuatana na baba yake katika kuelekea kwenye janga. Huku Husein akiwa ameathiriwa na kulia kwa mwanawe, alimbeba na kumuweka mkononi kwake na akaanza kulia. Wakati huo huo, mtoto alidungwa na maadui na kutobolewaa sikio lake, na kufariki mikononi mwa babake. Husein aliiweka maiti hiyo ndogo ardhini na kusema: 'Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea!' Kisha akalia akisema: 'Ee Mola! Nipe nguvu ya kuvumilia misiba hii!' … Akilemewa na kiu, na amechoka kutokana na majeraha aliyokuwa nayo, alipigana kishujaa sana na kuwaua baadhi ya maadui. Hatimaye alikatwa kutokea upande wa nyuma; akadungwa kwa nguvu mgongoni na kuanguka chini; wakati muuaji wake alipokuwa akiitoa silaha yake, mwanawe Ali alianguka akiwa tayari ameshakufa. Kichwa ikilikuwa kimeharibiwa kwa kukatwa; na mwili wake usio na kichwa ukakanyagwa na kwato za farasi wa maadui; asubuhi iliyofuata watoto na wanawake waliobaki hai walipelekwa mji wa Koufa. Miili ya Husein na wafuasi wake waliouwawa iliachwa bila kuzikwa pale ilipoanguka. Kwa siku tatu ilibaki ikipigwa na jua na umande wa usiku, na kuvamiwa na tai na wanyama wengineo; lakini kisha wakaazi wa viji vya jirani walihuzunishwa kuwa mwili wa mjukuu wa Mtume uwe katika hali hiyo ya aibu ukiachiwa wanyama wachafu, hivyo hawakujali hasira za Ubaidallah, waliuzika mwili wa shahid huyo na ya marafiki zake mashujaa.
  [*Islam Under the Arabs*, Delaware, 1976, Uk. 126-7]

✶ ✶ ✶ ✶ ✶

**Sir William Muir**

*(1819-1905) Msomi Mskochi na kiongozi. Alikuwa waziri wa mambo ya nchi za nje katika serikali ya India na Luteni Gavana wa mkoa wa Kaskazini Magharibi.*

- "Msiba wa Karbala haukuamua tu majaaliwa ya ukhalifa, bali pia ufalme wa ummah ya Mohammed muda mrefu baada ya ukhalifa kutoweka."

[*Annals of the Early Caliphate*, London, 1883, Uk. 441-2]

*...Na mcheni Mwenyezi Mungu, naye Atawafundisha...*
(Qur'an, 2: 282)

Mtume mtukufu (s.a.w.w.) wa Uislamu amesema: “Kutafuta elimu ni wajibu kwa kila Muislamu, mwanamume au mwanamke.”
[Al-Majlisi *Bihar al-Anwar,* Juz. 1. Uk. 177]

## Thamani ya roho ...

# Kutafuta Elimu

Kulingana na mafunzo ya kiislamu, kutafuta elimu ni moja katika matendo ya ibada yamuongozayo mtu kwenye njia ya Peponi. Hata hivyo, lengo la kutafuta elimu ni muhimu zaidi kuliko hata elimu yenyewe. Kutafuta elimu ya kweli kwa lengo la kidini, kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu na kuwahudumia viumbe wake, humpeleka mtu Peponi akiwa pamoja na mitume na mawalii. Lakini kutafuta elimu kwa madhumuni ya kibinafsi, au mazoea tu, au kwa malengo ya kidunia humpeleka mtu kwenye ujinga, madhambi kwa viumbe, na hatimaye kuingia Motoni.

## Mambo muhimu kwa atafutaye elimu

- Mtu anayepaswa kutafuta elimu ni lazima, hatua ya kwanza kabisa, apitie utakaso wa kiroho, aingize *taqwa* (uchaji Mungu) ndani ya roho yake, aondoshe nia mabaya na malengo ya kidunia, na kujipima mara kwa mara kuangalia iwapo elimu yake anaitafuta kwa ajili malengo ya kidunia. Mtu ni lazima akumbuke kwamba kumcha Mungu ni sifa maalum ya *'alim* (mwanachuoni) na yeyote asiye kuwa na ucha Mungu huyo yuko nje ya daraja za wenye elimu, hata akiwa amehifadhi vitu vingi moyoni au awe anavutia anapozungumza.
- Katika kila hatua ya kutafuta elimu, ni lazima ufikiri kwa undani sana kuhusu lengo lako la msingi la kutafuta elimu. Jiulize: kwa nini natafuta elimu? Je ni kwa ajili ya kupata kazi nzuri, au kushindana na mwenzio au na kikundi, au kupata tuzo, shahada au nafasi kubwa katika jamii? Ikiwa unatafuta elimu ya juu, je waitafuta kwa ajili tu ya kuandika vitabu, nakala, au kutoa hotuba ili usifiwe kuwa ni mwanamume au mwanamke msomi? Au kwa sababu ya kumridhisha Mungu na kuwatumikia waja wake?
- Elimu uipatayo ni lazima ikuongoze uwe mwema zaidi, ufanye vitendo vya uaminifu na ikufanye umpende na kumcha Mungu zaidi wakati ukiendelea. Elimu isiyomuongoza mtu kufanya mambo mema, hiyo si elimu ya kweli. Elimu inayoishia kwenye maneno tu na haina vitendo vyenye kuwatumikia viumbe wa Mwenyezi Mungu hiyo ni elimu duni sana na itatoweka na wakati.
- Chunguza tabia yako wakati ukitafuta elimu. Je elimu yakufanya uwe mnyenyekevu zaidi na mvumilivu kwa marafiki zak na wenzio? Au itakufanya uwe jeuri, mwenye kibri na mbishi? Je inafanya iwe ni vigumu kwako kukubali ukweli na kukubali kibri chako kwenye kadamnasi ya watu? Je inakufanya uwaonee wivu wale wenye elimu zaidi yako? Kumbuka kwamba ubinafsi unaondoshwa na kufutwa kwenye elimu ya kweli, miongoni mwa alama za maadili ya elimu ya kweli nikutokuwa na ubinafsi, ujuba, kujipenda na kibri.
- Unapokuwa ukitafuta elimu, basi daima muamini Mungu, mheshimu mwalimu wako na usione haya kujifunza hata kutoka kwa mdogo wako. Durusi na zingatia chochote ulichokisoma. Kila siku muombe Mwenyezi Mungu akusaidie na huruma zake akupe fikra njema, na akulinde kutokana na kuitumia elimu unayoipata kwa ajili ya mambo ya kidunia na malengo ya kibinafsi.

## Hitimisho:

- Imam Ali (a.s.) amesema: "**Mtu anayejitolea kwenda kutafuta elimu ni kama anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu.**" [Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar*, Juz. 1, Uk. 179]

**Kwa maelezo zaidi juu ya Uislamu sahihi, tazama Tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

## Ukweli wa elimu

- Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amesema: "**Elimu si kitu kinachopatikana kwa kusoma sana, bali ni nuru ya Mwenyezi Mungu anayoiingiza ndani ya moyo wa mja wake apendaye kumuongoza.**" [Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar*, Juz. 67, Uk. 140]
- Matawi yote ya elimu, licha ya asili yake, yanaweza kugawanywa katika mafungu mawili: (1) Elimu ya Akhera, ambayo lengo lake kuu ni kufikia daraja ya juu ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, kuwatumikia viumbe wa Mungu, na kupata malipo mema ya Akhera. (2) Elimu ya kidunia, ambayo lengo lake kuu ni kupata mambo ya kimaada, utajiri, cheo cha kijamii, na kujitosheleza kwa tamaa za kibinafsi. Kwa hivyo, ni nia ya kupata elimu ndiyo inayoangaliwa, aidha itakuwa ni ya kidunia au ni kwa ajili ya Akhera.
- Kila roho inayoendelea kujitakasa kutokana na mielekeo michafu na ubinafsi itapata motisha wa kimalaika. Hivyo basi elimu anayoipata mtu ni ya kweli, ni ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu inamuongoza kufanya matendo mema na kumuelekeza kuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Elimu hii ya kweli ni taa ya kiroho inayomuonyesha njia ya moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu na kwenye makazi ya baraka Zake.
- Roho inayotawaliwa na ubinafsi na mielekeo miovu hupata motisha wenye hulka za kishetani, na hivyo kumuongoza kwenye ujinga-mkanganyo (m.y. Mtu kuwa mjinga na kutojua kama yeye ni mjinga), na kwenye kifuniko chenye utata kinachoziba ukweli wa lengo la Mwenyezi Mungu la kuumba, dhati ya Mwenyezi Mungu, na maisha ya Akhera. Kwa hivyo, elimu yoyote inayopatikana moja kwa moja kwa malengo ya kidunia, ubinafsi, na matendo maovu, hatimaye ni yenye kupelekea motoni.
- Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amesema "**Hakika**, **elimu inakusanya mambo matatu: 'alama imara', 'wajibu adilifu', na '*sunnah* thabiti'. Zaidi ya hayo ni ziada tu.**" [Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 1, "*kitab fadhl ul-'ilm"*, *"bab sifat al-'ilm wa fadhluh*", Hadith #1]
- Neno 'alama imara' linamaanisha elimu yenye maana kiakili, miongozo sahihi na mafuzo ya Mwenyezi Mungu. 'Wajibu adilifu' inamaanisha elimu ya maadili na utakaso wa kinafsi. 'Sunnah thabiti' maana yake ni elimu yenye mitazamo ya kimaada na inahusisha aina ya harakati za kimwili. Kuna wakati ambapo kutafuta elimu huwa ni 'wajibu adilifu' na wakati mwingine huwa ni 'sunnah thabiti'.
- Elimu za utabibu, anatomia (viungo vya mwanaadamu), elimu ya falaki, unajimu n.k. ikwa zitaangaliwa kama ni ishara na alama za Mwenyezi Mungu, au elimu zinazohusu historia na ustaarabu, zitakapoangaliwa kama ni njia ya kupata funzo na kuwa na hadhari na matukio, haya yote yatawekwa katika fungu la \`alama imara', kwa sababu kwa njia ya hizo, elimu ya Mwenyezi Mungu au ya ufufuo hupatikana au huthibitishwa.

### Faida ya kutafuta elimu ya kweli

- Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amesema: **"Anayefuata njia ya kutafuta elimu, Mwenyezi Mungu humsahilishia ya kwenda Peponi. Na Malaika huwakunjulia mbawa zao watafutao elimu kwa kuridhika nao. Kila kiumbe aliyeko mbinguni na duniani humtakia msamaha atafutaye elimu, hata samaki baharini. Ubora wa mwanachuoni *(alim)* kwa mcha Mungu (*abid)* ni kama ubora wa mwezi kamili unapong'aa usiku juu ya nyota zingine. Wanavyuoni ni warithi wa mitume, kwani mitume hawakuacha urithi wa mali bali wa elimu. Kwa hivyo anayejishughulisha nayo hupata faida nyingi."** [Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 1, "*kitab fadhl ul-'ilm*", Hadith #1]

## Sifa za kimaadili za elimu ya kweli

- Elimu inapotafutwa kwa nia ya Mwenyezi Mungu, huifanya shakhsiya ya mtu kuwa ya kidini. Mtu kama huyo ana sifa zenye motisha wa Allah, na tabia, maneno na vitendo vyake huonyesha hayo.
- Imam Ali (a.s.) alikuwa akisema: '**Ewe mtafutaji elimu, elimu ina fadhla nyingi. (Ikiwa utaifikiria kuwa ni kama mwanaadamu) kichwa chake ni unyenyekevu, jicho lake ni kutokuwa na wivu, sikio lake ni kuelewa, ulimi wake ni ukweli, kumbukumbu yake ni kutafiti, moyo wake ni nia nzuri, utambuzi wake ni maarifa *(ma`rifah)* ya vitu na mambo, mkono wake ni huruma, mguu wake ni kuwatembelea wanavyuoni, azimio lake ni uaminifu, busara yake ni ucha mungu, makazi yake ni uokovu, kupanda kwake ni uaminifu, silaha yake ni ulaini wa mazungumzo, upanga wake ni kuridhika (*ridha*), jeshi lake ni kujadiliana na wanavyuoni, utajiri wake ni mwenendo mwema, akiba yake ni kutofanya madhambi, mahitaji yake ni safari ya mema, maji yake ya kunywa ni upole, mwongozo wake ni wa Mwenyezi Mungu, na marafikizake ni kuwapenda wateule."** [Al-Kulayni, *al-Kafi*, *kitab fadhl al-'ilm, bab al-nawadir*, Hadith # 3]
- Mtume Muhammad (s.a.w.w.) aliulizwa: "**Elimu ni nini?**" Akajibu: "**Ni kunyamaa kimya"**. Akaulizwa: "Kisha?" Akajibu: **"Kusikiliza kwa makini."** Akaulizwa tena: "Kisha?" Akajibu: **"Kukumbuka."** Akaulizwa: "Kisha?" Akajibu: **"Kuifanyia kazi** (uliyoisoma)." Akaulizwwa tena: "Kisha?" Akajibu: **"Kueneza."** [Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar,* Juz. 2, Uk. 28]
- Imam Ali (a.s.) alikuwa akisema: "**Kuna alama tatu za mwanachuoni: "Elimu, Subira na kuwa kimya**". [*Ibid*, Juz. 2, Uk. 59]

## Imekatazwa kutafuta elimu kwa…

Kulingana na mafunzo ya Ahlul Bayt (a.s.) wa Mtume (s.a.w.w.), imekatazwa kutafuta elimu kwa ajili ya mambo ya kidunia na malengo ya ubinafsi.

Imam Ali (a.s.) amesema: "**Usitafute elimu kwa malengo manne: (1) Kutukuzwa mbele ya watu wa elimu (2) Kushindana na asiye na elimu (3) Kujionyesha kwenye kadamnasi ya watu (4) Kuwavutia watu kwa minajli ya kupata ukubwa.**" [Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar,* Juz. 2, Uk. 31]

*... Na kwa nafsi na kuilinganisha kwake! Akaifahamisha uovu na takua yake. Hakika amefaulu aliyeitakasa*
(Qur'an, 91: 7-9)

Imam Ja'far al-Sadiq (as) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad(s) alipeleka kikosi cha jeshi (kwenye uwanja wa mapambano). Walipata ushindi wakati waliporudi kwao, yeye Mtume (s) alisema: '. Heri yao wale ambao walifanya *jihadi* ndogo na bado kufanya *jihadi* kubwa' Wakati alipoulizwa, 'Ni ipi *Jihad* kubwa? Mtume (s.a.w.w) akasema : '*jihadi* ya nafsi (mapambano dhidi ya wewe mwenyewe)' ".
[Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar*, Juzuu ya 19, uk. 182, hadith namba. 31]

# Faida za Nafsi ...

## Mapambano dhidi yaNafsi

# *(jihad al-nafs)*

Roho ya binadamu ni eneo la mapambano ya nguvu mbili za mashindano. Nguvu ya Mungu humvutia mtu kwenye nyanja ya mbinguni, na kumhamasisha kwenye matendo ya wema. Nguvu za kishetani humshawishi kuelekea maeneo ya giza na aibu, na kumualika kwenye matendo maovu. Wakati nguvu ya Mungu ni ushindi, mtu anaibuka kuwa mwema na mpole, kwenye ufuasi wa Mtume (S), watu wa Mungu, na wacha Mungu. Wakati, hata hivyo, vikosi vya kishetani hutawala, mtu anakuwa muasi na muovu na kuwa katika kundi pamoja na makafiri, madhalimu, watenda maovu na wale ambao wamelaaniwa.

**Ushauri wa muamko wa mapambano dhidi ya nafsi**

- Ni asili ya binadamu kumshukuru mwingine ambaye amekuwa mwema. Tafakari na kadiria zile fadhila za dhahiri na za siri alizotupa Mwenyezi juu yetu. Viumbe wote wa Mungu hawawezi hata kutoa sehemu ya fadhila hizo.
- Angalia hewa tunayopumua sisi mchana na usiku, na juu ya maisha yetu ambayo pia ile ya viumbe hai wengine ni tegemezi. Hakuna kinachoweza kubakia hai kama kikinyimwa hewa hata kwa dakika chache**.** Ni vipi zawadi hii ya ajabu ya Mungu! Kama watu wote wa ulimwengu wataungana pamoja kwa kazi hii, hawataweza kuunda zawadi hii, hawataweza kufanya hivyo. Katika njia hiyo hiyo, tafakari juu ya karama zingine za Mungu kama vile hisia za nje za mwili za kuona, kusikia, ladha, harufu, na kugusa, na uwezo wa ndani kama vile kufikiri, dhana, na kuhoji, kila mmoja ambaye amebeba faida zisizo na ukomo na ambazo zimetolewa kwetu na Bwana wetu. Mwenyezi Mungu Muumba na Mfalme wa ulimwengu huu. Binadamu, ni kiumbe aliyewekwa katika moja ya sayari ndogo, ameshindwa kabisa kufahamu kiwango kidogo cha dunia yake mwenyewe, jua ambalo hawezi hata kulilinganisha na sayari nyingine ya jua iliyoko mbali zaidi ya kundi la nyota. Mfumo wetu wa jua ni kitu kisicholinganishwa na mifumo kadhaa ya nishati ya jua, ambayo bado haijaepuka darubini yenye nguvu kubwa ya wapelelezi na wachunguzi. Angalia katika ubongo wa binadamu-ni kipi wanachovutia viumbe! Je, yawezekana binadamu kuunganisha jitihada zao na kuweza kufanya hata moja seli hai ya ubongo (kiini cha ubongo) ambayo Mwenyezi Mungu ameumba na ameiumba kwa wakati wote! Hakika hii akili tuliyopewa na Mungu inastahili kuwa kiti cha mawazo na maongozi mema tu, na wala sio mawazo mabaya!

Kila kiumbe hai katika ulimwengu huu kimo ndani mpangilio wa maono yake ya Kimungu, kwa hiyo mkumbuke Mungu na neema zake zote, na usiache kumtii. Yeye anatimiza mahitaji yetu yote bila ya kuwa na haja yoyote ya ibada yetu. Kama wewe utazishika amri zake au usizishike hakuna tofauti yoyote kwake. Ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe kwamba amekuusieni mazuri na amekuharamishieni uchafu. Nguvu na mawazo ya kishetani na kubadilisha maeneo ya akili yako kwenye ulimwengu wa Kimungu kwa kuondoa kwa nguvu yale maovu na kuyakaribisha majeshi ya Mungu, ili Mungu akusaidie na kukulinda katika hatari ya vitisho itakayokupata katika vita hii. Usiwe na matarajio yoyote kutoka kwa mtu yeyote isipokuwa Mungu. Kwa unyenyekevu wote na majonzi, macho yako yanaweza kuomba kwa Mungu na kutafuta msaada wake kwa kuibuka mshindi katika vita hii muhimu dhidi ya kujitegemea.

## Hitimisho:

- Imam Ali (as) akasema: ". Yule mapambano dhidi yake ili kutii amri ya Mungu, katika macho ya Mungu, kituo wake ni ule wa shahidi wacha Mungu" [Al-Amidi, Ghurar ul Hikam wa Durar ul Kalim, Hadith # 3546]

**Ili kujua zaidi kuhusu uislamu tembelea, tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

## Ni nini mapambano dhidi ya nafsi?

***Jihad al-nafs* ni mapambano dhidi ya mawazo mabaya, tamaa na nguvu ya tamaa, hasira, na kushibishwa mawazo, kuweka yote hayo chini ya utawala wa hoja na imani katika kutii amri za Mungu, na hatimaye, kusafisha mawazo yote ya kishetani na ushawishi kutoka kwenye nafsi ya mtu. Mapambano haya huchukuliwa kama mapambano makubwa (al-Jihaad al-akbar) kana kwamba ni magumu zaidi kuliko mapigano katika uwanja wa vita, kwa ajili ya mapambano dhidi ya nafsi, mtu daima awe katika vita vya maadui ambao ni mwenyeji ndani ya kuwepo kwake. Mafundisho ya Kiislamu ya kimaadili ni kwamba mtu mmoja ambaye amefanikiwa katika harakati hizi anaweza kupanda juu na nje ya ngazi ya malaika, na mmoja ambaye atashindwa katika mapambano haya atashuka kwa kiwango cha chini ya kiwango cha wanyama, na anaweza hata kuwa na makundi kati ya majeshi ya shetani.**

**Hatua ya mapambano dhidi ya ubinafsi**

- Hatua ya 1: kutafakari: Mtu lazima kutenga muda kila siku kutafakari kuhusu majukumu yake kwa Mungu, nani amemwingiza dunia hii, amefanya naye kwa sauti ya mwili na ubongo, na vifaa yake na akili na uwezo, yote ambayo ni vyanzo vya anasa na furaha katika maisha yake. Mungu pia alituma manabii na Kitabu chake Kitakatifu kama njia ya mwongozo na uokovu. Lengo la maisha na madhumuni ya baraka hizi zote ni usikivu zaidi kuliko kufuata tamaa na mwenemdo mbaya ambao ni maisha mafupi na ya muda mfupi. Kifo kinaweza kuja kugonga wakati wowote. Dunia hii ni mahali pa kufanya vitendo vizuri ambavyo matokeo yake ni furaha ya kudumu na kuchukua moja katika nyanja ya juu ya kuwepo. Mtu kwa hiyo kutafakari juu ya hatima yake na maisha yasiyokuwa na matumaini yake katika mikono ya muda na umri kuwa ni kupita. Yeye anatakiwa kujisikia majuto mbele ya Mungu kwa hasara ya miaka ya thamani ya maisha na kwa matendo zamani ambayo kuleta aibu yake juu ya siku ya hukumu. Anapaswa kisha kuanza mapambano yake kwa kupanda juu ya hali hii ya unyonge na kuomba Mungu kwa ajili ya kusaidia ambariki kwa matumaini katika ukweli,, na nguvu ya mapambano dhidi ya maelekeo kishetani na sifa mbaya wa tabia, na kupanda kwa zaidi ya raha na mafanikio ya kidunia vifaa.

- Hatua ya 2: matakwa na utatuzi: Umakini katika ufumbuzi ni asili ya binadamu na mahitaji ya msingi ya kupata uhuru kutoka kwenye utawala wa tamaa mbaya. Nia ambayo inahitajika katika hatua hii ni sawa na kuweka msingi wa maisha bora. Mpiganaji katika vita hivi vya nafsi lazima ajisafishe mwenyewe kutokana na madhambi, afanye matendo yote ya wajibu, aweke nia ya kulipa fidia ya siku alizopotea (katika dhambi), na hatimaye, kufikia ufumbuzi wa kuishi kama mtu wa kidini na binadamu halisi. Tabia yake inapaswa kuiga katika uhai wa Mtume (S), na anatakiwa kumfuata Mtume (s) kutokana na makatazo yote na kufanya aliyoamrisha. Haya yote hayawezi kupatikana isipokuwa kujua Shari 'ah zote na kuzifuata kwa uaminifu.

Hatua ya 3: Uchunguzi binafsi, tathmini na kujikosoa: Baada ya kutoa nadhiri kuwa mtu mwenye nguvu imara na kuazimia hilo, ni lazima kuelewa kuwa Akhera ni mahali ambapo siri yake itakuwa wazi. Hivyo unapaswa kutathmini mwenyewe juu ya kila siku

- kuepuka tabia mbaya na tamaa, na kupata zaidi tabia za watu watukufu, na kufanya vitendo vizuri zaidi kuliko hapo kabla. Ni lazima kutambua kwamba kufanya dhambi hukuweka mbali na utukufu muhimu wa kibinadamu na lazima kuomba kwa Mungu msaada wake na kwa ajili ya maombezi ya Mtume (s) na wajumbe wa nyumba yake (a).

- Hatua ya 4: Kuidhibiti nafsi: ufumbuzi na kujitathmini kutoka hatua za awali lazima kujigawa katika ahadi maalum kwa hali ya kujitegemea. Kwa mfano, mtu ambaye ana tabia mbaya ya tamaa ya macho, kusengenya, au ubinafsi lazima aisemeshe nafsi yake mwenyewe, "mimi si kukiuka sheria ya Mungu leo" na kwa uangalifu aepuke tabia kama hiyo kwa siku moja. Kwa kufanya jaribio hilo kwa na ufumbuzi wa dhati, atakuwa ametambua jinsi kazi hii ilivyorahisi. Anapaswa kumpuuza Shetani na mawazo mabaya ambayo yataikuza kazi hii ndogo na kuwa ngumu au hata isiwezekane. Hivyo, hatua kwa hatua, anaweza kupanua kipindi hiki kwa majaribio na kuona ni jinsi gani ni rahisi kujikwamua na tabia mbaya au kupata sifa chanya.

- Hatua ya 5: Ulinzi dhidi ya maovu: mtu ajitahidi dhidi ya nafsi yake mwenyewe, daima lazima awe makini juu ya nia yake. Kama wakati wowote wazo la kukiuka amri za Mungu limemtokea, yeye anapaswa kujua kuwa dhana hii imekuwa imejikita ndani ya akili yake na Shetani na washirika wake, ambao wanataka kumzuia kutokana na azimio lake zuri. Hivyo, ni lazima awlaani, na kuomba huruma ya Mungu, ulinzi, na kukomesha mawazo hayo mabaya kutoka kwenye eneo la moyo wake. Anatakiwa kumjibu Shetani kuwa siku hizi anatakiwa kujifungamanisha yeye na amri zilizowekwa juu ya nafsi yake mwenyewe kuwa yeye hatakwenda kinyume na amri za Mungu. Hivyo, kwa msaada wa Mungu, Shetani atakuwa ametupwa mbali. Mtu lazima kubaki katika hali hii hii ya akili mpaka usiku wakati wa uchunguzi binafsi na tathmini ya matendo yake ya siku nzima. Huu ni wakati wa kuona kama yeye amekuwa mkweli kwa Muumba wake. Kama yeye alikuwa mwaminifu kwa Mungu, anapaswa kumshukuru. Mtu kama huyo amekwenda hatua moja mbele katika mwelekeo wake na kuwa na tahadhari. Hivyo, Mungu ataendelea kumsaidia katika kutekeleza majukumu yote ya kidunia na kidini, na kupunguza maumivu yake ya mapambano katika siku ya pili. Na kama yeye atarudia zoezi hili mara nyingi, itakuwa desturi ya matendo ya ucha Mungu na kutokomeza tabia mbaya. Yeye azingatie kwamba hahitaji juhudi sana na utii kwa Mungu utampa furaha tele kiroho. Mungu ni msamehevu, kama kuna kupotea kokote kwa upande wake, ni lazima aombe msamaha kwa Mungu, na kwa dhati huashiria kwamba yeye atakuwa makini zaidi katika siku zijazo. Mungu mwenye kurehemu ataacha wazi milango ya neema na huruma kwake, na atamwongoza kwenye njia ya sawa.

Hatua ya 6: Kumbukumbu: Wakati wa safari nzima ya mapambano dhidi ya nafsi, daima mtu anapaswa kukumbuka Mungu na neema toka kwake. Ni lazima kwa kila hatua, kumshukuru daima kutokana na msaada na rehema yake, na uongozi katika kutimiza malengo yake. Shahada ya shukrani kwa Mungu inapaswa kuiongeza ili afike hatua kubwa katika mapambano yake dhidi ya kujitegemea. Ni lazima kutambua kuwa ni kwa sababu ya msaada wa Mungu na majibu ya maombi ya kweli kwamba alikuwa na uwezo wa kujikwamua kutokana na Shetani na washirika wake kutoka uwanja wa moyo wake na kupata sifa tukufu za binadamu na kupendwa na Mungu. [ilichukuliwa kutoka kwa Al-Khumayni, Forty Hadith, ch. 1, 'Jihad al-Nafs']

*...Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya) dhiki, na wazuiayo hasira na wanaosamehe watu, na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao hisani.*
(Qur'an, 3: 134)

Imam Jafar Sadiq (a.s.) amesema:
"Hasira ni ufunguo (unaofungua mlango) wa aina zote za maovu."

[Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 2, Uk. 303, Hadith # 3]

maradhi ya roho...

# Hasira

(*ghadhab)*

Imepokewa kutoka kwa Imam al-Sadiq (a.s.) kwamba alimsikia baba yake Imam al-Baqir (a.s.) alisema: "Bedui mmoja alikwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) akasema: `Mimi naishi jangwani. Nifundishe roho ya busara.' Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: `Nakuamuru usiwe na hasira'. Aliporudia swali lake mara tatu (na kila wakati kupewa jibu hilo hilo na Mtume), yule bedui akajisemea: `Baada ya hapa sitauliza swali lolote, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) haamrishi jambo lolote ila jema'." Imam al-Sadiq (a.s.) amesema: "Baba yangu alikuwa akisema, `Kuna kitu kiovu zaidi kushinda hasira? Hakika, mtu hushikwa na hasira akaua mtu ambaye damu yake imeharamishwa na Mungu, au akamvunjia heshima mwanamke aliyeolewa'."

[Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 2, Uk. 303, Hadith # 4]

## Ushauri wa kutibu hasira

- Mtu mwenye tabia ya kuasirika mara kwa mara ni lazima ajue kwamba hasira ni uwezo aliopewa na Mwenyezi Mungu mtukufu kwa ajili ya kulinda, na kuwapo kwa wanaadamu, na kwa ajili ya kuwa na nidhamu, utaratibu wa kifamilia, kulinda haki za binadamu na sharia za Mungu. Iwapo mwanaadamu atakwenda kinyume na lengo hili la Mwenyezi Mungu na kutumia nguvu ya hasira dhidi ya mpango wa Mwenyezi Mungu, itakuwa ni kukiuka uaminifu ambapo kutastahili adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ni ujinga na dhulma iliyoje kwa kutofanya uaminifu na kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu! Kwa hivyo mtu ni lazima afikirie sana juu ya matendo maovu na ya kikatili yanayosababishwa na hasira, na kujaribu kuondoa yanayosababishwa na uovu, kila moja katika hayo yanayoweza kumsababishia matatizo mtu milele, hapa duniani na adhabu kesho Akhera.
- Moja katika dawa ya hasira ni kujiepusha na sababu zinazoileta. Miongoni mwazo ni ubinafsi, unaofanya kupenda utajiri, ukuu, heshima, tamaa ya mtu kulazimisha apate matakwa yake na kupenda kupanua nguvu ya utawala wake kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Mambo haya kwa kawaida yanachochea moto wa hasira, ambapo wale watu wanaokuwa nayo hupenda kuyatukuza mno. Mtu anapoyapenda mambo haya, huwa ni rahisi kughadhibika ikiwa moja kati ya malengo yake hayajatekelezwa. Sababu nyingine inayoichochea, ni kuwa mara nyingine hasira huchukuliwa kuwa ni sifa na hivyo kuonekana kama ni ushujaa kutokana na kutofahamu kwa mtu. Kwa hivyo hasira ni natija ya udhaifu wa kiroho. Upungufu wa imani, na kutokuwa na tabia na moyo mwema.
- Mtu mwenye hekima hufikiria kwa makini matokea mabaya ya hasira na faida ya kujizuia, na hivyo kumfanya aweze kuutoa moto huu kutoka moyoni mwake kadri awezavyo. Atausafisha moyo wake kutokana na kupenda utajiri, heshima na mengine kama hayo yachocheayo hasira zake. Ikiwa ataweza kujikwamua na ubinafsi na tamaa zake za kidunia, kwa msaada na baraka ya

Mwenyezi Mungu, hupunguza na huupa umuhimu mdogo sababu hizo. Utulivu wake wa moyo wa ndani, utakaoletwa na kutotamani utajiri, heshima au mengineyo, hautaweza kujiruhusu kutotenda uadilifu. Kidogo kidogo ataweza kuhifadhi kujizuia pale hasira inapouchochea moyo wake. Hatimaye, ataweza kufikia kuweza kuitawala kwa ukamilifu hasira yake. [Imenukuliwa kutoka kitabu cha Al-Khumayni, *Forty Hadith*, Sehemu 7, 'Ghadhab']

## Hitimisho

- Imam Jafar al-Sadiq (a.s.) amesema: "**Mumini ni yule ambaye anapokasirika, hasira yake haimpeleki nje ya jambo la kweli**..." [Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 2, Uk. 186, Hadith # 11]

**Kwa maelezo zaidi juu ya Uislamu sahihi, tazama Tovuti:**

***http://al-islam.org/faq/***

## Ukweli wa hasira

Hasira ni hali ya kisaikolojia inayosababishwa na usongo wa ndani na kutaka kulipiza kisasi. Na usongo huu unapozidi sana, ndio unakuza moto wa hasira. Msongamano huo wa nguvu unasonga akili kwa namna ambayo akili na ufahamu unashindwa kumiliki na kuwa dhaifu. Wakati huo, hali ya undani wa mtu inafanana na pango lililowaka moto, na kujaa miale na mawingu yasongayo koo ya moshi unaotoka mlangoni kwake ukiwa na fukuto kali na mvumo mkubwa. Na inapotokea hivyo, huwa ni vigumu kumtuliza mtu kama huyo na kuuzima moto wa hasira zake; chochote kinachotupwa hapo kuupoza, huwa ni sehemu ya moto huo, na kuuzidisha mwako. Na ni kwa sababu hii ndipo mtu kama huyo huwa kipofu na kiziwi wa muongozo wa maadili mema. Katika hali kama hiyo, juhudi zote za ushauri na kumzuia hushindwa kumtuliza mtu huyo. Kadri mtu anavyojaribu kumtuliza kwa maombi na juhudi za unyenyekevu, ndivyo hali ya kutumia nguvu inavyozidi mpaka aumize mtu au alipize kisasi.

- Imam al-Baqir (a.s.) amesema: "..**Kwa hakika, hii hasira ni umeme unaowashwa na shetani ndani ya moyo wa mwanaadamu**.." [Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 2, Uk. 304, Hadith # 12]

### Madhara mabaya na matokeo ya hasira

- Mtu anayekasirika hujifanyia mambo ovyo kama mwendawazimu bila ya kuzingatia natija ya vitendo vyake. Hufanya vitendo vibaya na vichafu, na ulimi wake, na mwili huwa hauwezi kudhibitika.
- Hasira zinaweza kumsababisha mtu kuwatukana mitume na mawalii wa Mwenyezi Mungu, kuzivunjia heshima sehemu takatifu na kubobokwa maneno machafu dhidi wa watukufu, kuua roho yenye kumcha Mungu na isiyo na hatia, kuharibu maisha ya viumbe wa Mwenyezi Mungu, kuharibu familia, au kufichua siri za wengine akizirarua pazia zilizozifunika. Katika matendo hayo ya kikatili hakuna mpaka na vitendo vionevu anavyovifanya mtu wakati huo vinaweza kuharibu nyumba nyingi na jamii nzima.
- Ama kwa upande wa ubaya wa maadili, hasira inaweza kusababisha chuki kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu, na hata mara nyingine kuleta uadui, si kwa mitume na mawalii pekee, bali pia

kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye kuruzuku. Pia inaweza kuzusha maovu mengine, kama vile *hasad* (kijicho), kinyongo na kisasi kisichokuwa na uadilifu.

- Mfano wa hasira duniani hapa ni kama vile moto wa hasira za Mwenyezi Mungu Akhera. Na ni vivyo hivyo kwa hasira itokayo moyoni, pengine ukweli wa kiroho wa hasira hii ni moto wa hasira za Mwenyezi Mungu ambao pia watokana na ndani kabisa ya moyo na kuenea nje, ambapo miale yake mikali huchomoza na kutoka nje ya viungo vya nje kama vile macho, masikio, na ulimi.
- Hasira inayokita daima na kuwa ni sehemu ya maumbile ya mtu ndio janga kubwa. Inaudhoofisha moyo wa mtu, inaufanya usiwe na huruma na kudhuru busara iliyo nayo. Hali atakayoipata mtu huyo katika *barzakh* na siku ya kufufuliwa itakuwa ni ya kinyama zaidi isiyo na kifani katika dunia hii; kwani ukatili wa mtu huyo katika hali hii hauwezi kulinganishwa na aina yoyote ya wanyama wabaya.
- Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) amesema: "Imeelezwa katika Taurat kuhusu Mwenyezi Mungu alivyomwambia Musa (a.s.): "**Ewe Musa! Zuia hasira yako kwa wale ambao nimekupa mamlaka juu yao, ili isikupate hasira Yangu.**" [Al-Kulayni, *al-Kafi*, Juz. 2, Uk. 302, Hadith # 7]
- Imam Ali (a.s.) amesema: "**Jizuie na hasira, kwani mwanzo wake ni wazimu, na mwisho wake ni majuto**." [Al-Amidi, *Gharar ul-Hikam wa darar ul-Kalim*, Hadith # 2635]

## Sifa za kuzuia hasira

- Tabia ya mtu jasiri iko kwenye misingi ya busara na utulivu wa roho. Hukasirika katika mazingira yafaayo, ana subira na hujizuia. Hasira zake huwa zina kikomo maalum, ama kama atalipiza kisasi, huwa ni kwa sababu maalum na hadhari. Yeye anajua vizuri nani amsamehe na na lipi la kulifungia macho na lipi la kulipuuza.
- Hasira za muumini wa kweli huwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Anapokuwa amekasirika, anazingatia wajibu wake, haki za viumbe na hamuonei yeyote. Hatumii lugha chafu wala hakosi adabu. Vitendo vyake vyote huwa kwenye mazingatio ya maana na hufanya kulingana na daraja ya uadilifu na sharia za Mwenyezi Mungu. Siku zote hufanya kwa njia ambayo hatakuja juta baadaye kwa vitendo vyake.
- Imam Ali (a.s.) amesema: "**Mtu aliye na nguvu zaidi ni yule aliyeishinda hasira yake kwa kujizuia.**" [Al-Rayshahri, *Mizan al-Hikmah*, Hadith # 15027]
- Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) amesema: "**Anayezuia hasira zake (kwa mtu), Mwenyezi Mungu atamfichia siri zake.**" [Al-Majlisi, *Bihar al-Anwar* Juz. 73, Uk. 264 Hadith # 11]

## Wakati hasira inapopandishwa…

Moja katika dawa ya hasira inapopandishwa ni kuizuia na kuipoza mapema wakati akili ya mtu bado inaweza kudhibitiwa.

- Imam al-Baqir (a.s.) amesema "..**Yetote atakayemkasirikia mtu, basi na akae chini haraka ikiwa amesimama; kwani, hakika, kwa kufanya hivyo kutamuweka mbali na uchafu wa shetani. Na yeyote atakayemkasirikia mtu katika familia yake, basi na amkaribie na kumgusa (kwa upole); kwani hisia za mshikamano wa udugu zinaposisimuliwa kwa kuguswa, huleta utulivu.**" [Al-Kulayni, *al-Kafi,* Juz. 2, Uk. 302, Hadith # 2]

Imam Ali (a.s.) amesema "**Mtu anapokasirika, akiwa amesimama basi aketi chini haraka kwa muda, kwani kufanya hivyo kunamuondoshea uchafu wa shetani wakati huo.**" [Al-Rayshahri, *Mizan al-Hikmah*, Hadith # 15059]